

TOLEO LA 2.0

# MFUMO WA SAUTI, UCHAGUZI NA MATENDO

## Mwongozo kwa Wahifadhi Kupitia Wazawa na Wenyeji

The Nature Conservancy

# Shukrani

**“Mfumo wa Sauti, Uchaguzi na Matendo (VCA): Mwongozo kwa Wahifadhi Kupitia Wazawa na Wenyeji, Toleo la 2.0”** ni mwendelezo wa msingi wa Toleo la 1.0 (2017). Uliundwa kwa heshima na msaada wa Wazawa na wenyeji duniani kote. Waandishi na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (TNC) wanawashukuru wamiliki wa jadi, walinzi na mawakili wa ardhi na maji ambao Mfumo huu wa VCA unakusudia kuwasaidia, na wale ambao maeneo yao ya kiutamaduni ambayo waandishi wa kutoka maeneo mbalimbali ya kijiografia wamejumuisha wakati wa kuandika ripoti hii.

***Toleo la 1.0 (2017)*** *lilihaririwa na kuratibiwa na Nicole R. DeMello na Erin Myers Madeira. Michango, utaalam, uhariri migawanyo na uchunguzi wa nyenzo na rasilimali, utoaji wa tafiti kifani naMatt Brown, Laurel Chun, Rane Cortez, Eric Delvin, James Fitzsimmons, Herlina Hartanto, David Hinchley, Andrew Ingles, Allison Martin, Patricia Mupeta-Muyamwa, Luke Preece, Helcio Souza na Heather Wishik. Nakala- imehaririwa na Claire Peters. Usanifu umefanywa na Epstein Creative.*

**Nukuu ya pendekezo:** Uhifadhi wa Mazingira (2017). Sauti za Juu,Uchaguzi Makini: Mfumo wa TNC wa Wahifadhi wa Kuimarisha Matokeo kwa Binadamu na Mazingira, Toleo la 1.0. Arlington, VA.

***Toleo la 2.0 (2022)*** *lilihaririwa na kuratibiwa na Nicole R. DeMello. Timu kuu ya uandishi—Nicole R. DeMello, Brandie Farris, Lisa Ferguson, Shiteng Kang (康诗腾), Allison Martin, Yuta J. Masuda, Jessica Musengezi, Luke Preece na Chrissy Schwinn. Utafiti wa kawaida umefanywa na Carol Bogezi, Nicole R. DeMello, Caitlin Doughty, Brandie Fariss, Christina Oraftik, Luke Preece na Geoffrey Whittle-Walls. Michango ya tafiti kifani imefanywa na Colin Apse, Javkhlan Ariunbaatar, Gankhuyag Balbar, Eduardo Barnes, Andrea Akalleq Burgess, Julie A. Damon, Gala Davaa, Eric Delvin, Meghan Gombos, Celene Hawkins, Robert Jones, Luciana Lima, Peter Limbu, Philipo Lukumay, George Maina, Alphonce Mallya, Yedityah Mella, IFPRI na EcoAdvisors. Nakala imehaririwa na Claire Peters. Usanifu umefanywa na Macarena Soto Olivares na kukamilishwa na Wakala MABU.*

**Nukuu ya pendekezo:** Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (2022). Mfumo wa Sauti, Uchaguzi na Matendo: Mwongozo kwa Wahifadhi Kupitia Wazawa na Wenyeji, Toleo la 2.0. Arlington, VA.

**Tunapenda kuwashukuru watu wafuatao kwa miongozo na michango yao:**

**Timu ya Ushauri** ambayo ilitoa mwongozo, mapitio na uhariri wa rasimu—Allison Aldous, Rane Cortez, Erin Myers Madeira, Andrea Akalleq Burgess na Chrissy Schwinn.

**Kikosi Kazi** ambacho kilitoa mawazo, maoni, mifano, mapitio na michango—Awaludinnoer, Javkhlan Ariunbaatar, Fernando Bittencourt, Rony Brodsky, Corissa Busse, Jaime Camacho, Eric Delvin, Rynal Fadli, Natalio Godoy, Berna Gorong, Celene Hawkins, A. Kusworo, Caroline Lumosi, George Maina, Patricia Mupeta-Muyamwa, Alexis Nakandakari, Crystal Nelson, Karen Oliveira, Felipe Torres, Francisco Torres na Sherie Simms.

**Washirika wa Wazawa na Wenyeji** ambao walishiriki katika kusikiliza ili kutoa mitazamo na michango yao kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha sha Mfumo wa VCA—Leah Armstrong, Nikoosh Carlo, tish carr, Kristian Thebu, Darren Ranco na Chrissy Warren.

**Wanachama wa Mtandao wa Wazawa wa TNC** ambao walishiriki katika mazungumzo ili kutoa mitazamo na michango yao ili kuimarisha na kuthibitisha Mfumo wa VCA—Marshall Birch, Faith Cherop, Amy Croover, Caroline Gitari, Sam Gon, Kristina Jenkins, Nohealani Ka'awa, Ericka Moussavou, Crystal Nelson, Cheryl Martinez Thibodeau, Peter Van Kampen, Tracey Williams Ulalia Woodside.

*Ufadhili mkubwa kwa ajili ya Mfumo wa VCA 2.0 ulitolewa na Mfadhili ambaye hakupenda kujulikana*

# Yaliyomo


**Shukrani** ... 3

**Shukrani kwa Wazawa wa Awali** ... 6

**Kanuni Zinazozingatia Washirika** ... 7

**Nini Kipya katika Toleo la Pili?** ... 8

**Utangulizi Kuhusu Mfumo wa Sauti, Uchaguzi na Matendo (VCA)** ... 9

- Wazawa na Wenyeji ... 9
- Uhusiano wa Watu na Mazingira ... 11
- Nadharia Simulizi ya Mabadiliko ... 12
- Uwakilishaji kwa Lugha ya Picha ... 12
- Uwakilishaji wa Mfumo wa CVA kwa Njia ya Picha ... 13
- Nguzo za Mfumo wa VCA ... 14
- Vipengele vya Msingi vya Mfumo wa VCA ... 16
- Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mfumo wa VCA ... 17
- Kuelewa Sifa za Rasilimali za Maji Safi na Maana Zake ... 20

**Mfumo wa VCA: Kuelewa na Kutumia Nguzo na Vipengele vya Msingi** ... 21

**Nguzo ya 1: Kupata Haki za Ardhi, Maji na Rasilimali** ... 22

- Maarifa, Ushahidi na Mazoea ... 22
- Chunguzi Kifani ... 28
- Nyenzo na Rasilimali ... 33

**Nyenzo ya 2: Uongozi Thabiti, Utawala na Uwezo wa Kuongoza** ... 34

- Maarifa, Ushahidi na Mazoea ... 34
- Chunguzi Kifani ... 41
- Nyenzo na Rasilimali ... 44

**Nguzo ya 3: Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali na Kufanya Maamuzi** ........ 45

Maarifa, Ushahidi na Mazoea ........ 45

Chunguzi Kifani ........ 50

Nyenzo na Rasilimali ........ 51

**Nguzo ya 4: Fursa Endelevu za Maisha** ........ 52

Maarifa, Ushahidi na Mazoea ........ 52

Chunguzi Kifani ........ 57

Nyenzo na Rasilimali ........ 59

**Kipengele cha Msingi cha 1: Manufaa, Athari, na Ujumuishwaji Sawa** ........ 60

Maarifa, Ushahidi na Mazoea ........ 60

Chunguzi Kifani ........ 67

Nyenzo na Rasilimali ........ 70

**Kipengele cha Msingi cha 2: Uhusiano Thabiti wa Maarifa na Mahali** ........ 71

Maarifa, Ushahidi na Mazoea ........ 71

Chunguzi Kifani ........ 78

Nyenzo na Rasilimali ........ 81

**Kipengele cha Msingi cha 3: Matokeo ya Kudumu kwa Ajili ya Watu na Mazingira** ........ 82

Maarifa, Ushahidi na Mazoea ........ 82

Chunguzi Kifani ........ 89

Nyenzo na Rasilimali ........ 91

**Kiambatanisho: Rasilimali za Ziada** ........ 92

**Marejeleo** ........ 99

Ili kupata toleo la kisasa la Mfumo wa VCA mtandaoni, tembelea **www.tncvoicechoiceacgion.org**

# Shukrani kwa Wazawa wa Awali

Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (TNC) ni shirika la uhifadhi lililodhamiria kuboresha mustakabali ambapo = watu na mazingira hustawi, na kufanikisha dhima yetu ni lazima tuwe na ujumuishaji, ushirikiano na kuwasaidia wazawa asilia na wa sasa wa mifumo asilia ya Dunia. Tunatambua kuwa kama shirika linalomiliki na kusimamia ardhi, mifumo na kanuni za mali binafsi, ulinzi na usimamizi wa ardhi na maji ambao umekuwa msingi wa kazi yetu uliwagharimu sana Wenyeji. Kwa maneno haya, tunawashukuru wazawa wa jadi, wa zamani, wa sasa na wanaoibuka, na tunaitambua historia yetu ya taasisi, wajibu na dhamira yetu. Tumedhamiria kufahamu kwa kina zaidi historia na athari zinazoendelea za ukoloni—ikiwa ni pamoja na michango yetu wenyewe katika historia hii kama shirika—na majukumu yatokanayo, ikiwa ni pamoja na kujenga ushirikiano kwa kuzingatia heshima, usawa, mazungumzo ya wazi, uadilifu, na uwajibikaji wa pande zote.


© AMI VITALE

# Kanuni Zinazozingatia Washirika

Kazi ya TNC inayofanywa na Wazawa na wenyeji inatokana na kujenga uhusiano, kuheshimu uamuzi binafsi, kujenga uaminifu na kuzingatia maslahi ya pamoja. Kanuni za TNC zinazozingatia washirika ni pamoja na:

- **Kuongozwa na Wazawa na wenyeji:** Tunalenga kuelewa jukumu ambalo jamii ingependa tuwe nalo. Kwa kushirikiana na jamii, tunashirikiana kuweka mipango inayolingana na vipaumbele vya jamii, na uzoefu na dhima ya TNC.

- **Tofauti na jumuishi:** Tunatambua na kuheshimu tofauti za tamaduni za Wazawa na wenyeji, na utofauti uliopo ndani ya jamii. Tunalenga kuweka usawa wa kijinsia na uongozi wa vizazi mbalimbali katika kazi yetu.

- **Msingi wa kunufaishana:** Ushirikiano wetu na Wazawa na wenyeji ni fursa za kujifunza pamoja, kushiriki na kufaidika kati ya jamii na TNC. Tunajitahidi kuleta ushirikiano wa kimabadiliko—wala si wa kuijinufaisha binafsi—kwa msingi wa kutendeana.

- **Kulingana na mawasiliano na uwajibikaji:** Tunasikiliza kwa kina na kufungua njia za wazi za mawasiliano. Tunadhamiria kutimiza wajibu na majukumu tuliyokubaliana, na kuwajibishana kwa ajili ya ushirikiano na dhamira za muda mrefu.

- **Urahisi, uwezo wa kubadilika na uvumilivu:** Tunajitahidi kubadilisha mbinu zetu kulingana na mahitaji, hali halisi, na vipaumbele pinzani ndani ya jamii. Tunatambua uhusiano

Tunadhamiria na kukaribisha mashirika mengine yote ya uhifadhi na washirika kuheshimu na kuzingatia viwango vya haki za binadamu ikiwa ni pamoja na **Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wazawa** na mikataba mingine husika, kutekeleza na kufuatilia ulinzi wa jamii na mazingira, na kuunga mkono ipasavyo utawala, mifumo ya maarifa, na maono endelevu ya kujiamulia ya vizazi vya sasa na vijavyo vya Wazawa na wenyeji.

Tunadhamiria kudumisha na kuheshimu kikamilifu **haki za Wazawa na wenyeji** ambazo ni tofauti na maalum, na kushirikiana kwa kuzingatia maadili shirikishwa, na mbinu bora za kuhakikisha, kwa kadri ya uwezo wetu, kujiwezesha kwa Wazawa na wenyeji, na uongozi na mwongozo wao katika uhifadhi jumuishi na fanisi wa bayoanuai, maendeleo endelevu, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

# Nini Kipya katika Toleo la Pili?

“Sauti za Juu,Uchaguzi Makini: Mfumo wa TNC wa Wahifadhi wa Kuimarisha Matokeo ya Watu na Mazingira, Toleo la 1.0” liliandaliwa kwa pamoja kwa mara ya kwanza na kutolewa mwaka 2017 na kikundi tofauti cha wafanyakazi wa TNC wenye majukumu tofauti na wanaotoka maeneo tofauti ya kijiografia, na kwa kuzingatia uzoefu wa kupanga mipango, utaalam kuhusu mada, na maandiko ya kisayansi. Katika kipindi cha miaka 5 iliyopita, mfumo huu umepata umaarufu na kutumika ndani ya shirika kama mbinu yetu ya pamoja ya kushirikiana na Wazawa na wenyeji kuhusu malengo ya pamoja ya ustawi wa kibinadamu na mazingira. Mrejesho umekuwa chanya, huku kukiwa na ongezeko la uetekelezaji na matumizi. Tangu kuandikwa kwake awali, kumekuwa na tafiti na changanuzi mpya za ndani na nje. Juhudi hizi, pamoja na mabadiliko ya kijamii na kimazingira duniani kote, zimeongeza uelewa na mbinu zetu katika tasnia hii. Sasa ni muda mwafaka wa “kubadilisha” mfumo. Wasomaji watagundua kwamba maudhui mengi zaidi yaliyo kwenye waraka wa awali wa wahifadhi yamebakia, huku yakiwa na marekebisho na nyongeza. Hii ni pamoja na:

- Michango na mapitio ya Wazawa na wenyeji kuhusu mfumo wa nadharia na simulizi, kuhakikisha umuhimu wa nyenzo katika kuendeleza matarajio na maono ya wazawa na wenyeji,
- Kuleta mtazamo kamili wa mifumo asilia kwa kupanua wigo wa mfumo na maudhui husika, lugha, mifano na ushahidi wa kujumuisha na kutumika kwa mifumo ya maji safi na ya ikolojia ya pwani, pamoja na mifumo ya ikolojia ya nchi kavu,
- Nyongeza ya ushahidi na nukuu mpya, na pia nyenzo na rasilimali kutokana na tafiti na vyanzo vya ndani na nje,
- Usasishaji na uboreshaji wa sehemu za “Nyenzo na Rasilimali” ili kujumuisha nyenzo chache zaidi, zinazotekelezeka, ambazo zinaweza kutumika zaidi kwa wahifadhi wanaotekeleza mfumo huu,
- Muunganisho wa wazi zaidi kati ya mfumo na hatua husika za kawaida, na vipimo vya shirika vya TNC, na
- Ongezeko rasmi la vipengele vitatu vya msingi mtambuka ambavyo vinahusu kila nguzo ya mfumo kama masharti muhimu wezeshi kwa ajili ya mafanikio:
    - Manufaa sawa, Athari na Ujumuishwaji,
    - Uhusiano Thabiti na Maarifa na Maeneo, na
    - Matokeo Endelevu kwa ajili ya Watu na Mazingira.

Kadri wahifadhi na mashirika yanavyofanya kazi kutekeleza na kukuboresha dhana hizi za pamoja, ambazo sasa zinajulikana kama **“Mfumo wa Sauti, Uchaguzi na Matendo: Mwongozo kwa Wahifadhi Kupitia Wazawa na Wenyeji, Toleo la 2.0”**—au Mfumo wa VCA kwa kifupi—tunatarajia masasisho haya yatakunufaisha na kwamba yatakusaidia kuendeleza kazi ya uhifadhi ambayo ni muhimu na endelevu. Tunapokua kwa pamoja, kustawi na kukuza mbinu zetu zinazozingatia haki za uhifadhi unaoongozwa na jamii, tunajitahidi kuunga mkononа kuimarisha sauti, uchaguzi na matendo ya Wazawa na wenyeji.

# Utangulizi Kuhusu Mfumo wa Sauti, Uchaguzi na Matendo (VCA)

## Wazawa na Wenyeji

Mfumo wa VCA unatumika zaidi kwa watu ambao:

- wameunganishwa na ardhi, maji, na maliasili ya eneo au mahali pao ikijumuisha uhusiano thabiti unaofanana wa kifamilia na kitamaduni (k.m., lugha, dini, mila, imani, kabila), na desturi zinazofanana (k.m., ukulima, uvuvi, ufugaji ),
- wanategemea mifumo hii kwa mahitaji ya kiuchumi, kifamilia, kitamaduni, kidini na/au kiafya na lishe,
- wana nia ya kubadilisha mustakabali wa kiafya wa viumbehai katika eneo husika,
- wana vielelezo vya kihistoria au kiutamaduni vya kujitawala katika eneo husika, na
- wenye kiwango fulani cha usimamizi wa mali ya kijamii au ya pamoja ya maliasili za eneo husika.

Watu walioelezwa hapo juu wanaweza kukosa fursa za kiuchumi, njia mbadala au ajira, wanaweza kukabiliwa na shinikizo kubwa la maendeleo kutoka nje, wanaweza kuwa na athari zinazoonekana kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri uwezo wao wa kusimamia, kutunza na kutumia maliasili zao, na wanaweza kujumuisha wakazi wa awali wa maeneo na/au watu ambao wamepata makao hivi majuzi na wana uhusiano wa karibu na ardhi, maji na maliasili ya eneo hilo. Wazawa na Wenyeji ni jamii ambazo watu wake wanajumuisha wakazi wa awali wa mahali fulani na hivyo wanajichukulia kuwa tofauti na watu wengine wa jamii ambao pia wanaishi katika maeneo ambayo Wenyeji walimiliki awali kabla ya ukoloni.[1]

### Sifa kuu za Wazawa:

Wazawa, Watu, na Mataifa ni wale ambao, wakiwa na mwendelezo wa kihistoria na jamii za kabla ya uvamizi na kabla ya ukoloni zilizokuzwa katika maeneo yao, wanaojiona kuwa tofauti na sehemu nyingine za jamii zinazoishi sasa katika maeneo hayo, au sehemu yake. Makundi haya hivi sasa yanajumuisha sehemu ndogo za jamii na yameazimia kuhifadhi, kukuza na kusambaza kwa vizazi vijavyo maeneo ya mababu zao na utambulisho wao wa kikabila kama msingi wa kuendelea kuishi kama watu, kulingana na mifumo yao ya kitamaduni, taasisi za kijamii na mfumo wa kisheria (Martinez Cobo 1982). Zaidi ya hayo, tunatambua na kuthibitisha tena kwamba wazawa bila kubaguliwa, wana haki ya kupewa haki zote za kibinadamu zinazotambuliwa na sheria za kimataifa, na kwamba Wazawa wana haki za pamoja ambazo ni muhimu kwa uwepo na ustawi wao, na maendeleo shirikishi kama watu.[2]

## Tofauti za Jamii za Wenyeji:

Jamii za wenyeji mara nyingi zina uhusiano na utegemezi sawia wa ardhi, maji na rasilimali kwa ajili ya utamaduni na maisha yao, pamoja na mifumo ya usimamizi wa maliasili wa jamii au wa pamoja wa maliasili . Hata hivyo, wanachama wa jamii za wenyeji hawajajitambulisha kwa pamoja kuwa Wenyeji. Kwa hiyo, haki za pamoja chini ya sheria za kimataifa zinazopatikana kwa ajili ya Mataifa ya Wazawa huenda zisitumike au kupatikana kwa ajili ya wenyeji. Hata hivyo, tunaendeleza dhamira yetu ya kudumisha haki za binadamu za wenyeji ambazo tunafanana.

Wazawa (IP) na wenyeji (LC) mara nyingi hurejelewa kwa pamoja kama "IPLC" katika mikataba ya kimataifa (k.m., Mkataba wa Anuwai ya Kibayolojia, Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi). Tunatambua tofauti kati ya "IP" na "LC," huku IP zikiwa na haki za pamoja kama zilivyoainishwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Wazawa.[3] Katika nyaraka hii yote, tumejiepusha kutumia kifupi "IPLC" kwa heshima ya tofauti hii kati ya Wazawa na wenyeji na badala yake tunatumia jina kamili na herufi kubwa ifaayo ya "Wazawa" ili kutambua jamii mbalimbali huru ambazo zilikuwa zikiishi katika maeneo mahususi wakati Wazungu walipojaribu kuzitaja, kuziainisha na kuzitawala kwa mara ya kwanza.

Wazawa na wenyeji ni viongozi muhimu katika shughuli ya kutafuta majawabu ya kudumu kwa changamoto kubwa zaidi za kimazingira na ustawi wa binadamu duniani. Wanasimamia au wana haki ya kumiliki zaidi ya asilimia 25 ya ardhi ya dunia nzima[4] na zaidi ya mara mbili ya ardhi inayodaiwa lakini ambayo haijatambulika kisheria,[5] ikijumuisha mifumo iliyoingiliana ya misitu, nyika, ardhi oevu, mito, maziwa, maji ya chini ya ardhi na pwani. Huku maeneo yao yakiwa na zaidi ya asilimia 24 ya hewa ya ukaa inayotokana na misitu ya kitropiki[6] kote duniani na kiasi kikubwa cha bayoanuai[7] duniani, na huku wavuvi tisa kati ya 10 kati ya wavuvi milioni 32 duniani kote wakiwa wavuvi wadogo,[8] Wazawa na wenyeji ni miongoni mwa washirika wetu ambao ni muhimu zaidi, na wamejidhihirisha kuwa mawakili wazuri zaidi wa mazingira kote duniani—huku wakipata matokeo makubwa zaidi ya uhifadhi na kudumisha bayoanuwai zaidi ya maeneo yanayohifadhiwa na serikali. [9-10]

Wazawa na wenyeji wanakabiliwa na changamoto za kuwa na jamii na mazingira yenye afya na ustawi kutokana na alama na kuendelea kwa vitendo vya ukoloni, mwendelezo wa ukosefu wa usawa, na kuongezeka kwa kujilimbikizia uwezo wa kiuchumi. Kupanuka zaidi kwa dhana hii, wakati mamlaka na uwezoa wa Wazawa na wenyeji za kusimamia ardhi, maji na rasilimali zao unapoimarishwa, wakati fursa za maisha zinapoendana na tunu zao, na wakati fursa na manufaa haya yanagawanywa kwa usawa, basi majawabu ya kudumu kwa ajili ya watu na mazingira yatapatikana. Kwa hiyo, tunashirikiana ili kuunga mkono usimamizi na uwakili wa maliasili unaofafanuliwa, unaoongozwa na kutekelezwa na Wazawa na wenyeji; uliojikita katika tunu za jamii, maarifa, na mitazamo; na kulenga masuala fungamanishwa ya kusaidia jamii hai, tamaduni thabiti, uchumi unaowezekana wa ndani, na mifumo mizuri ya kiikolojia.

---

a. Kwa kuzingatia muktadha wa Mfumo wa VCA, mamlaka inafafanuliwa kama mtazamo wa watumiaji wa maliasili na wenye haki ya umiliki ambao kundi la kiutawala linawakilisha maslahi yao kwa uaminifu, na lina mamlaka ya kisheria au ya kimila ya kutawala maliasili "zao"[11]. Uwezo ni dhana yenye vipengele vingi inayodhaniwa kwa ujumla kuwa "yenye uwezo wa kutenda," na aina mbalimbali za mitaji ikiwa ni pamoja na mtaji wa rasilimali watu, kijamii, kitaasisi, kiasili na kiuchumi lazima zitumike kufanya hivyo.[12-13]

# Uhusiano wa Watu na Mazingira

Mfumo wa VCA umejikita katika kuelewa kwamba afya ya ulimwengu asilia na ustawi wa watu ni vipengele vilivyounganishwa bila kutenganishwa. Hali hii inazidi dhana ya ya huduma za mifumo ya kiikolojia (yaani, utoaji, udhibiti na utendakazi saidizi ambao mazingira huwapa watu) kwa mtazamo kamilifu unaojumuisha uhusiano mbalimbali na wingi wa maoni katika mfumo wa kijamii na kiikolojiab (Mchoro wa 1).

Katika kielezo kilicho hapa chini, njia ya bluu inawakilisha njia moja ambayo mikakati ya uhifadhi wa mazingira inasababisha mabadiliko katika uadilifu wa mfumo wa kiikolojia—na baadaye huduma za mfumo wa kiikolojia—ambayo baadaye huathiri ustawi wa binadamu. Hii ndiyo njia inayotambulika na kurejelewa zaidi baina ya mashirika ya uhifadhi. Njia nyingine, ambayo ni muhimu pia katika uhifadhi unaoongozwa na jamii, inawakilishwa na njia ya rangi ya chungwa-mipango hujihusisha na mikakati ya uhifadhi yenye mwelekeo wa kijamii (k.m., kujenga uwezo, maisha endelevu, n.k.) ambayo husababisha mabadiliko ya kijamii, ambayo huathiri moja kwa moja usitawi wa binadamu na uadilifu wa kiikolojia. Wakati huo huo, ustawi wa watu huathiri uwezo wao, uthabiti na nia yao ya kushiriki katika shughuli za uwakili, kama inavyoonyeshwa na njia ya kijani.. Mwisho, mahali ambapo kuna uhusiano wa kina na ardhi, maji na rasilimali, mtazamo wa watu kuhusu afya ya maeneo hayo unaweza kuathiri moja kwa moja afya na utambulisho wao (njia nyekundu).




**Mchoro wa 1:** *Mchoro wa uhusiano wa mazingira na watu*[14]

b. Mfumo wa kijamii na kiikolojia unarejelea dhana jumuishi ya binadamu katika mazingira, na inasisitiza uhusiano kati ya mazingira asilia na mifumo ya kijamii inayoshughulikia haki za mali, mifumo ya umiliki wa rasilimali, mifumo ya maarifa inayohusiana na mazingira na rasilimali, na maoni na maadili ya ulimwengu. kuhusu mazingira na rasilimali.[15]

# Nadharia Simulizi ya Mabadiliko

Mbinu yetu ya kawaida ya kuunga mkono mamlaka ya Wazawa na wenyeji katika usimamizi wa maliasili na kufanya maamuzi ni Mfumo wa VCA. Mfumo wa VCA unakusudiwa kutumika katika hali ambapo kuna mwingiliano na kutegemeana kati ya ustawi wa binadamu na matokeo ya mazingira, ambapo uongozi wa Wazawa na wenyeji ni muhimu katika kufikia malengo ya pamoja, ambapo kukoseakana kwa usawa wa mamlaka kunaweza kukwamisha kufikia matokeo chanya kwa ajili ya watu na mazingira, na ambapo miradi inaweza kuathiri wenyeji kwa kiasi kikubwa.

Matokeo chanya ya usawa na endelevu kwa watu na mazingira kwa ujumla yanahitaji uwepo wa Mfumo wa VCA wa kutegemeana na kuimarisha nguzo nne na vipengele vitatu vya msingi (Mchoro wa 2). Nguzo nne za mfumo (haki, uwezo, kufanya maamuzi na mstakabali) zinawakilisha sifa zinazohitajika kwa mafanikio ya uhifadhi unaoongozwa na jamii. Kwa kweli, ukaguzi wa hivi karibuni wa utaratibu na uchambuzi unapendekeza kwamba kadri nguzo hizi nne zinavyopatikana, kuna uwezekano mkubwa wa matokeo ya pamoja ya kimazingira na kijamii na kiuchumi yenye mafanikio kuibuka.[16] Vipengele vitatu vya msingi (usawa, maarifa na mahali, na uimara) vinawakilisha hali muhimu zinazowezesha uhifadhi unaoongozwa na jamii.

Kutokana na hali ya kutegemeana ya Mfumo wa VCA, hatumaanishi kuna utaratibu maalum wa nguzo na vipengele vya msingi. Vipengele vyote vinahitajika kwa ajili ya matokeo chanya endelevu kwa watu na mazingira, na vipengele vingi mara nyingi hutekelezwa kwa wakati mmoja. Zaidi ya hayo, muktadha (k.m., uwezo uliopo wa jumuiya, sera ya mamlaka na taasisi, aina ya mfumo wa kiikolojia, vichochezi vya mabadiliko, historia, n.k.), kutokana na uchanganuzi wa kina wa hali, utaamua kipengele/vipengele vya kipaumbele katika mkakati wa mradi.

# Uwakilishaji kwa Lugha ya Picha

Mchoro huu unawakilisha **kasa**, ambaye ni kiumbe kinachonawiri katika mazingira yote makuu.Kasa pia ni kipengele maarufu cha hadithi za uumbaji za Wazawa wengi. Turubai linafanana na **ngoma ya kupiga kwa mkono**, ambayo inaashiria mapigo ya moyo ya ulimwengu. Katika tamaduni nyingi za Wazawa, ngoma ya kupiga kwa mkono ni chombo kitakatifu kinachounganisha mbingu na dunia, huku pia kikidumisha mpangilio wa mapigo wa ulimwengu.

Nguzo nne (4) zimeungana mithili ya miguu ya kasa. Alama ya nyayo za **dubu** ni ishara ya ulinzi, nwakati Mianga ya Kaskazini inayoizunguka ni ishara ya uhusiano wa milele na mababu zetu. **Mwewe** anatambulika sana kama ishara ya uongozi.Nao **moto** ni ishara ya mahali pa kukusanyikia na umezungukwa na miale inayocheza ambayo ni ishara ya watu wanaozungumza kwa pamoja. Mwisho, **jua** ni ishara ya uzima wa milele, na miale ya mwanga inayotoka humo inawakilisha furaha, nishati na uchangamfu.

Vipengele vya msingi vimeungana katika mfumo wa picha wakilishi katika maeneo matatu (3) tofauti kwenye mgongo wa kasa. Sehemu hizi zimetenganishwa na alama za maji ambazo zimeunganishwa katikati na **kitanzi kitakatifu**. Kitanzi kitakatifu, ambacho wakati mwingine hujulikana kama gurudumu la dawa, ni ukumbusho kwamba vitu vyote vinahusiana, na vitu vyote viko katika mchakato unaoendelea wa ukuaji na maendeleo.

Kichwa cha kasa kinajengwa kwa vipengele vya maji yanayotiririka, vinavyowakilisha safari ya maisha. Kwa asili yake, kichwa kinawakilisha hekima, wakati moyo ulio chini yake unaonyesha namna kimeungana na moyo na nafsi.

# Uwakilishaji wa Mfumo wa VCA kwa Njia ya Picha

**"Nguzo na vipengele VYOTE vya msingi vinahusiana na kutegemeana, na vinahitajika kwa matokeo chanya ya kudumu kwa ajili ya watu na mazingira"**




**Mchoro wa 2:** *Uwakilishaji wa Mfumo wa VCA kwa Njia ya Picha*

# Nguzo za Mfumo wa VCA



NGUZO YA 1:

## Upatikanaji wa Haki za Ardhi, Maji, na Rasilimali

Inarejelea hali halisi ya kisheria na vile vile mtazamo wa Wazawa na wenyeji kwamba haki zao za ardhi, maji na rasilimali zitazingatiwa na wanajamii wengine, ikiwa ni pamoja na jamii za nje, mashirika na serikali. Inategemea aina (k.m., umiliki, usimamizi, kujitoa, matumizi, au upataji) na muundo (k.m., za jumuiya, za umma, au za binafsi) wa haki zinazoshikiliwa, na kutambua na kutekelezwa kwa haki na taasisi za kitamaduni na rasmi. Wazawa na wenyeji wanapopata haki juu ya ardhi, maji, na rasilimali ambazo zinatambuliwa na kutekelezwa na jamii na serikali, wanaweza kusisitiza maslahi yao kwa jinsi rasilimali hizi zinavyotumiwa na kusimamiwa. Matokeao yake, hii inaweza kusababishausalama imara wa jamii na ushirikishwaji katika usimamizi wa maliasili na matumizi endelevu ya maliasili, hasa wakati jamii inapokuwa na maadili safi ya uwakili, miundo thabiti ya utawala, uongozi unaowajibika, na fursa za kiuchumi ambazo zina uhusiano wa karibu na uwakili wa mazingira na usimamizi endelevu wa rasilimali.



NGUZO YA 2:

## Uongozi Thabiti, Utawala, na Uwezo wa Kusimamia

Inarejelea uwezo mbalimbali wa Wazawa na wenyeji kuongoza katika kufanya maamuzi kuhusu ardhi, maji na rasilimali; kudumisha sheria na taratibu zilizo wazi na za usawa za usimamizi wa maliasili; na ujuzi, maarifa, na teknolojia ya kushiriki katika majukwaa, kusimamia biasharana fedha, na kusimamia mifumo asilia. Wazawa na wenyeji wanapokuwa na watu binafsi, viongozi na taasisi zenye uwezo mkubwa, wanaweza kufikia hatua ya pamoja, mshikamano wa kijamii na utawalabora unaohitajika kwa usimamizi endelevu wa maliasili; kukabiliana na vitisho vya nje kwa ardhi, maji, na rasilimali; kufuata, kutekeleza, na kutetea haki zao; kuendeleza fursa za namna ya maisha iliyo endelevu; na kushiriki katika kufanya maamuzi ambayo yana athiri kwa ardhi, maji na rasilimali wanazozitegemea.



NGUZO YA 3:

## Mazungumzo yenye Ufanisi ya Wadau Mtambuka na Kufanya Maamuzi

Inarejelea uwezo wa Wazawa na wenyeji kupanga au kuhudhuria, kutoa mawazo na maarifa, na kuona mawazo na matamanio yao yanatumika kwenye majukwaa ambayo huwaleta pamoja watendaji wengi wenye maslahi katika ardhi, maji, au rasilimali. Majukwaa haya yanaweza kutumika katika ngazi ya mtaa, kanda, taifa, au kimataifa, yanaweza kuingiliana kimajukumu au kimamlaka, na yanaweza kuwa na malengo ya kubadilishana ujuzi, kutatua migogoro, na/au kufanya maamuzi. Wazawa na wenyeji wanaposhiriki kwa ufanisi na kwa kudhamiria katika mazungumzo na kufanya maamuzi ya wadau mbalimbali,na miundo endelevu inapoanzishwa ili kudumisha ushirikiano huo, maamuzi ya usimamizi wa maliasili huakisi vyema mitazamo mbalimbali ya uendelevu, kujumuisha maarifa ya kipekee kuhusu usimamizi na uthabiti, na kufaidika kutokana na uelewa wa hali ya juu wa kuhusianishwa kwa watu na mazingira. Zaidi ya hayo, Wazawa na wenyeji wenye haki ya umiliki wanafaidika kutokana na kuongezeka kwa sauti na mwonekano, nafasi thabiti wa majadiliano ili kuendeleza maono yao ya mafanikio ya kiuchumi, na kuwekeana usawa kwenye uwezo.



NGUZO YA 4:

## Fursa Endelevu za Maisha

Inarejelea uwezo wa Wazawa na wenyeji kutafuta fursa za maisha zinazoendana na utamaduni (k.m., kuongeza thamani au uthabiti kwenye maisha ya sasa, kubuni njia mpya za mustakabali au biashara zinazoimarishwa kupitia upataji wa mikopo, na ufadhili mwingine, au kupata ajira au fidia kwa ajili ya uwakili mwema) zinazoendana na maono yao ya siku zijazo na kuwawezesha kustawi mahali walipo. Wazawa na wenyeji wanapopata fursa endelevu za maisha kwa mazingira na zinaendana na utamaduni, wanaweza kusisitiza maslahi yao ya kimazingira na kiuchumi huku wakidumisha msimamo thabiti wa majadiliano dhidi ya uchaguzi wa maendeleo usio endelevu unaoharibu mazingira na ambao hauendani vyema na maadili ya kiutamaduni.

# Vipengele vya Msingi vya Mfumo wa VCA



KIPENGELE CHA MSINGI CHA 1

## Faida endelevu, Athari, na Ujumuishaji

Inarejelea uwezo wa Wazawa na wenyeji, na watu wengine tofauti walio kwenye jumuiya, kufaidika kwa usawa kutokana na ushirikiano, kuongeza athari chanya na kupunguza athari hasi (hasa kwa utambulisho wa jamii zenye maisha duni au uwakilishi mdogo), na kufikia ushiriki sawa katika uamuzi, mafunzo, na fursa za kiuchumi. Wazawa na wenyeji, na watu wengine tofauti walio kwenye jumuiya, wanapoweza kushiriki na kufaidika kwa usawa kutokana na mipango ya uhifadhi, shughuli za uwakili huimarishwa na mitazamo ya kipekee na maarifa ya wanajamii tofauti na athari ya muda mrefu ya maamuzi na vitendo vya kijamii huongezeka, na kusababisha matokeo bora kwa watu na mazingira.



KIPENGELE CHA MSINGI CHA 2

## Uhusiano Madhubuti wa Maarifa na Mahali

Inarejelea kuendelea kuwepo, matumizi, na uenezaji wa maarifa, lugha, utamaduni, masimulizi na desturi za jadi za Wazawa na wenyeji ambazo ni muhimu kwa ustawi wao, na ndio msingi wa mafanikio ya usimamizi wao wa maliasili, uongozi na maisha yao. Wazawa na wenyeji wanapoweza kudumisha, kufufua, kuimarisha, kutumia, na kueneza maarifa yao—ambayo mara nyingi yanatokana na wakati, utamaduni, na mahali—wana uwezo bora zaidi wa kuweka maamuzi ya usimamizi wa maliasili kwenye kanuni za kunufaishana, na kuhakikisha vizazi vijavyo vinaweza kufaidika kutokana na njia za jadi za kutambua maarifa na maisha.



KIPENGELE CHA MSINGI CHA 3

## Matokeo Endelevu kwa ajili ya Watu na Mazingira

Inarejelea masharti wezeshi ya nje yanayoathiri mafanikio ya muda mrefu ya uwakili unaoongozwa na jamii, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa fedha za uhifadhi ili kufadhili gharama za muda mrefu za uendeshaji na usimamizi; mazingira mazuri ya kisera ya mtaa, kikanda, kitaifa na kimataifa; na uenezaji wa mawazo mapya kupitia mitandao na kuongeza bila kuathiri tunu.Wazawa na wenyeji wanapopata fedha ambazo hulipa gharama kamili ya shughuli za uwakili; taasisi nzuri za serikali zinazoinua haki zao za pamojana ushiriki katika kutunga sera; na uwezo wa kufikia kiwango kinachohitajika cha athari kupitia upanuzi, uigaji, na uenezaji wa mifano ya mafanikio ya uhifadhi unaoongozwa na jamii, jitihada zao za kuishi kwa raha mahali wana uwezo mkubwa wa kufikia uendelevu wa muda mrefu wa kijamii, kiuchumi na wa kimazingira.

# Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mfumo wa VCA

> Angalia **"Nyenzo ya 1: Nyaraka ya Mwongozo wa Mfumo wa VCA"** kwa mwongozo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfumo wa VCA

Tuliandaa mbinu ya ufuatiliaji, tathmini na mafunzo (MEL) ili itumike kwenye mipango inayotekeleza Mfumo wa VCA, inayojumuisha vipimo vya kawaida. Vipimo hivi hurahisisha uwezo wetu wa kuzungumzia matokeo katika mipango na maeneo tofauti kwa mujibu wa ushahidi, kujenga msingi wa ushahidi wa mikakati ya uhifadhi yenye mwelekeo wa kijamii, kukuza mafunzo ya pamoja, na kuwezesha usimamizi himilivu. Mbinu hii inalenga kupata uwiano kati ya uthabiti na unyumbufu—kwa hatua 10 za kawaida za kiwango cha matokeo na uwezo wa kuchagua kutoka kwenye menyu ya viashirio mahusus vya muktadha ili kuvibainisha. Vipimo vitano kati ya 10 vya kawaida hufungamana moja kwa moja na vipimo vya shirika la TNC (vinavyoonyeshwa kwa kutumia kinyota katika Jedwali la 1), na hivyo basi hutoa fursa ya kuongeza majawabu na athari za juhudi za ufuatiliaji. Jedwali la 1 linaonyesha Vipimo vya kawaida vya VCA pamoja na nguzo ya VCA inayohusishwa au kipengele cha msingi.

**Jedwali la 1:** *Vipimo vya VCA.*

| Nguzo ya Mfumo wa VCA au Kipengele cha Msingi | Vipimo vya VCA |
|---|---|
| Kupata Haki za Ardhi, Maji, na Rasilimali | *1) Idadi ya watu walio na haki nyingi juu ya ardhi ya jadi, maji, au rasilimali |
| Uongozi Thabiti, Utawala, na Uwezo wa Kusimamia | 2) Idadi ya watu walio na uwezo mkubwa wa utawala<br><br>3) Idadi ya watu walio na uwezo mkubwa wa usimamizi wa raslimali |
| Mazungumzo Thabiti ya Wadau Mtambuka na Kufanya Maamuzi | *4) Idadi ya watu walio na uwezo mkubwa wa kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi ya ardhi ya jadi, maji, au rasilimali |
| Fursa za Namna ya Maisha Iliyo Endelevu | *5) Idadi ya watu walio na fursa kubwa endelevu za kiuchumi za mahali fulani |
| Faida endelevu, Athari, na Ujumuishaji | Mazingatio ya usawa yanapendekezwa kwa kila kipimo (angalia sehemu tofauti za **jarida la mongozo**) |
| Uhusiano Madhubuti wa Maarifa na Mahali | 6) Idadi ya watu walio na uhusiano mkubwa wa maarifa na mahali |
| Ardhi, maji au rasilimali bora za kitamaduni na endelevu[c] | *7) Idadi ya hekta za ardhi au maji/kilomita za mto/kilomita za ukanda wa pwani unaohifadhiwa<br><br>*8) Idadi ya hekta za ardhi au maji/kilomita za mto/kilomita za ukanda wa pwani ulio chini ya usimamizi ulioboreshwa<br><br>9) Idadi ya hekta za ardhi au maji/kilomita za mto/kilomita za ukanda wa pwani wenye hali ya kiikolojia iliyoboreshwa<br><br>10) Idadi ya hekta za ardhi au maji/ kilomitaza mto/kilomita za ukanda wa pwani wenye maboresho ya maeneo au spishi muhimu za kitamaduni |

**Vipimo vya VCA vilivyo na alama ya kinyota vinafanana kabisa na vipimo vya shirika la TNC.*

c. Kumbuka, ingawa "ardhi, maji, au rasilimali za kijadi zenye afya na zinazosimamiwa kwa uendelevu" si nguzo ya Mfumo wa VCA, ni matokeo ya wazi ya mfumo huu, na inahusishwa kwa karibu na ustawi wa Wazawa na wenyeji. Kwa hiyo, tunajumuisha vipimo hivi ili kuelewa athari ya mikakati yetu kwa mazingira.

## NYENZO YA 1: NYARAKA YA MWONGOZO WA MFUMO WA VCA

Kadiri Mfumo wa asili wa VCA ulivyozidi kufana katika programu zote, tulipata wito kutoka kwa wahifadhi wa mwongozo rahisi, wa kawaida, unaoweza kubadilika, na unaoweza kutumika wa kufuatilia matokeo yanayotokana na utekelezaji wa Mfumo wa VCA. Kwa kuzingatia mwelekeo wa mfumo kwenye mikakati inayoelekezwa kijamii inayotokana na watu/uhusiano wa asili, na kuungwa mkono kwa ushahidi unaoongezeka, mwongozo huu unaweka mkazo katika kufuatilia viashiria vya ustawi wa binadamu pamoja na mazingira. Mwongozo huo unakusudiwa kuunganisha kwa uwazi **Ajenda ya Uhifadhi ya TNC (SCA)** na **Uhifadhi kwa Usanifu 2.0**, na kusaidia mipango inayopitisha Mfumo wa VCA kutoa maelezo ya kufuatilia maendeleo yao kwenye ustawi wa binadamu na matokeo juu ya mazingira ili kuelekeza juhudi pana za TNC.

Zaidi ya hayo, **mtaala wa mafunzo ya mtandaoni unaoamua kasi yake binafsi kuhusu Ufuatiliaji, Tathmini, na Mafunzo ya Mfumo wa VCA (MEL)** unapatikana kwenye **conservationtraining.org**, unaojumuisha uundaji wa mpango wa MEL; maadili, haki za binadamu, na usawa katika MEL; kikundi lengwa na muundo wa usaili wa watoa taarifa wakuu; muundo wa uchunguzi wa kijamii; nyenzo za kukusanyia data na utekelezaji; mifumo na taratibu za usimamizi wa data; na uwasilishaji wa data na mawasiliano. Ili kupata mtaala wa mafunzo, wasiliana na **conservationtraining@tnc.org.**

“Nyenzo na Rasilimali” zote zilizorejelewa ndani ya nyaraka hili zinapatikana kupitia **www.tncvoicechoiceaction.org**


© BRIDGET BESAW

## Kuelewa Sifa za Rasilimali za Maji Safi na Maana zake

Mfumo wa VCA uliandikwa ili utumike katika mazingira ya nchi kavu, maji safi na kwenye mifumo ya kiikolojia ya pwani. Rasilimali za maji safid zina sifa fulani za kipekee ambazo haziendani namifumo ya kiikolojia ya nchi kavu au pwani. Kufahamu sifa za kipekee za rasilimali za maji safi ni muhimu katika kuelewa tofauti ndogo ndogo za jinsi ya kutumia vema mfumo.

**Uwezo wa Kuhamishika:** Rasilimali za maji safi kwa asili zinaweza kahamishika, na hivyo kujenga uwezekano wa utofauti mkubwa katika mtiririko na upataji wa rasilimali kwa nafasi na wakati, na kuongeza kasi ambayo hueneza athari kwa rasilimali. Kwa kuongezea, kutokana na uhamaji huu, muunganiko ni muhimu kwa spishi na taratibu nyingi. Kwa hiyo usimamizi wa rasilimali za maji safi lazima uwe himilivu kwa sababu upataji hubadilika kadri muda unavyopita, na inaweza kuwa ghali kufanya rasilimali za maji safi zipatikane wakati na mahali zinapohitajika na watu.

**Athari juu ya ubora na kiasi:** Hali ya rasilimali za maji safi katika eneo moja huakisi athari limbikizi za matumizi yote ya maji kwenye maji na kwenye nchi kavu katika maeneo yaliyopo juu ya mito (ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, utengenezaji wa bidhaa, uzalishaji wa umeme na usafirishaji) na utawala katika maeneo ya juu ya mito, pamoja na hali za tabianchi na mambo mengine. Kwa hiyo, kuwepo kwa maji kwa watumiaji wa maeneo yaliypo chini ya mto—na ubora wa rasilimali hiyo ya maji—haujathibitishwavc, mara nyingi kwa muda mfupi sana kati ya sababu na matokeo kutokana na uhamaji mkubwa wa maji. Zaidi ya hayo, mbinu ya usimamizi wa rasilimali za maji safi inaweza kutofautiana kulingana na mahali mmoja alipo kwenye mkondo wa mto.

**Changamoto za uchunguzi:** Mara nyingi, ni vigumu kuchunguza na kufuatilia rasilimali za maji safi (k.m., maji yaliyo chini ya ardhi, hifadhi ya samaki wanaohama), jambo ambalo huleta changamoto kubwa katika kukuza uelewa sahihi wa rasilimali hizi, kuweka mipaka kuhusu haki na utawala, na kutoa maoni ambayo watumiaji huhitaji ili kuzihifadhi. Hii ni changamoto hasa kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

**Hasara isiyojulikana:** Hasara isiyojulikana—au gharama/faida ambazo hazijaonyeshwa katika bei inayotozwa kwa bidhaa na huduma—huchangia na kuathiri mienendo ya nguvu miongoni mwa watumiaji wa rasilimali za maji safi. Kuwa kwenye maeneo ya juu ya mto huwa na faida fulani kuliko kuwa kwenye maeneo ya chini ya mto, na ukosefu wa usawa wa nguvu huchangia kukabiliana na au kuzidisha mienendo hii. Hili limekuwa suala zito katika mifumo mingi ya maji mipakani, ambapo watumiaji wa maeneo ya juu ya mto wametengeneza miundombinu na kuelekeza rasilimali za maji mbali na vijito au mito, na kuwaacha watumiaji wa maeneo ya chini ya mto na maji kidogo na mtiririko unaobadilika badilika. Migogoro kama hiyo inaongezeka wakati kuna uhaba mkubwa wa maji, kama vile kutokana na ukuaji wa haraka wa idadi ya watu, mabadiliko ya tabianchi, na machafuko.

**Isiyo na mbadala na ni muhimu:** Hakuna mbadala wa maji safi—ni muhimu kwa viumbe vyote duniani. Kwa kuzingatia hadhi yake kama haki ya msingi ya binadamu, ni nadra sana kwa watu kuwa na haki za kumiliki maji. Badala yake, aina za haki zinazotumika zaidi zinazohusiana na maji safi ni upataji, uondoaji na utengwaji (pata maelezo zaidi katika sehemu ya "haki salama"). Maji ndio kichocheo cha sekta nyingi za kiuchumi (k.m., kilimo, uzalishaji wa nishati, utengenezaji wa bidhaa) na hivyo, usambazaji na usimamizi wake mara nyingi huwa na utata.

d. Mifumo ya ikolojia ya maji safi ni pamoja na maji yaliyo chini ya ardhi na chemchemi, mito na vijito, maziwa na madimbwi, na maeneo oevu. Neno "rasilimali za maji safi" linamaanisha maji yenyewe kama rasilimali, pamoja na viumbe vya majini vinavyoishi ndani ya maji.

# Mfumo wa VCA: Kuelewa na Kutumia Nguzo na Vipengele vya Msingi

Sehemu hii inaelezea maarifa na ushahidi unaotegemeza Mfumo wa VCA, jinsi unavyotumika, na seti ndogo ya nyenzo na rasilimali zinazoweza kutekelezeka ambazo zimeratibiwa kama ufunguo wa kusaidia katika utekelezaji wa Mfumo wa VCA. Inaanza kwa nguzo nne, ikifuatiwa na mambo matatu ya msingi. Nguzo za mfumo (haki, uwezo, kufanya maamuzi, na namna za maisha) zinawakilisha sifa zinazohitajika kwa mafanikio ya uhifadhi unaoongozwa na jamii. Vipengele vya msingi (usawa, maarifa na mahali, na uwezo wa kudumu) yanawakilisha mazingira wezeshi yaliyo muhimu kwa uhifadhi unaoongozwa na jamii. Kila sehemu ya nguzo na kipengele cha msingi kinajumuisha vipengee vidogo vya "Maarifa, Ushahidi, na Mazoea," Chunguzi Kifani," na "Nyenzo na Rasilimali." Maelezo haya yametolewa kutoka kwa mhifadhi na uzoefu wa programu, ujuzi na uzoefu wa Wazawa na wenyeji, wataalam wa mada hii na machapisho ya kisayansi. Nukuu na marejeleo yanaweza kutumika katika kuunga mkono na kuelezea umuhimu wa mbinu ya kimkakati inayosaidia kama ushahidi na uzoefu ili kusaidia mamlaka na uwezo wa Wazawa na wenyeji katika usimamizi wa maliasili na kufanya maamuzi kwa viongozi, wafadhili, mashirika, na washirika. Wahifadhi wanaweza kupata nyenzo na rasilimali zilizoangaziwa kuwa muhimu katika hatua yoyote ya maendeleo ya mradi—kutoka kwa kupanga na uchambuzi wa hali; hadi utekelezaji; ufuatiliaji, tathmini na mafunzo.

Tunakubaliana kwamba ushahidi unaotolewa katika sehemu zinazofuata unategemea zaidi sayansi ya Mataifa ya Magharibi na unaweza kugawanya na kurahisisha mahusiano changamano na mienendo kati ya watu na mazingira katika maeneo mahususi ambayo huunda mifumo inayostawi na imara kwa kipekee. Ndani ya jamii nyingi za Wazawa na wenyeji, uendelevu ni matokeo ya njia za maisha zinazotokana na jukumu na wajibu wa wanadamu katika kudumisha usawa wa maisha yote,[17] ambayo kimsingi inakinzana na uainishaji unaohusishwa na sayansi ya Mataifa ya Magharibi. Katika muktadha wetu wa sasa, tunatambua kuwa kazi ya uhifadhi unaoongozwa na jamii bado ipo ndani ya jamii ambapo mawazo ya sayansi ya Mataifa ya Magharibi huwa msingi wa maamuzi na kanuni za mazingira katika ngazi ndogo na kubwa. Maarifa Asilia na sayansi ni mfumo mzima wa maarifa ndani na yenyewe, sawa na mengine yote.[18] Matokeo yanayotarajiwa kutokana na kutumia mchanganyiko wa sayansi ya Mataifa ya Magharibi ni kuwasaidia wahifadhi ambao wanatumia njia nyingi za kupata maarifa na kuepuka kutegemea maarifa ya sayansi ya Mataifa ya Magharibi pekee, ili kupanua njia za kupata maarifa kuhusu uhifadhi. Sehemu hii inakusudiwa kuwasaidia watu wanaopata maarifa kutoka pande zote, kwa kutumia nyenzo za mfumo wa maarifa wa Mataifa ya Magharibi pamoja na maarifa Asilia na njia nyinginezo za kupata maarifa.

Kwa nyongeza, TNC imedhamiriankuzingatia mfumo unaotegemea haki za binadamu katika uhifadhi, kuwaunga mkono Wazawa na wenyeji wanapolinda na kutekeleza haki zao. Ahadi hiyo inaonekana katika **Dira, Tunu, Kanuni za Maadili** yetu na mbinu ya msingi ya uhifadhi, ikiwa ni pamoja na Mfumo huu wa VCA. Tunatambua umuhimu mahususi wa Idhini Huru, ya Awali na ya Kumaanisha. Kuheshimu na kukuza haki za binadamu za Wazawa na wenyeji ni wajibu wa kimaadili na hali wezeshi kwa uhifadhi endelevu na ustawi wa binadamu. Kwa maelezo zaidi kuhusu mbinu yetu inayozingatia haki za binadamu, rejelea **Mwongozo wa TNC kuhusu Haki za Binadamu** (ambao umejadiliwa pia katika sehemu ya "Faida Endelevu, Athari, na Ujumuishaji").



© EVA LEPIZ

NGUZO YA 1

# Kupata Haki za Ardhi, Maji, na Rasilimali

## Maarifa, Ushahidi, na Utekelezaji

HOJA KUU

- Utambuzi rasmi wa haki unaweza kuwa muhimu katika miktadha fulani, lakini si siku zote inamaanisha kupata haki. Aina ya haki za kumiliki mali zinazomilikiwa, maarifa ya jamii kuhusu haki zao, uwezo wao wa kutumia haki hizo, na utambuzi na heshima ya haki kutoka kwa wahusika wengine huchangia katika usalama juu ya umiliki.
- Kupata haki kunaweza kusaidia kuoanisha motisha kwa matumizi na usimamizi endelevu wa ardhi, maji na rasilimali kwa kuwezesha jamii—ikiwa ni pamoja na zile zilizo na maadili dhabiti na maarifa kuhusu uwakili na uendelevu—kutoa msimamo wao na kuwajibikia maamuzi ya usimamizi.
- Kwa ujumla, usalama juu ya umiliki unahusishwa na ustawi wa binadamu na matokeo chanya juu ya mazingira, lakini yote hayawezi kufikiwa kwa wakati mmoja. Maarifa yetu kuhusu jinsi usalama juu ya umiliki unavyoingiliana na vipengele vingine vinavyoathiri matumizi endelevu na usimamizi wa rasilimali bado yanaongezeka, kuashiria umuhimu wa uchambuzi makini wa hali na ufuatiliaji.
- Haki za kupata rasilimali za pwani na za maji safi ni ngumu, zinabadilika na zinahitaji mazingatio ya ziada ikilinganishwa na haki za kupata rasilimali za ardhi. Vipengele vya kipekee vya rasilimali hizi huchangia moja kwa moja katika utata wa haki, utawala na usalama—na haki za matumizi mara nyingi hujulikana zaidi kuliko haki za udhibiti katika miktadha hii.

**MANENO YA MSINGI**

**Haki za Kumiliki Mali**—mamlaka ya kufanya hatua fulani zinazohusiana na kitu maalum. Haki za kumiliki mali ni pamoja na upataji, uondoaji (yaani, kutolewa), usimamizi, utengwaji, unyang'anyi (yaani, uhamishaji wa hatimiliki), na mchakato unaostahili kufuatwa na fidia. Haki za kumiliki mali mara nyingi huunganishwa na haki za matumizi (patikanaji, uondoaji) na haki za udhibiti (usimamizi, umiliki, utengwaji, unyang'anyi).[19]

**Haki Jumuishi**—Wazawa wana haki za pamoja ambazo ni muhimu sana kwa kuwepo kwao, ustawi wao, na maendeleo shirikishi kama watu. Kutokana na hilo, Nchi hutambua na kuheshimu haki ya Wazawa kwa hatua zao za pamoja; kwa mifumo au taasisi zao za kisheria, kijamii, kisiasa na kiuchumi; kwa tamaduni zao wenyewe; kuamini na kutekeleza imani zao za kidini; kutumia ndimi na lugha zao wenyewe; na kwa ardhi, eneo, na rasilimali zao. Nchi zitakuza, kwa ushiriki kamili na wa ufanisi wa Wazawa, kuishi pamoja kwa usawa wa haki na mifumo ya makundi na tamaduni mbalimbali za watu.[20]

**Fomu ya Umiliki**—hubainisha nani anaweza kutumia rasilimali gani, kwa muda gani, na katika hali gani.[21] Baadhi ya mifano ni pamoja na umma, mtu binafsi, jumuiya, ya pamoja ya Wazawa au ya kimila.[22]

**Usalama katika Umiliki**—mtazamo au imani ambao mwenye haki ya umiliki anayo kwamba haki za kumiliki mali zitazingatiwa na jamii—ikiwa ni pamoja na jamii, serikali na wahusika wengine.[23] Unatokana na mwingiliano kati ya fomu ya umiliki, haki za kumiliki mali na taasisi.

## Haki za Kumiliki Mali

Angalia "Nyenzo ya 2: Kuainisha Mwenye Umiliki wa Haki za Umiliki na Mdau" kwa kiolezo cha kusaidia katika kutambua wenye haki za umiliki na wadau katika eneo, pamoja na kama haki zinalindwa kwa njia rasmi au isiyo rasmi.

Mambo yanayoathiri kama mtu au jamii ina usalama katika umiliki ni tata. Haki za kumiliki mali huamuru aina ya hatua ambazo mwenye haki ya umiliki anaweza kuchukua kuhusu ardhi, maji, au rasilimali. Haki za umiliki hujumuisha haki za kutumia—upataji na uondoaji—na haki za kudhibiti—usimamizi, utengwaji, na haki ya kugawa au kuuza[19, 24]—pamoja na taratibu zinazostahili kufuatwa na fidia. Aina ya haki zinazotolewa kwa watu na jamii zinaweza kutofautiana ndani na katika maeneo tofauti. K.m., jamii inaweza kuwa na haki za matumizi kamili na udhibiti wa ardhi ya malisho na inaweza kuruhusu umiliki wa ardhi hiyo na jamii jirani wakati fulani wa mwaka au wakati wa ukame. Eneo la ziwa linaweza kumilikiwa na serikali, na jamii zinazoishi kando ya ziwa zinaweza kuwa na haki za upataji na uondoaji (k.m., uvuvi) katika mwaka, isipokuwa wakati wa msimu wa samaki kutaga mayai. Eneo la bahari linaweza kuwa na ufikiaji wazi, na haki za jadi za usimamizi zinazotambuliwa na kuzingatiwa na wenyeji na jamii jirani, na kufika eneo hilo kuruhusiwa tu kulingana na msimu au haki za uondoaji kuruhusiwa kwa spishi maalum pekee.

Ni muhimu kufahamu kuwa, *kumiliki haki tu haitoshi*. Haki hizi lazima zitambuliwe na kutekelezwa (yaani, ziheshimiwe). Watu binafsi, familia, jamii, biashara na wadau wengine wanaweza kutambua na kutekeleza haki za kumiliki mali kwa njia isiyo rasmi hata kama haki hizi hazitambuliwi rasmi na serikali (yaani, de facto/haki zisizo rasmi). Kirasmi, serikali inaweza kutoa hati na utambuzi wa kisheria wa haki kwa mwenye haki ya umiliki (yaani, de jure/haki rasmi). Kulingana na muktadha, jamii zinaweza kuhitaji utambuzi na utekelezaji usio rasmi na rasmi, ilhali katika baadhi ya matukio utambuzi usio rasmi unaweza kutosha kutoa usalama katika umiliki kwa wakati huo. Uamuzi wa ikiwa haki rasmi zinahitajika hatimaye unategemea ikiwa serikali au wahusika wengine wanaunga mkono au kupinga mfumo huo. Mwingiliano kati ya utambuzi na utekelezaji wa haki za kumiliki mali usio rasmi na rasmi ni jambo muhimu katika kubaini usalama katika umiliki.

## Usalama juu ya Umiliki

> Angalia **"Nyenzo ya 3: Tathmini ya Usalama juu ya Umiliki"** kwa utambuzi ili kusaidia kuelewa usalama juu ya umiliki katika muktadha fulani, na vile vile jinsi unavyoweza kuungwa mkono kwa ushirikiano na Wazawa na wenyeji.

Usalama katika umiliki ni mtazamo au imani ambayo mwenye haki ya umiliki anayo kwamba haki za kumiliki mali zitazingatiwa na jamii, ikiwa ni pamoja na jumuiya, serikali, na wahusika wengine.[23,25-26] Hasa ni maoni ya kibinafsi ambayo watu wanayo juu ya haki za ardhi, maji, na rasilimali, na ni mwingiliano wa haki za kumiliki mali na taasisi rasmi na zisizo rasmi zinazoamuru matumizi na upataji. Kutokana na hilo, inawezekana kuwa na usalama juu ya umiliki bila hatimiliki rasmi—kama ilivyotajwa hapo juu, watu wanaweza kujisikia salama sana katika umiliki wao wa kimila kama haitapingwa. Kwa Mfano, kuna matukio machache ambapo hatimiliki ya kisheria ya maji inashikiliwa na watu binafsi au jamii, lakini watumiaji wengi wa maji mara nyingi wanahisi kuwa wana usalama wa kufikia na kutumia maji. Mara nyingi tunazingatia usalama juu ya umiliki kwa sababu mtazamo wa usalama juu ya ardhi, maji, na rasilimali ni jambo la muhimu katika maamuzi ambayo watu hufanya kuhusu jinsi ya kutumia na kusimamia mali zao. K.m., ikiwa mwenye haki ya umiliki atatambua kuwa ana umiliki usio na uhakika, huenda kusiwe na uwezekano wa kujihusisha katika uwekezaji wa muda mrefu (k.m., kusimamia uvunaji wao wa mbao kwa njia endelevu, kuwekeza katika mbinu za kuhifadhi udongo na maji) kwa sababu faida zozote kutokana na uwekezaji huu hazitakuwepo kwa miaka mingi na hakuna hakikisho kwamba bado atakuwa na haki ya umiliki wakati huo. Kwa kulinganisha, mwenye haki ya umiliki aliye na umiliki salama anaweza kuwa na uhakikisho mkubwa zaidi kwamba wao wenyewe watafaidika na uwekezaji wowote au maamuzi ya matumizi ya rasilimali kwa sababu kuna wasiwasi mdogo wa uvamizi, migogoro, au hatua nyingine ambazo zinaweza kusababisha kupoteza matumizi au udhibiti wa ardhi, maji, au rasilimali. Kwa ufupi, kadiri jamii zilivyo salama katika umiliki wao, ndivyo inavyowezekana zaidi kushiriki katika matumizi na usimamizi endelevu.[27-30]

**Jedwali la 2:** *Vielelezo vya masuala ya kawaida ya usalama juu ya umiliki na hatua ambazo mtu anaweza kufuata ili kuzishughulikia.*[27] *Tathmini kamili ya hatari ni muhimu ili kuelewa matokeo yasiyotarajiwa ya vitendo vya usalama wa muda (kama vile kuongezeka kwa migogoro au kulipiza kisasi) kwa kuwa haki zinaweza kuleta utata. Haswa, kufaa (na uwezekano wa kufaulu au kutofaulu) kwa mkakati wowote wa kuimarisha usalama juu ya umiliki utategemea muktadha, chanzo na vichochezi vya ukosefu wa usalama, na mazingira wezeshi. Angalia* *Nyenzo ya 3 kwa maelezo zaidi*.

| Suala la Usalama juu ya Umiliki | Mfano wa Shughuli za Kuimarisha Usalama juu ya Umiliki |
|---|---|
| Jamii zina haki zisizo rasmi au za kimila, lakini haki hizi hazitambuliwi au kuzingatiwa na serikali au wahusika wengine. | Usaidizi wa uainishaji na upangaji, usaidizi wa kisheria wa kufahamu mifumo ya kisheria na urasimu, pamoja na kujenga uwezo wa kutekeleza haki, na kutafuta msaada wa serikali katika kutambua na kutekeleza haki za jamii. |
| Jamii zina haki rasmi lakini hazifahamu haki hizi | Kampeni za kuongeza uelewa, pamoja na kujenga uwezo wa kutekeleza haki |
| Jamii zina haki na zinafahamu haki hizo rasmi lakini hazijui jinsi ya kutekeleza | Usaidizi wa kisheria wa kufahamu mifumo ya kisheria na urasimu, pamoja na kujenga uwezo wa kutekeleza haki |
| Wahusika wengi wanaotekeleza haki rasmi na zisizo rasmi au madai juu ya ardhi, maji au rasilimali sawa. | Kuwezesha utatuzi wa migogoro kati ya wenye haki ya umiliki, msaada wa kisheria ili kufafanua haki, na kutafuta msaada wa serikali katika kutekeleza haki hizi za jamii |
| Vyombo vya kisheria vya jamii kutafuta haki rasmi vipo, lakini jamiihazina haki rasmi | Usaidizi wa uainishaji na upangaji, usaidizi wa kisheria wa kufahamu mifumo ya kisheria na urasimu, pamoja na kujenga uwezo wa kutekeleza haki. |
| Hakuna vyombo vya kisheria vinavyoweza kutumiwa na jamii kutafuta haki rasmi | Utetezi wa sera katika kuunga mkono mageuzi ya udhibiti |

## Fomu ya Umiliki

Fomu ya umiliki hubaini ni nani anayeweza kutumia rasilimali gani, kwa muda gani, na chini ya masharti gani.[21] Kwa mfano, kunaweza kuwa na vizuizi au vikwazo kwa haki za kumiliki mali ambavyo huathiri rasilimali mahususi ambazo haki hizo zinatumika (k.m., haki za kudhibiti spishi moja maalum), na kwa muda gani haki hizo zitatumika (k.m., haki ambazo hudumishwa hadi zitakapohamishwa dhidi ya zile zilizowekewa muda maalum). Kigezo hiki kinahitaji kuzingatiwa katika kubainisha jinsi haki salama zilivyo. k.m., ikiwa jamii ina haki ya kutumia na kudhibiti msitu kwa miaka 20, lakini haki za kuchimbua madini na vitu vilivyo chini ya ardhi zimepewa kampuni katika eneo lenye madini mengi, jamii zinaweza kukosa kuhisi na kuwa salama katika haki zao.

Katika mahali ambapo Wazawa na wenyeji hukaa, kunaweza kuwa na mchanganyiko wa fomu ya umiliki wa umma, wa kibinafsi, wa jumuiya, wa Wenyeji kwa pamoja, na/au ya kimila. Katika hali ambapo Wazawa wamepokonywa umiliki wao wa jumuiya au wa pamoja, mara nyingi tunafanya kazi kwa ushirikiano kurejesha umiliki huu (k.m, kurejesha ardhi ya kibinafsi, maji, au rasilimali kwa umiliki wa jumuiya au wa pamoja; utetezi wa sera kwa ajili ya uundaji wa maeneo asili yanayohifadhiwa) au kurejesha na kuunga mkono mamlaka ya Wazawa na wenyeji. Katika fomu za umiliki wa umma, jumuiya, na wa pamoja, rasilimali mara nyingi ni rasilimali ya pamoja—kwa kuwa wengi wana haki za ukutumia (yaani, upataji na uondoaji) bila uwezo rahisi wa kuwatenga watu (k.m., uvuvi wa pwani, maeneo ya misitu, nyika na vyanzo vya maji.) Katika hali hizi, inaweza kuwa muhimu kufafanua ni nani au nini huamua haki za kudhibiti (hasa haki za usimamizi na utengwaji) ikiwa muktadha unaruhusu, na kuimarisha mifumo ya utawala wa pamoja (inayoangaziwa katika sehemu inayofuata), haswa kwa kukosekana kwa maadili thabiti ya uwakili au mbele ya makundi mbalimbali ya watendaji au vichochezi vikali vya uchumi.

## Ushahidi Unaoibuka

Mantiki ya sababu na vile kuimarisha usalama juu ya umiliki unaweza kusababisha faida jumla ni wazi: kupata umiliki kunaweza kupunguza hali ya kutokuwa na uhakika, kutoa ufafanuzi wa mtu aliye na usemi katika maamuzi ya matumizi na usimamizi, kutambua atakayefaidika kutokana na ardhi, maji na rasilimali, na kuwa sehemu muhimu katika kufungua mtaji (k.m., utoaji wa mikopo, kuwawezesha wenye haki ya umiliki kushiriki katika maamuzi).[31-34] Hata hivyo, kwa ujumla kuna ushahidi mkubwa zaidi kwamba kuimarisha usalama juu ya umiliki kunahusishwa vyema na matokeo ya ustawi wa binadamu ikilinganishwa na matokeo ya kimazingira, na mapitio ya utaratibu ya hivi majuzi yanaonyesha kwamba matokeo juu ya matokeo ya mazingira katika viumbe hai, idadi ya viumbe, nchi na mambo mengine hayalingani.[27] K.m., kuna matukio ya mipango ya kuwa na hati miliki kuanzia ngazi ya juu kwenda chini ambayo yamesababisha matokeo yasiyofaa kama vile migogoro mikubwa na ukosefu wa usalama juu ya umiliki kwa sababu ilipuuza au haikuwa na uwiano na taasisi za kimila na mifumo ya usimamizi wa maliasili.[35]

Kwa sababu bado kuna ushahidi ibuka juu ya uwezekano wa ikiwa kuimarisha usalama juu ya umiliki kutasababisha matokeo chanya ya mazingira na ya ustawi wa binadamu, ufuatiliaji wa makini unahitajika ili kuepuka au kushughulikia matokeo yasiyotarajiwa. K.m., usalama juu ya umiliki ulioimarishwa unaweza kuongeza vivutio vya kufanya uwekezaji wa muda mrefu wa ardhi, lakini hii inaweza kusababisha uwekezaji mkubwa katika kilimo au miundombinu kuliko katika usimamizi endelevu wa ardhi au ulinzi.[27] Kwa upande mwingine, maeneo ambayo jamii zina usalama mkubwa wa umiliki zitakuwa na ukataji miti uliopungua kwa kutoa motisha kwa faida zinazotokana na misitu kupitia njia nyinginezo, kama vile malipo kwa ajili ya huduma za mfumo wa kiikolojia. [36] Kwa mifumo ya majini, usalama juu ya umiliki wa—ambao unafafanua mtu aliye na haki kwa baadhi ya maji au

viumbe vya majini na wakatii—inaweza kuibua hali ya kuwepo kwa mazungumzo ya mikataba ya uchimbaji na matumizi, pamoja na jinsi wenye haki za umiliki watakavyosimamia na kutekeleza makubaliano haya.[37] Katika maeneo ya pwani, kuanzisha mifumo ya usimamizi inayozingatia haki za uvuvi kunaweza kusababisha athari chanya kwenye hifadhi ya samaki na matokeo tofauti ya kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, hii inaweza isitoshe kushughulikia athari pana za uvuvi kwa mazingira, kwa mfano juu ya spishi zisizolengwa au zinazolindwa pamoja na mfumo wa kiikolojia unaozunguka.[38-39]

## Mazingatio Maalum ya Haki katika Miktadha ya Maji Safi na ya Pwani

Kwa sababu ya hali yao ya ugiligili, rasilimali za maji safi na za pwani zina uwezekano mdogo wa "kumilikiwa" kama vile ardhi au mali nyingine zinavyomilikiwa. Badala yake, ni muhimu kuangalia ni nani anashikilia (na mara nyingi zinazopishana) "haki tofauti za kupata miliki," ikiwa ni pamoja na haki za matumizi na za kudhibiti, na jinsi haki za maji zinavyofungamanishwa na haki za ardhi. K.m., kutokana na kuwepo kwa rasilimali nyingi za maji safi, kiwango cha haki na usimamizi wa rasilimali hailingani na kiwango cha ikolojia ya mifumo (k.m., mito mara nyingi huvuka mipaka mingi ya nchi). Zaidi ya hayo, hata kama jamii ina haki ya kutumia au kusimamia rasilimali ya maji safi, kama rasilimali hiyo itaisha katika maeneo ya juu ya mto, hawawezi kamwe kutekeleza haki hizi. Kwa hivyo, ni muhimu kutathmini kwa uangalifu jinsi sifa za maji safi na rasilimali za pwani zinaweza kuleta changamoto au fursa za usalama juu ya umiliki, na hatari mbalimbali kwa usalama juu ya umiliki ambazo zinaweza kutokana moja kwa moja na sifa za maliasili fulani. Haki pekee hazitoi hakikisho la uwezo wa kutumia au kufaidika kutokana na rasilimali za maji safi na za pwani. Vyanzo vingi vya maji vimetengewa watu kupita kiasi, kwa hivyo haki zinazidi rasilimali zilizopo (k.m., haki za uondoaji wa maji safi, haki za uvuvi wa pwani). Katika muktadha wa maji safi, hali hii inazidishwa wakati wa miaka ya ukame. Vile vile, vyanzo vingi vya maji vimechafuliwa, na kufanya rasilimali zilizopo kutotumika kwa madhumuni fulani. Kutokana na hili, ni muhimu kuzingatia mienendo ya nguvu kati ya watumiaji wa maji safi na rasilimali za pwani kwa sababu kukosekana kwa usawa kunaweza kuzuia vikundi fulani kutumia haki zao.









# Utafiti Maalum

## Kulinda Haki za Maeneo na Rasilimali nchini Tanzania

Nyanda za malisho zilizoko kaskazini mwa Tanzania zimeenea kwenye ekari milioni 8 (hekta 3.2) na zina baadhi ya makao muhimu za wanyamapori, kama vile Serengeti na Kasoko la Ngorongoro, vilevile ni makao ya wafugaji Wamaasai, Wahadzabe na Akie, baadhi ya makabila duniani yanayoendeleza uwindaji na uchumaji. Idadi ya watu unakaribia kuongezeka mara tatu kwenye eneo hili katika miaka 40 iliyopita, jambo hili linaongeza ushindani kati ya matumizi ya ardhi (hasa kilimo na malisho), ikitishia wafugaji na mbinu za maisha za uwindaji na ukusanyaji, vilevile wanyamapori wanaotegemea ardhi hizi kwa malisho na uhamiaji. Vijiji vya wenyeji vina haki kugawana ardhi yao yote ya kijiji, na punde ardhi inapogawiwa rasmi kwa mtu binafsi, ardhi hiyo inaweza kugawiwa zaidi kwa watoto wa kiume. Sheria hii inapendelea uenyeji na umiliki wa mtu binafsi. Isitoshe, mamlaka ya serikali kuu nchini Tanzania na inaweza kuchukua ardhi na kuifanyiza mashamba makubwa ya kibiashara iwapo vijiji havina cheti rasmi (umiliki) kupitia Hati ya Kumiliki Ardhi Kimila (CCRO)

TNC barani Afrika inafanya kazi na jamii na washirika kupata umiliki wa kisheria na usimamizi wa haki wa jamii za wafugaji na za uwindaji na uchumaji kupitia **Umiliki wa pamoja wa Ardhi Kimila**. Chombo hiki cha kisheria—kilichoanzishwa naTimu ya Rasilimali Jamii ya Ujama na kuiimarisha umiliki wa ardhi kimila kwa mtu binafsi—unaruhusu jamii kumiliki na kusimamia ardhi za jadi na kunufaika kupitia makampuni ya biashara ya mali asili kama vile Utalii wa kiikolojia na Pongezi kwa ajili ya kupunguza hewa ya ukaa. Umiliki wa pampja wa Ardhi Kimila unatoa ulinzi wa ziada kwa raslimali za pamoja wenye manufaa ya usimamizi wa muda mrefu na upatiakanaji wa malisho bora na salama baada ya muda.

Kwa kueneza mfumo huu kwenye nyanda za juu za malisho za Tanzania, tunashuhudia usawa zaidi katika upataji na umiliki, na njia halali zaidi na haki za kijamii kwa muda mrefu kama msingi wa uzalishaji wa ufugaji mifugo na mifumo ya usimamizi wa ardhi. Pale wanapovuka mipaka kutafuta malisho mapito huachwa wazi, mifugo na wafanya pori wanakuwa na afya zaidi, jambo ambalo linapunguza vita kati ya wanavijiji na inaweza kuongeza mapato kupitia fursa endelevu za maisha. Utaratibu wa umiliki wenyewe unahusiana na usimamizi endelevu wa ardhi kupitia mahitaji ya Mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji na inatoa msingi wa kujadiliana na serikali na waendeshaji utalii Ingawa kesi za uzamizi kilimo zipo, zinapojaribiwa, mahakama imepitisha kwa manufaa ya CCRO na urahisi. Zaidi ya miaka

**PICHA YA AIKONI**
Maeneo ya Mfumo wa VCA

**NCHI KAVU** **MAJI SAFI** **PWANI**

tisa iliyopita, ekari milioni 5 (~hekta milioni 2) zimewekwa chini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji (hatua ya kwanza katika kupata umiliki wa CCRO). Katika mandhari nzima, ekari milioni 4.2 (~hekta milioni 1.7) za nyanda za malisho zimelindwa kupitiaCCRO 80 na Maeneo mawili ya Usimamizi ya Wanyamapori (maeneo ya ardhi ya jamii yamewekwa kando na wanakijiji kama makazi ya wanyamapori), pamoja na CCRO za ziada zinazofikia ekari 370,650 (~hekta 150,000) kufikia Juni 2022. Mafanikio ya CCRO yanaonyesha njia ya kubadili matumizi ya ardhi unaoweza kuleta kupotea kwa maeneo ya malisho.

Hata hivyo, bado pana changamoto zinazoendelea zinazopaswa kutatuliwa. Hata baada ya mipango ya matumizi ya ardhi kutengwa na CCRO kuundwa, kulikuwa na ufugaji kupita kiasi kwenye CCRO Programu ya. Usimamizi wa kijumla wa malisho wa TNC unakusudia kueneza njia bora zaidi za malisho kwenye CCRO, kama vile malisho ya mzunguko, ufugaji kwa njia ya uzio, na ufugaji wa mzunguko unaoweza kupunguza kuchunga kupita kiasi kwenye ardhi ya CCRO. Mpango utasaidia pia kuleta makubaliano baina ya vijiji yanayolenga kuunganisha CCRO na maeneo mengine ya malisho. Wakati CCRO zinaendelea kuonekana halali na wadau wa eneo husika, pana matatizo endelevu ya uongozi na hata haja ya kuhakikisha CCRO zinaheshimiwa pia.



## Kushugulikia Uhaba wa Maji kupitia Haki za Wazawa kwenye Bonde la Mto Colorado

Bonde la Mto Colorado ni moja ya madhari nzuri sana Marekani, ndo sehemu yenye kutumika Mchezo mkubwa wa kuogelea pamoja na Mawakili weng wa kijadi na kikabila. Una aina mbalimbali za maji safi na mifumo ya kiikolojia ya ardhi yenye kutunza bayoanuai kubwa, na unabeba maslahi mapana ya tamaduni nyingi, jamii na uchumi. Kwa maelfu ya miaka, maji kutoka Mto Colorado na vijito vyake yamekuwa chanzo cha maisha cha Wazawa wa eneo hili, na ni muhimu kwa utamaduni na ustawi wa kiuchumi. Ukoloni wa walowezi juu ya ardhi na maji kwa kiasi kikubwa uliathiri uwezo wa Wazawa kuendelea kukaa hapo, kutumia, na kutunza mito na ardhi kwenye eneo hili. Mauaji ya kimbari, matumizi ya nguvu katika kutolewa kwenye mashamba ya mababu, uvunjwaji wa mikataba, na matumizi ya sheria za shirikisho na sera zilizoundwa kudhoofisha udhibiti wa kikabila wa kulinda raslimali na kuiga Wazawa kuliwanyima upatikanaji ardhi, maji, chakula na maliasili mengine ya bonde. Kuongezea, ujenzi pana wa miundombinu ya maji ya mabwawa, mifereji, na hifadhi ilishia kuharibu zaidi mazingira asili na kupuuza kwa wingi mahitaji ya maji ya watu asili, ambao walilazimishwa katika kilimo kisicho asilia na ufugaji na maisha ya kutoridhishwa kwa ukame.

Ukitumiwa na na watu zaidi ya milioni 40 wakiitegemea kwa ajili ya kilimo na mahitaji ya nyumbani, Mto Colorado unasimamiwa vema, nakanuni na sheria nzito zinalazimisha uhifadhi wa maji na matumizi baina ya watumiaji wengi wa Bonde. Sheria ya awali inaruhusu Wazawa ndani ya Marekani kutumia, haki zenye kugusa kipaumbele cha Bonde. Hata hivyo, majukwaa mengi yenye kuhusa ufanyaji wa maamuzi yanayohusiana na maji na mchakato bado hayajatambua vya kutosha jukumu la Usimamizi wa maji na mali asili. Kikabila Kwa sasa, 22 kati ya Wazawa 30 ndani ay Marekani kwenye Bonde wamehesabu haki za maji angalau kwenye jimbo moja ambamo uhifadhi wao unafanyuikia, na udhibiti wa karibu bilioni 3.5 za mita za ujazo, ambazo ni takriban asilimia 20 ya maji kwenye Bonde. Kiasi hicho kinatarajiwa kuongezeka pale ambapo Wazawa ndani ya Marekani wenye madai yaliyosalia kwenye baadhi ya majimbo yaliyo kwenye

---

a. Ugawaji na matumizi ya maji na mashirika yasiyo ya shirikisho kwenye majimbo mengi Magharibi mwa Marekani yanaongozwa na Mafundisho ya Kabla ya Ugawaji, pale ambapo shirika la kwanza kugawa wingi wa maji kutoka kwa chanzo kwa matumizi ya manufaa inapata mamlaka ya matumizi yake dhidi ya watumiaji wa baadaye. Haki zilizohifadhiwa za shisikisho, ikiwamo zile zilizohifadhiwa kwa niaba ya Wazawa ndani ya Marekani, zinahusishwa na ufihadhi wa ardhi wa shirikisho wa Marekani na huwa zina tarehe za kipaumbele zilizofungamana na tarehe za uhifadhi wa ardhi wa shirikisho. Kwa sababu ya hili, Haki za Maji za Kikabila magharibi mwa Marekani aghalabu huwasilishwa mapema sana na tarehe ya kipaumbele cha juu.




Bonde wanahesabu haki zao za maji. Sehemu muhimu za hizi haki za maji bado hazijaimarishwa (kumaanisha bado hazifuatwi au kutumiwa) lakini zinaweza kutumika badala ya matumizi ya maji ya sasa zinapoimarishwa.f Licha ya kiwango cha maji ya Kikabila, wahusika wengi kwenye bonde (kama vile serikali ya shirikisho na jimbo, watumizi wakuu wa maji kama vile biashara za manispaa na kilimo) wamewatenga kwa maksudi na utaratibu ya Wazawa ndani ya Marekanikutokana na juhudi za kuhifadhi na kuendeleza haki zao za kupata maji, ilizuia ushiriki wa hiari wa kikabila kwenye mazungumzo ya sera. Hivi karibuni kama 2019, kwa sababu ya kutotaka kwa jimbo na shirikisho kuangalia kwa makini juhudi za Kabila la Maji kuchanganua uhaba wa maji na suluhisho, wazawa ndani ya Marekani wamekuwa wakitengwa sana katika mipango inayonuia kupunguza athari ya uhaba. Kutengwa huku kumesababisha masuluhisho ambayo yameshindwa kutambua na kuheshimu mkataba na haki nyingine za wazawa, na kukosa fursa ya kufanya kazi na Wazawa ndani ya Marekani kuhamasisha Maji ya Kikabila kushugulikia changamoto za jamii-uchumi na mazingira ya Bonde. Hii michakato za sera pia inakosa fursa muhimu kuleta pamoja mitazamo asilia kwa usimamizi wa raslimali—ikiwamo miunganisho ya kitamaduni asilia na ya kiroho yanayohusiana na ardhi na maji kwenye Bonde—ili kuweka sawa mstakabali wa mto huu mtakatifu wenye kutumika na wote.

Programu ya TNC juu ya Mto Colorado inafanya kazi kote kwenye majimbo saba Marekani ambamo mto unapita (Wyoming, Colorado, Utah, New Mexico, Arizona, Nevada,na California), Mexico pia kwenye maeneo ya bonde. Mikakati ya kuzingatiwa ni mitatu: kufanya kazi kuletea usawa wa maji kati ya watumiaji wengi (ikiwemo asili), kuboresha miundombinu ya maji na shughuli nyingine.kuboresha mtiririko wa maji, na kuendeleza mpango wa maji wa Kikabila. Kupitia Mpango wa maji ya Kikabila, tunafanya kazi na Wazawa ndani ya Marekani kuendeleza maslahi yao na nafasi zao kushugulikia changamoto kubwa za kijamii, kiuchumi na kimazingira, kwa kuinua sauti za Kikabila kwenye majadiliano ya sera muhimu ili kuunga mkono usimamizi wao wa Bonde, na pia kutengeneza mbinu bunifu za kuhifadhi maji safi zinasosaidia mbinu zaidi za usawa na ufumbuzi wa kudumu kwa watu na mazingira. Kwa mfano, kwenye mazungumzo mapya ya **Mwongozo wa Mpito wa Mto Colorado kwa ajili ya Uhaba wa Bonde la Chini na Uendeshaji Unaoratibiwa kwa ajili ya Maziwa Powell na Mead**, TNC iliombwa kufanya kazi na Wazawa ndani ya Marekani na mashirika mengi ya Kikabila ili kuelewa na kuendeleza malengo yao, kama vile kuhakikisha miongozo inaonyesha uelewa mpana wa Haki za Kikabila za maji.

Kuhusisha Wazawa ndani ya Marekani kwenye Bonde la Mto Colorado kunabadilisha mbinu ya TNC kuhusu kazi ya kushughulikia uhaba wa maji. Maamuzi yetu ya awali yanaonyesha fursa za uhakika za kazi za mradi na sera ili kushugulikia uhaba wa maji na mahitaji ya mazingira kwenye Bonde. Inatubidi pia tuanze kuzingatia baadhi ya usawa muhimu na athari za haki za binadamu za Wazawa kwenye kazi yetu, ikiwa ni pamoja na haja ya mchakato wa upatanisho inayoshughulikia rasilimali iliyonyimwa kitambo na kukiri jukumu la sekta ya uhifadhi katika kuacha alama. Tumedhamiria kuleta ufumbuzi ambao hauleti hasara zaidi kwa jamii zenye maisha magumu ila, badala yake, unaojenga ushirikiano kukuza nguvu na mamlaka ya jamii hizi kuunda kwa pamoja ufumbuzi na miradi yenye manufaa kwa pande zote.

---

f. Hii ni kwa sababu ya tarehe ya kipaumbele ya juu ya madai ya Shirikisho la kikabila la haki zilizohifadhiwa na kwa sababu ya machapisho mengi juu ya bonde la Mto Colorado yanayosema eti Haki za kikabila hazihusiani na mkusanyiko..



© MWANGI KIRUBI

## Haki za Kijamii Zinazohusu Uvuvi Pwani ya Kenya



Ikipatikana mwishoni mwa kaskazini ya pwani ya Kenya, Madhari ya Bahari kati ya Lamu na Tana ina utajiri na raslimali mbalimbali za pwani, ikiwemo karibu asilimia 66 ya mikoko ya Kenya, baadhi uzito mkubwa wa samaki za mapezi, krasteshia, na mkusanyiko wa kipekee wa ghuba za Arabu zenye matumbwe na aina za samaki. Matumbwe nadra pamoja na samaki waliohatarini, kasa wa baharini, papa wa pwani, na idadi ndogo sana ya dugo hupatikana hapa. Riziki za wanajamii kwenye eneo zinategemea sana mali asili, na kwa kuwepo kwa njia chache mbadala za kuajiriwa, shinikizo na matumizi kupita kiasi yanaongozeka. Pamoja na vita vinavyoendelea na umbali unaokwaza maendeleo na kufikishwa kwa masoko, maisha na raslimali kwenye eneo yapo hatarini.[40]

Kuongezea umiliki na usimamizi wa wenyeji wa rasilimali hizi, TNC, Mfuko wa Nyanda za Juu za Malisho za Kaskazini (NRT) na washirika wengine wanasaidia jamii kupata haki za usimamizi wa pamoja kwa kutumia mamlaka tofauti ya kisheria ya usimamizi wa mali asili na jamii kuleta pamoja mbinu ya kijumla ya usimamizi wa mifumo ya kiikolojia ya pwani. Mbinu ya ‘‘uhifadhi wa jamii’’, iliyo chini ya Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori (2013), imetumika kwa upana na matumizi ya jamii kwa usimamizi ya maeneo ya nchi kavu. Kwa msaada na mwongozo wa kitaalamu wa NRT na TNC, mbinu hii imepewa nafasi kutumika kwenye mandhari ya Lamu-Tana kwa jamii za pwani na maeneo ya baharini, ikiunganisha vijiji vingi, uvuvi, na makazi chini ya Mpango kabambe wa Maendeleo ya Uhifadhi. Mpango huu unajumuisha miongozo muhimu ya ubunifu muhimu kwa ajili ya uhifadhi murua maeneo ya pwani.

Hifadhi nne za jamii za pwani—Kiunga, Awer, Pate na Tana Delta ya chini—zimeanzishwa, na katika hifadhi hizi taasisi nyingi za maamuzi ya kijamii lazima zipewe meno ya kisheria ili kuwezesha kisheria kwenye uhifadhi na jamii kusimamia zoezi kamili la raslimali za pwani, ikizingatiwa kuna sheria mbalimbali na mamlaka. Jamii inaendeleza vitengo vya pamoja vya usimamizi, viitwavyo Vitengo vya Usimamizi vya Fukwe (BMU), zinazojishugulisha na uvuvi mdogo wa kujikimu na wa wazi. BMU zinalindwa na mfumo wa sheria kwenye Kanuni za Uvuvi za Kenya (2007), na zinakusudia kuleta vikundi vya watumiaji wa raslimali na vyombo vya serikali kugawana majukumu ya usimamizi na uhifadhi katika uvuvi. Kati ya hifadhi hizi nne za jamii, BMU 21 za uvuvi zimeimarishwa na mafunzo kufanyika juu ya uongozi, usimamizi

wa pamoja wa maeneo ya uvuvi, na usimamizi wa hela. Kila BMU iliwasilisha sheria zake ndogo kwa serikali za kaunti kwa ukaguzi na kupokea hati mpya ya usajili wa BMU, kuwezesha kwa ufanisi udhibiti wa jamii juu ya rasilimali zao za uvuvi. Kuanzishwa kwa hifadhi BMU husianishwa kumewezesha Hifadhi ya Bahari ya Jumuiya ya Pate kuzuia kwa muda uvuvi wa pweza (aina ya eneo bahari linalosimamiwa na wenyeji) ambavyo vimeleta kuongezeka kwa wanawake katika shughuli za uhifadhi, kuongezeka uvuvi na ukubwa wa pweza, bei nzuri la soko, kuongezeka kwa idadi ya samaki wengine, na kuboreshwa kwa hali ya makazi.

Kujifunza kupitia ziara za kubadilishana kati ya hifadhi za Kiunga na Delta ya Chini ya Tana ulihamasisha Uhifadhi wa Jumuiya ya Kiunga pia kuzuia kwa muda uvuvi katika maeneo yao ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Bahari ya Kiunga (KMNR). Ulinzi na uhifadhi wa bahari unasimamiwa na Shirika la Wanyamapori la Kenya (KWS) kwa mfumo wa hifadhi za bahari, ambazo ni maeneo ya sheria kali za kutoruhusu uvuvi zenye kuhifadhi uvuvi muhimu na maeneo tengefu ya bahari, pale ambapo uvuvi wa kujikimu kwa kutumia mbinu za jadi unakubalika na hautiliwi maanani. Kwa sababu ya cheo cha hifadhi ya bahari ya Kiunga, mwelekeo mgumu zaidi rasmi, na ruhusa ya kiwango cha taifa ilihitajika ili kuwezesha mamlaka ya usimamizi wa kijamii chini ya KWS. Hii ilihusisha kumalizisha, kijiji kwa kila kijiji, kufahamisha jamii na mikutano ya kujenga uwezo kuhusu kuanzisha mafungo ya muda ya pweza, kubadilisha jina la hifadhi kuwa Chama cha Wanyamapori cha Jumuiya ya Kiunga (KICOWA) Muungano wa wanyamapori wa jamii ya Kiunga (KICOWA) kufanya kazi kwenye eneo lilitangazwa kwenye gazeti la serikali, na kutuma barua kwa KWS kuhusu uamuzi wa jamii kufunga kwa muda uvuvi wa pweza ndani ya KMNR. Kufikia kukamilika kwa mchakato huu, KICOWA ilifanikiwa kuzuia uvuvi wa pweza maeneo mawili mwezi Machi 2021, ambayo yalikuwa ya kwanza kukamilishwa ndani ya eneo tengefu la taifa la bahari na maendeleo makubwa kuhusisha mtazamo wa kijamii katika usimamizi wa maeneo ya uhifadhi wa bahari nchini Kenya.

Kufikia ufanisi wa usimamizi wa mifumo ya kiikolojia kaskazini mwa Kenya kunahitaji mpangilio mkali wa sheria na taasisi zinazohusiana na kila raslimali na jina la umiliki. Kazi ya TNC na washirika wa karibu wamejikita katika kuimarisha utawala kwa kusaidia jamii kujenga na kutafuta wafanyakazi wa taasisi muhimu ili kushirikiana katika kusimamia maliasili, na kuwezesha ushirikiano kujengwa baina ya taasisi tofauti za uhifadhi zinazoongozwa na jamii.

# Nyenzo na Rasilimali

## NYENZO YA 2: KIOLEZO -KUAINISHA MWENYE HAKI ZA UMILIKI NA MDAU

Kwa kuwa haki zinazodumishwa (au zisizodumishwi) kuhusu ardhi, maji, na rasilimali ni muhimu ili kuelewa msingi wa muktadha wa mahali, ni ya muhimu kufanya zoezi la kuongeza uelewa juu ya aina ya umiliki wa rasilimali, wenye haki ama wenye hisa za umiliki wa rasilimali, aina ya utambuzi wanayojua, na haki zinazoweza kuingiliana au madai. Kiolezo hiki kinaweza kutumika kwa uchambuzi wa hali ili kutunza ujumbe huu kwa kutafuta ushauri wa wenyeji, kikanda, vyombo vya sera za kitaifa, idara ya mali asili (au taasisi za aina hiyo za serikali), na jamii au taasisi itayoiwakilisha. Zoezi hili linapaswa kufuatiwa na "Nyenzo ya 3: Tathmini ya Usalama juu ya Umiliki" kuamua usalama wa haki, na shughuli gani zinaweza kuwa sahihi kushughulikiwa vyanzo vya kutokuwepo usalama.

## NYENZO YA 3: TATHMINI YA USALAMA JUU YA UMILIKI

Usalama juu ya umiliki ni mada ngumu yenye kuzingatia mengi yanayohusiana na kuathiriana. Katika "Nyenzo ya 2: Kuainisha Wamiliki na Wadau," tulibaini mmiliki kutoka kwa maliasili, suite ya wenye haki ama wenye hisa kwa raslimali, aina ya kutambuliwa wanayoshikilia, na haki zinazoweza kuingiliana au madai. Kwa kutumia habari hii, tunatambua vyanzo vinavyowezekana vya kutokuwepo na usalama juu ya umiliki vinavyowapata wazawa na jamii ya wenyeji, na vitendo ambavyo mashirika ya kuhifadhi yanaweza kuchukua kwa ushirikiano na Wazawa na wenyeji kuunga mkono usalama juu ya umiliki uliomarishwa. Habari hii inapaswa kujadiliwa na jamii, ama taasisi za uwakilishi, wakati wa uchambuzi wa hali ya mahojiano makuu tukitumia na kuzingatia majadiliano ya kundi.

**Tafadhali kumbuka, **tathmini nzima juu ya hatari inahitajika** kuelewa matokeo yanayowezekana ambayo hayakukusudiwa (kama vile, kuongezeka kwa mizozo au kulipiza kisasi) ya hatua za kupunguza, kwa kuwa sheria inaweza kuwa tata. Hatimaye, kufaa (na uwezekano wa kufaulu au kutofaulu) kwa mkakati wowote kuimarisha umiliki usalama utategemea muktadha, chanzo na sababu za kukosekana kwa usalama, na masharti wezeshi.*

Nguzo ya 2

# Uongozi Thabiti, Utawala, na Uwezo wa Kuongoza


© KEVIN ARNOLD

## Maarifa, Ushahidi, na Mazoea

HOJA KUU

- Uwezo thabiti ni nguzo kwa jumuiya kutenda kwa pamoja, kutawala ipasavyo, na kusimamia kikamilifu rasilimali , pamoja na kutetea haki za umiliki maeneo na rasilimali zao, kuisimamia mamlaka ya utoaji maamuzi, kujadiliana na wadau wengine na/au wenye haki ya umiliki, kupata na kusimamia fedha na msaada kutoka nje, kutafuta fursa za kiuchumi zilizojidhatiti kuendana na utamaduni.

- Mikakati ya ujengaji uwezo hutumia aina mbalimbali za shughuli zinazolenga aina mbalimbali za rasilimali—ikiwa ni pamoja na rasilimali watu, rasilimali jamii, taasisi, mifumo, maliasili na uchumi ambayo inahitaji kupangwa kulingana na viwango vya sasa vya ujuzi na mahitaji ya jamii.

- Ni muhimu kufanya kazi na viongozi waliochaguliwa na jumuiya kwa kutumia mifumo ya maarifa iliyopo na taasisi pale inapowezekana, huku tukiweka masharti maalum kwa ajili ya ushirikishwaji wa jamii zenye maisha duni au uwakilishi mdogo (k.m.,wanawake, vijana, wasiojiweza kiuchumi au wanaokandamizwa, makabila madogo, n.k.) katika kutafsiri sheria na kanuni zinazowaongoza.

- Jumuiya zinaweza kuwa nzuri sana katika kusimamia rasilimali za pamoja lakini mara nyingi jumuiya za namna hiyo na rasilimali husika huwa na sifa kadhaa zinazofanana (kwa maelezo zaidi kuhusu sifa hizi, endelea kusoma)

**MANENO YA MSINGI**

**Uwezo—**dhana yenye kubeba sura mbalimbali kwa ujumla hufafanuliwa kama "kuwa na uwezo wa kutenda," na ni lazima aina mbalimbali za mtaji zitumiwe kufanya hivyo zikiwemo za kibinadamu, kijamii, kitaasisi, kiasili na kiuchumi[12-13]

**Hatua ya Pamoja—**Hatua inayochukuliwa na kikundi ili kufanikisha lengo la pamoja.[41-44]

**Rasilimali ya pamoja**—Bidhaa yoyote yenye kushikika ambayo kupitia matumizi hupungua wingi au ubora (yaani inayoweza kupunguzwa) na inagharimu au vigumu kuwatenga wengine wasitumie.[45]

**Utawala**—katika muktadha wa usimamizi wa maliasili, unarejelea mila, taasisi, na taratibu ambazo ndizo huamua ni kwa jinsi gani mamlaka na wajibu unatekelezwa, jinsi ya kufanya maamuzi maamuzi, na jinsi watu wanavyoshiriki na kunufaika na usimamizi wa maliasili.

**Maarifa ya Wazawa**—Mkusanyiko wa maarifa, mazoea, na imani, zinazobadilika na kusimamiwa na taratibu himilivu na kurithishwa kwa vizazi na vizazi kwa njia ya urithi wa kitamaduni, kuhusu uhusiano wa viumbe hai (wakiwemo na watu) wao kwa wao na mazingira yao.[46] Dhana hii wakati mwingine inajulikana kama "maarifa ya wenyeji" kwa wale ambao hawajitambulishi kama wazawa.

**Taasisi**—ni kanuni na /au au mashirika yanayounda mwingiliano wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Zinajumuisha kanuni zisizo rasmi (k.m., vikwazo, miiko, desturi, tamaduni, na kanuni za maaadili), na kanuni rasmi (k.m., katiba, sheria, haki za kumiliki mali).[47]

**Ushirikiano wa jamii**—aina ya mtaji wa kijamii unaoathiri hatua za pamoja; ni sifa ya kikundi inayoelezea kiwango cha muunganiko na mshikamano wa wanajamii wake, ambao ukiwa na nguvu unaweza kukuza uzalendo na kushirikishana uzoefu ambao utajenga msingi imara wa ushirikiano.

## Aina za Uwezo, Kujengea uwezo, na Matokeo juu ya Mazingira

Usimamizi wa maliasili unaoongozwa na jamii ni mchakato changamano wa kijamii unaohitaji hatua ya pamoja na usimamizi makini wa rasilimali za pamoja, na unasaidiwa na uwekezaji katika aina mabalimbali za mtaji (k.m., mali—za kifedha na zisizo za kifedha; angalia Jedwali la 3). Uhitaji wa wanajamii imara na wenye uwezo, viongozi, na taasisi hufanya kujengea uwezo kuwa mojawapo ya mikakati ya msingi ya mfumo wa VCA na inayotumika mahali pengi. Kuna ushahidi ulio wazi kuwa uwekezaji katika mikakati ya kujengea uwezo ni muhimu kwa matokeo ya kimazingira.[48-49] Uwezo ni dhana yenye kubeba sura nyingi kwa ujumla hufafanuliwa kama "kuwa na uwezo wa kutenda," na ni lazima aina mbalimbali za mtaji zitumiwe kufanya hivyo zikiwemo za kibinadamu, kijamii, kitaasisi, kiasili na kiuchum.[12-13] Shughuli za kujengea uwezo kwa kawaida hulenga kuimarisha moja au zaidi ya aina hii za mtaji, hasa ambapo mahitaji yamebainishwa na uchambuzi wa hali au vipaombele vilivyotajwa na wazawa na washirika wa wenyeji (Jedwali la 3). Ingawa usimamizi wa maliasili kwa njia ya jamii hutegemea sana muktadha,[50] uwezo ni msingi na uwekezaji katika kuimarisha aina moja au zaidi za mtiaji hii kuhitajika karibu wakati wote.

**Jedwali la 3:** *Aina za mitaji, malengo ya kujengea uwezo, na baadhi ya mifano ya shughuli. Kumbuka kuwa, muhimu kuzingatia kila aina ya mtaji katika tathmini yoyote ya kuangalia uwezo wa wanajamii (kwa mifano jinsi ya kutathmini, angalia Hartanto et al., 2014).*[51]

| Aina ya Mitaji | Malengo ya kujengea uwezo | Mifano ya shughuli |
|---|---|---|
| Ya kibinadamu | • Ufahamu<br>• Maarifa<br>• Ujuzi<br>• Uzoefu | • Kuunga mkono tathmini, kufufua, na kupitisha uwakili unaoendana na wazawa au maarifa ya mazoea ya wenyeji (e.g., uchomaji wa kimila, malisho, uvuvi)<br>• Kutoa elimu na uhamasishaji/ kuendesha kampeni za kuongeza uelewa<br>• Kuanzisha sayansi jamii, ufuatiliaji kwa ajili ya usimamizi himilivu, na tathmini ya matokeo ya mradi (k.m., kuripoti viumbe vamizi, uangalizi wa viumbe)<br>• Kutoa mafunzo na usaidizi wa kiufundi (k.m., usimamizi bora wa maliasili, mazoea ya kuhifadhi udongo, matumizi bora ya vifaa) Convening knowledge exchange<br>• Kuwezesha fursa za kujifunza kati ya rika na rika |
| Ya kijamii | • Maarifa/ Uelewa<br>• kufahamiana<br>• Utambulisho<br>• Uaminifu<br>• Ushirikiano wa kijamii/ hatua ya pamoja<br>• Uhusiano na eneo | • Kutoa elimu na uhamasishaji/ kuendesha kampeni za kuongeza uelewa<br>• Kutoa fursa za mwingiliano<br>• Kuhamasisha kuhusu malengo/madhumuni ya pamoja<br>• Kushiriki katika ujengaji mtandao<br>• Kujenga uaminifu ndani au na jamii<br>• Kuunga mkono mipango ya kukuza utambulisho wa pamoja, malengo, na uhamishaji wa maarifa kutoka kizazi na kizazi (k.m.makundi ya vijana, Wazee, na wanawake)<br>• Kusaidia uponyaji na usawa wa rangi<br>• Kutenga maeneo yanayofaa kwa hadithi, sheria za kimila na za asili ili kuibua na kuhabarisha juu ya upangaji mradi, taratibu za kiutawala na utekelezaji Kuunda na kusaidia upatikanaji na umiliki wa maeneo ya jadi ikiwa uhamishaji umetokea / unatokea |

*(Jedwali la 3 linaendela)*

| Aina ya Mitaji | Malengo ya kujengea uwezo | Mifano ya shughuli |
|---|---|---|
| Ya kitaasisi | • Uongozi<br>• Uongozi bora<br>• Taasisi/ vyombo vya utawala/ miundo<br>• Utawala bora | • Kufanya tathmini ya ramani ya uongozi na utawala ili kuelewa mifumo ya kiutawala wa jadi na wa kisasa<br>• Kusaidia viongozi wa jamii katika kuimarisha miundo ya kiutawala iliyopo (k.m., warsha za uongozi, mashirika ya kijamii, walezi, waangalizi, n.k.)<br>• Kusaidia na kutumia maono ya jamii na mipango ya matumizi ya ardhi<br>• Kusaidia maendeleo na/au uwekaji kumbukumbu wa sheria na kanuni za jumuiya zinazosimamia matumizi ya maliasili Kutoa msaada kwaajili ya ufuatiliaji and utekelezaji<br>• Kuanzisha mifumo isiyo ya kikoloni na majukwaa kwaajili ya kusuluhisha ugomvi na migogoro<br>• Kutoa elimu kwa viongozi wa jumuiya juu ya usuluhishi wa migogoro/upatanishi<br>• Kusaidia, kutafuta, kuhimiza kurejesha na kufufua taratibu za jadi au za ndani za kuleta amani |
| Ya asili | • Rasilimali<br>• Huduma za mifumo ya kiikolojia | • Kushiriki katika miradi ya urejeshi<br>• Kusaidia kufufua desturi za usimamizi wa jadi na kutoa mafunzo ya mbinu bora za usimamizi<br>• Kutetea maeneo ya hifadhi kupitia Wazawa au wenyeji |
| Ya kiuchumi | • Miundombinu<br>• Rasilimali fedha<br>• Utawala | • Kusaidia fursa za mustakabali endelevu<br>• Kushiriki fursa za uboreshaji wa miundombinu (k.m., barabara, mifereji ya umwagiliaji, majokofu, mkongo)<br>• Kusambaza vifaa vilivyoboreshwa (k.m., zana za uvuvi, vifaa vya kilimo)<br>• Kutoa au kuwaunganisha kwa kutumia mikopo, mikopo midogomidogo, na fedha za kuanzia kwaajili ya kununua vitu muhimu (k.m., mashine ya kusaga ya jumuiya na vifaa vya usindikaji, boti/magari, vifaa vya ufatiliaji etc.)<br>• Mafunzo juu ya bajeti, uhasibu, na usimamizi wa mradi<br>• ufuatiliaji unaosaidia thamani ya kiuchumi ya maliasili<br>• Kufadhili dhana thabiti za uchumi zinazoongozwa na jamii |

Matokeo ya mapitio ya uhifadhi kwa njia ya jamii ya hivi karibuni yanazungumzia umuhimu wa uwekezaji mbalimbali kwa matokeo ya kimazingira.[16,48] Wengi wameonyesha ni aina gani za mtaji pamoja na shughuli za kawaida za kila siku zinazohusishwa zaidi na kuleta ustawi wa binadamu na manufaa ya kimazingira. Za kuzingatia ni zile zinazoimarisha rasilimali watu kwa nijia ya elimu, mafunzo, na msaada wa kiufundi;[48,52] zile zinazoimarisha rasilimali jamii kwa jitihada zake za kujenga uaminifu na kukuza ushirikiano wa jamii;[16,53-54] zile zinazoimarisha za kitaasisi kwa njia ya uwekezaji wa viongozi wa jamii na taasisi kwaajili ya usimamizi wa maliasili ambao hukuza mitaji ya kitaasisi kupitia uwekezaji wa viongoji na taasisi za usimamizi wa maliasili;[16,48,55-58] zile zinazoimarisha mitaji ya kiuchumi kupitia uwekezaji wa miundombinu, biashara, utawala, na usimamizi wa kifedha;[16] na zile zinazounda mitaji mbalimbali (k.m., rasilimali watu, rasilimali jamii, na za kitaasisi) kwa kutengeneza mitandao ya kujifunza na kubadilishana maarifa.[16,59]

## Uongozi wa Jamii na Taasisi

> Angalia **"Nyenzo ya 4: Viongozi wa jamii na Taasisi"** kwa orodha yenye vigezo muhimu katika kuunga mkono viongozi makini wa jamii na taasisi.

Viongozi makini wa jamii na taasisig ni muhimu katika uwakili unaoongozwa na jamii, na ni uwekezaji katika kuimarisha uwezo wa zote mbili na umehusishwa na matokeo chanya ya kimazingira .[16,48,55-58] Kimsingi viongozi ni mtu yeyote mwenye ushawishi, na uongozi huanzia mahali popote and unaweza kuwa wa aina tofautitofauti. Viongozi wanaweza kuwa wa kidunia au wa kiroho, waliochaguliwa au kuteuliwa, wanaume au wanawake, mtu binafsi au kikundi, na wanweza kuwa na sifa nyingi zenye kufanyia kazi matokeo ya kimazingira.[60-62] Ili viongozi na taasisi ziweze kuwa bora katika kuongoza na kujenga imani na uaminifu katika jamii ni lazima jamii iwatambue kuwa halali, wawazi, wawajibikaji, wamoja, wenye kufata haki, wenye kuungana, na wastahimilivu, na wawe na uwezo wa kubadili mazoea na mitazamo ya watu.[63-64] Vigezo hivi muhimu vinapokuwepo, viongozi na taasisi za jumuiya wanaweza kuwa watetezi na wahasishaji wenye nguvu wa hatua ya pamoja,[65] Pamoja na kuunga mkono usimamizi makini wa maliasili kwa kuboresha uratibu, utekelezaji, ufuatiliaji, na utatuzi wa migogoro.[66] Zaidi ya hayo, viongozi na taasisi za jumuiya wanaweza kuendesha mafunzo ya kijamii, na kufanya uenezaji wa ubunifu ndani ya jumuiya na kwingineko.[67-68] Uzoefu umeonyesha kuwa viongozi na taasisi za jumuiya zinapokuwa dhaifu, kwaajili ya rushwa au kupata faida kupitia wasomi, au kuwa na uratibu hafifu na wengine, mara nyingi jumuiya hizi hushindwa kuendeleza shughuli za utetezi mafunzo gani yatakubalika zaidi na.[56] Hivyo basi, unaposhirikiana na jumuiya katika kujengea uwezo kwa viongozi na taasisi za jumuiya, ni muhimu kufanya kazi na jamii kwa karibu ili kubaini ni watu gani na taasisi zipi za kushirikisha, kujua mafunzo gani yatakuwa na muitikio mkubwa na ya kuwa na msaada katika kuongeza maarifa na juzi za ndani, na kama mafunzo haya yanaweza kusaidia kufikia malengo ya uwakili kwa kiwango fulani. Kufanya kazi na viongozi waliochaguliwa na jumuiya na kupitia taasisi zake zilizopo ni muhimu na kuna uwezekano mkubwa wa kupata matokeo chanya na ya kudumu.Tarajia mafunzo hayo kufanyika kwa njia zote mbili huku viongozi wa mitaa nao wakiwa na mengi ya kufundisha mashirika ya uhifadhi, kwa nyongeza ya kile wanachoweza kujifunza kutoka kwetu na wengine katika sekta ya uhifadhi.

g. Hapa, matumizi ya neno "taasisi ya jumuiya" inarejelea makundi mbalimbali (k.m., viongozi, kamati, mashirika ya kijamii, n.k.) yanayosimamia utekelezaji wa mila, kanuni, miongozo, na sera zinazotungwa na jumuiya ili kusimamia maliasili.

## Hatua ya Pamoja na Ushirikiano wa jamii

> Angalia **"Nyenzo ya 5: Hatua ya Pamoja na Ushirikiano wa Kijamii"** kwa orodha yenye rasilimali kuu na sifa za kundi la mtumiaji zenye kuunga mkono uamuzi wa pamoja na ushirikiano wa kijamii.

Hatua ya pamoja kwaujumla inafafanuliwa kuwa hatua inayochukuliwa na kikundi ili kufikia lengo la pamoja[41-44] na ni kiwezeshi muhimu cha utawala bora wa rasilimali za pamoja na uwakili wenye tija unaoongozwa na jamii[69] Kuna jopo la wanafasihi linalojadili umuhimu wa ushirikiano wa kijamii katika hatua ya pamoja, Ambayo kwa upande mwingine huchangiwa na rasilimali mbalimbali pamoja na sifa za wanajamii. kama vile kufahamiana, mwingiliano wa mara kwa mara,utambulisho na madhumuni ya pamoja, kunufaishana, na uaminifu.[44,70,71] Kuna uwezekano mdogo wa sifa hizi kuwepo kwenye jamii ambazo ni kubwa, zenye tofauti, zinakuwa kwa haraka au kubadilika, zenye migogoro, zilizotangaza kutokuwepo kwa usawa au alama za ukandamizaji, zilizotengwa, na kunyang'anywa mali,[16,59,72-73] ambayo ni matokeo ya ukoloni yanayofahamika na simanzi ijayo ya kizazi hadi kizazi. Uchambuzi wa hivi karibuni uligundua miradi ya uhifadhi inayoongozwa na jamii ambayo ilitambua na kuweka wazi masuala ya uaminifu yaliyopo (kiwezeshi muhimu cha ushirikiano wa kijamii) miradi hiyo ilifanikiwa zaidi katika kukuza ustawi wa wanajamii na faida za kimazingira kuliko ambayo haikufanya.[54] Tafiti nyingine zimefanya uchunguzi unaohusiana na umuhimu wa utambulisho na madhumuni ya pamoja katika ushirikiano wa kijamii na hatua ya pamoja inayohitajika kwa ajili ya matokeo yenye mafanikio ya kimazingira.[54] Tafiti hizi zimekuwa na mjadala mkubwa wa kuongeza zaidi ufahamu juu ya umuhimu wa ushirikiano wa kijamii, hatua ya pamoja, kuukubali ukweli mchungu na kutumia uzoefu kama njia ya kujenga uaminifu, madhumuni ya pamoja , pamoja na kuongeza shughuli za uwekezaji zitakazosaidia kujenga na kurekebisha mambo haya muhimu.

## Rasilimali za pamoja, Utawala, na Usimamizi Endelevu wa Maliasili

> Angalia **"Nyezoyal 6: Usimamizi wa rasilimali za Pamoja"** kwa orodha yenye masharti muhimu yanayosaidia utawala bora wa rasilimali za pamoja.

> Angalia **"Nyenzo ya 7: Nyenzo ya Usimamizi wa Maliasili"** kwa mwongozo wa hatua kwa hatua wa kuunda muktadha maalum ili kufuatilia na kutathmini utawala katika ngazi ya jumuiya au taasisi ya jumuiya.

Bidhaa zozote za pamoja ni kitu chochote chenye kupungua wingi au ubora kupitia matumizi, na chenye kugharimu na/au vigumu kuwatenga wengine wasitumie.[45] Sifa kama hizo ni za kawaida kwa rasilimali ambazo nyingi, changamani, zisizotabirika na wakati, na/au zenye kuhamahama (yaani, huondoka kwa uhuru kutoka eneo moja kwenda jingine). Rasilimali nyingi za aina hii ni muhimu kwa mustakabali wa maisha na utambulisho wa wazawa na wenyeji wazawa.[74] Mali ya pamoja ni njia maalum ya kuhusianisha na rasilimali za pamoja, ambapo usimamizi wa rasilimali unafanywa na wote kwa njia ya vikundi vya watumiaji wenye kibali (rasmi au kisicho rasmi; haki rasmi au haki zisizo rasmi) haki za kukipata na matumizi yake (soma sehemu iliyopita kwa maelezo zaidi juu ya haki za kumiliki mali).[75] Aina hizi za mali na usimamizi wa maliasili zinajulikana hasa miongoni mwa Wazawa na wenyeji.

Watafiti wengi wamependekeza kwamba mali ya pamoja na usimamizi wa rasilimali za jumuiya si tu muundo wa utawala bora kwa rasilimali za pamoja, bali mara nyingi huwa na matokeo kwenye usimamizi endelevu wa maliasili,[76-79] huku tafiti nyinyi zikithibitisha kwamba ardhi na vyanzo vya maji vyenye historia ndefu ya kusimamiwa na wazawa na jumuiya za wenyeji (mara nyingi huwa za jumuiya) zimelindwa na kuwa na usimamizi endelevu kadiri ya muda.[80-82] Ardhi na vyanzo vya maji vinavyosimamiwa na wazawa na wenyeji huwa na upotevu mdogo wa misitu hai,[83] uwezo zaidi wa kuhifadhi hewa ya ukaa,[84-85] na msaada mkubwa wa utoaji wa huduma muhimu za mfumo wa kiikolojia[86] kuliko maeneo ya hifadhi yanayoendeshwa na serikali. Ingawa usimamizi wa rasilimali za pamoja unaweza kuzaa matokeo chanya ya usimamizi endelevu wa maliasili, ni muhimu kutambua kwamba matokeo haya hayana uhakika—particularly when faced with an increasing size and pace of external demand for resources. Masharti fulani yanasaidia utawala bora wa rasilimali za jumuiya, na yasipotimizwa, kushindwa kwa jina la "majanga ya jumuiya" kunaweza kutokea.[87] Baadhi ya masharti haya yafaayo ni pamoja na:[69-70]

- Mipaka ya rasilimali imefafanuliwa wazi,
- Sheria za matumizi ya rasilimali ambazo zimeundwa kulingana na jamii husika zipo, kuwepo kwa matumizi ya rasilimali ambayo yameundwa kulingana na wenyeji, na faida wanazozipata watu binafsi zinalingana na gharama,
- Walioathiriwa na sheria wanaweza kushiriki katika kurekebisha sheria
- Ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali hufanyika na wale wanaofatilia wanawajibishwa na watumiaji wa rasilimali,
- Adhabu kwa wavunja sheria inalingana na ukubwa wa kosa, na
- kuna njia za haraka, zenye gharama nafuu za kutatua migogoro.

Kwa mifumo ya mipakani yenye kuchukua sehemu kubwa, kama vile pwani, chemichemi, mito, au maziwa makubwa, uratibu wa jamii na wanajamii zaidi ya ngazi ya kaya au jamii unakuwa muhimu katika kusimamia rasilimali pamoja. Kwasababu ya muunganiko kati ya watumiaji wa rasilimali unaofanya kazi katika sehemu kubwa, ushirikiano na maelewano vinahitajika ili kuhakikisha mgawanyo wa haki wa rasilimali na faida. Kihistoria, tofauti mbalimbali za taasisi za kijamii zimeunda, zimefuatilia, na kutekeleza sheria zao wenyewe za kuchimba, kusimamia, na kuunda rasilimali hizo. Jumuiya za wenyeji zinaweza na zimesimamia rasilimali zao wenyewe—ndani ya mipaka mikubwa ya juu/chini ya mto au miunganiko mipakani—hata kama haki za kimila hazitambuliwi na serikali.




# Chunguzi kifani



## Uongozi wa Jamii na Ujengeaji uwezo kitaasisi kwenye Ukingo wa Emerald

Ukiwa na ukubwa wa ekari milioni 100 (hekta milioni 40), Ukingo wa Emerald ndio mfumo mkubwa zaidi wa misitu ya mvua maeneo ya pwani uliosalia duniani. Kundi hili la misitu minene na bahari huelekea kaskazini mwa Peninsula ya Olympiki ya Jimbo la Washington, kwa kupitia pwani ya jimbo la British Columbia nchini Canada na makubaliano ya msitu mnene wa Bear, na kutokea kwenye ukanda mwembamba wa kijiji kilicho Kusini-Mashariki mwa Alaska. Walinzi wazawa wameshazijua haki na mamlaka juu ya rasilimali hizi—hivyo Mpango wa Emerald Edge umekuwa ukilenga kuimarisha uwezo wa Wazawa na Wenyeji kwaajili ya kuendeleza uwakili mzuri. TNC inafanya kazi ili kuunga mkono uongozi wa jamii na utawala, pamoja na kukuza fursa za kiuchumi zinazoboresha mustakabali wa maisha ya wenyeji, kutoa motisha na elimu ya nyongenza kwaajili ya usimamizi endelevu wa maliasili.

Mpaka kufikia hapa, TNC imetekeleza mipango kadhaa maalum inayokusudiwa kujenga "ngazi ya fursa" kwaajili ya wazawa. Kusaidia Programu ya Mawakili Wazawa wanaochipukia (SEAS) —au "vijana kwenye programu ya ardhi"—inalenga kushirikisha, kuendekleza, kuandaa, na kuwawezesha vijana wazawa ili kuja kuwa mawakili wa kizazi kijacho wa mahali fulani. Vijana hutembelea maeneo yao ya kitamaduni ili kuunganika tena na ulimwengu wa asili, kushiriki shughuli za kimila, na kujifunza kutoka. Mpango mwingine ni wa, Walinzi Wazawa, unawasaidia Walinzi wazawa kudhibiti ufuatiliaji wa maeneo yao na kuendeleza kazi ya mababu zao na kuheshimu maliasili muhimu na rasilimali zao za kitamaduni kupitia taasisi za kitamaduni na miundo ya utawala Walinzi hawa huangalia usalama wa vyakula muhimu, kijamii, na kenye sherehe, kwa kuzingatia matumizi ya rasilimali katika eneo lao lote na kuchangia katika kufanikisha utekelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya mipango ya matumizi ya ardhi na bahari. TNC na washirika walitayarisha Zana na Walinzi Wazawa *ili kuwezesha upanuzi wa programu ndani na nje ya British Columbia. Kuufanyia kazi mradi wa* Mfuko wa Mandhari ya Baharini nchini Canada unaonzisha programu za Walinzi kwenye jimbo la Alaska kwa kutumia njia zote mbili zana na ufadhili wa uhifadhi kifedha na kufanikisha maono yao kwa siku zijazo.

**PICHA YA AIKONI**
Maeneo ya Mfumo wa VCA

**NCHI KAVU** **MAJI SAFI** **PWANI**

Upanuzi wa mpango huu wa kujengea uwezo umeendelea kukuwa katika Ukingo wa Emerald kwa njia ya Utoaji wa elimu muhimu ya kiufundi na uwezo wa kifedha ili kuunga mkono maono ya jamii na mipango ya matumizi ya ardhi kwaajili ya mji wa Ahousaht katika British Columbia. Uongozi wa mabadilishano uliofuata na kuratibiwa kati ya Ahousaht na Haida Nations uliusaidia uongozi wa Ahousaht kuimarisha mazungumzo yao na Serikali ya Mkoa na kufikia mamlaka ya utawala bora zaidi. Mji wa Ahousaht pia ulianzisha Programu **ya Ulinzi Pwani**, ambao umezaa juhudi za kuchora ramani kwa kushirikiana na TNC (ambao walitoa usaidizi wa kiufundi wa uchoraji ramani) ili kuainisha maeneo na rasilimali zao, yakiwemo maeneo ya utangamano wa maeneo yenye umuhimu wa kitamaduni. Haya yote yamesaidia kuimarisha hatua ya pamoja, utawala bora, na mazungumzo ya waahousaht na wadau wa nje. Kwa mfano, nchi ya Ahoisaht ilisaini makubaliano mapya hivi karibuni na British Columbia ili kutoa mpendekezo ya pamoja kenye Baraza la Mawaziri kwaajili ya utekelezaji wa dira yao juu ya matumizi ya ardhi ambao utaleta uhifadhi mpya, misitu, maeneo ya maendeleo ya kiuchumi na makubaliano ya utawala.

## Usimamizi wa Uvuvi wa kwenye Maji safi katika Ziwa Tanganyika

Kwa zaidi ya muongo mmoja, TNC imekuwa ikishiriki katika mipango ya uhifadhi kwa njia ya jamii na usimamizi endelevu wa uvuvi katika bonde la Ziwa Tanganyika la Afrika Mashariki. Ziwa Tanganyika ni la pili duniani kwa ukubwa, likiwa na asilimia 17 ya maji safi yaliyo kwenye uso wa dunia. Bonde hili ni sehemu ya mazalia ya viumbe hai wa majini na nchi kavu na linajulikana zaidi kwa kuwa na zaidi ya spishi 250 zinazojulikana za samaki wa mapambo, ambapo asilimia 98 katika hizo hupatikana kwenye bonde hili pekee duniani kote.Mtandao changamano wa mwingiliano kati ya mwonekano wa ziwa, biokemia, ongezeko la kina cha maji, na mifumo ya kiikolojia ufukweni imezaa uvuvi wa ndani wenye mafanikio unaowasaidia watu wapatao milioni 12 kama chanzo cha protini na mapato. Samaki huchangia asilimia 40 ya protini ya wanyama kwenye vyakula vya asili, na inakadiriwa kuna wavuvi hai 95,000 kenye ziwa hilo. Nchi zinazofikiwa na Ziwa Tanganyika ni—Tanzania, Jamhuri ya KIdemokrasia ya Kongo, Zambia, na Burundi—nchi hizi zina njia tofauti za kushiriki usimamizi wa uvuvi, na kimsingi ziwa linabakia kuwa la uvuvi mdogo wa kujikimu na wa wazi. Aidha, kanda hii ina ongezeko kubwa la watu na viwango vya juu vya umasikini, hivyo huongeza matumizi ya maliasili ambayo tayari imeshatumika kupita kiasi.

Mwaka 2012, TNC na washirika wake walianzisha mradi wa **Mradi wa Tuungane** nchini Tanzania kwa ajili ya kutoa majawabu katika kuboresha familia, uvuvi, na misitu yenye afya, kwa kutumia mbinu jumuishi yenye kugusa masuala ya afya na ya mazingira kwa pamoja. Majawabu haya kwa ujumla wake yanatupa matumaini ya matokeo mengine na ya kudumu kuliko ile mbinu ya kitamaduni zaidi ya kujitenga na wengine kwa sababu kawaida ya uhifadhi ni kuboresha pia maisha ya watu. Usimamizi wa uvuvi chini ya mradi huu umelenga katika kuanzisha Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe (BMUs) kusimamia rasilimali za uvuvi, kutoa mafunzo na zana za kuimarisha uongozi kwa BMUs na uwezo wa jamii, kuandaa mifumo ya ufatiliaji inayoongozwa na jamii na



© AMI VITALE

kuunda mifumo ya kifedha ambayo italipia gharama zote za usimamizi wa uvuvi. TNC inataka pia kuweka wazi athari za kwenye Ziwa Tanganyika. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (LTA)—Baraza la Utawala la Kanda ya Ziwa Tanganyika lenye jukumu la kusimamia maendeleo endelevu na maliasili za kanda—pamoja na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa. Jumuiya ya Kimataifa ya Uhifadhi wa Mazingira, na Kituo cha Mazingira Duniani, TNC inalenga kukuza taasisi za uvuvi za usimamizi shirikishi na kujenga hifadhi za samaki za jamii (maeneo yaliyohifadhiwa kwa kuzaliana) ziwani kote.

Uongozi makini na uwezo ni muhimu katika kuanzisha taasisi imara na kuratibu hatua za kusimamia rasilimali za pamoja. Kwa mfano, nchini Tanzania, viongozi wa vijiji huchaguliwa kila baada ya miaka 5. Viongozi hawa husimamia jumuiya pamoja na kamati tendaji. Viongozi wa BMU, wanaosimamia sheria ndogo za uvuvi, huchaguliwa kila baada ya miaka mitatu. Masharti ya ofisi juu ya uongozi yanaielekeza TNC kuendelea kujenga uhusiano na viongozi wapya na kutoa mafunzo endelevu kuongeza ufanisi wa BMU, uzalishaji kipato, na ununuzi wa ndani ya jumuiya bila BMUs. Masharti ya uongozi yameundwa kuyumbishwa ili viongozi wa ngazi za juu ili wawe na jukumu la kuwatambulisha warithi taratibu za utawala. TNC inajikita zaidi katika kuunga mkono uongozi thabiti na wenye usawa kijinsia unajitolea kutekeleza kwa ufanisi shughuli za uhifadhi katika kiwango cha BMU na kuongeza uwezo wa kifedha wa BMU. Ingawa kuna sera ya nchi inayoamuru asilimia 30 ya nafasi za uongozi lazima zishikiliwe na wanawake (pia imeongezwa katika sheria ndogo za in BMU), wanawake wenye nafasi uongozi wanaweza kuwa na ukomo katika mchango na ushiriki wao kutokana na kanuni za kitamaduni na za kidini. Ili kukabiliana na changamoto hizi, mradi huwezesha uteuzi wa makusudi wa viongozi wa kike, huandaa mafunzo yanayolenga kuongeza motisha, kujiamini, na kuwashirikisha kikamilifu wenzi wa wanawake walioteuliwa kama kama sehemu ya mchakato.

Kuwa na uongozi thabiti katika ngazi ya kijiji, sheria ndogo zilizo wazi na muundo wa taasisi, kushikwa mkono na serikali kwenye masuala magumu kiutekelezaji, Aidha, Maeneo Shirikishi ya Usimimizi wa Uvuvi (CFMA), yanayojumuisha shirikisho la mitandao ya BMU, yameundwa kwa kufuata mwongozo wa Tanzania. CFMA zimefanikiwa katika maeneo ambayo mitandao hii inaweza kusaidia na kufanyakazi na BMU za binafsi kwa kufanya doria kubwa kwaajili ya kulinda maeneo makubwa yaliyotengwa kama hifadhi za samaki.

Hata hivyo, ili kuifanya BMU kuwa endelevu kifedha itahitaji mabadiliko ya kisera na kiutendaji ambayo yanaweza kufanywa na serikali ya Tanzania pekee. TNC, kwa kushirikiana na serikali na LTA, inafanya majaribio ya mfumo wa biashara ya uvuvi, ambapo mafanikio yake yataigwa kwa njia ifaayao katika maeneo mengine ya Ziwa Tanganyika ili kuimarisha uhifadhi wa kudumu wa rasilimali za uvuvi. Ingawa mradi wa Tuungane umepata mafanikio makubwa, kazi za uhifadhi wa maji safi katika jamii ndio kwanza zinaanza safari yake kuelekea kwenye uendelevu wa kifedha. TNC inafanya kazi na washirika ili kutumia uchambuzi wa mnyororo wa thamani na hutumia motisha za soko ili kuhakikisha kwamba wavuvi walio ndani ya BMUs zinazosimamiwa vizuri wanapata faida ya kifedha ya mtu binafsi na/au ya pamoja kwa kipindi kirefu. Hatua ya kwanza ni kuiomba serikali kurejesha baadhi ya asilimia (asilimia10-15) ya mapato ya Serikali (ikiwa ni pamoja na gharama za usafirishaji wa mazao yatokanayo na uvuvi) ambayo inasimamiwa na BMUs kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali ya Wilaya. Mafanikio ya mradi yanategemea na kuwashirikisha kikamilifu wazawa na wenyeji kwenye majukumu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwaweka kama wamiliki wa ardhi na rasilimali, wamiliki na washirika, na kama viongozi na wanufaika. Kuanzisha na kuimarisha taasisi za ndani kunatazamwa kama msingi wa kudumu na uthabiti, na mradi unaongeza juhudi zake katika suala hili.

# Nyenzo na Rasilimali

## NYENZO YA 4: UTAMBUZI — VIONGOZI WA JAMII NA TAASISI

Viongozi imara wa jumuiya na taasisi ni msingi wa uhifadhi unaoendeshwa na jamii. Vigezo muhimu katika nyenzo hii vinaweza kutumika kutathmini ufanisi wa zote mbili, ambazo kwa upande mwingine huleta uaminifu na imani ambayo watu wanaweza kuiweka ndani yao. Taarifa hii inapaswa kujadiliwa na jumuiya, au taasisi zake wakilishi, wakati wa uchambuzi wa hali kwa njia ya mahojiano na watoa taaarifa wakuu na majadiliano ya makundi lengwa.Unaweza kutumia orodha kuingiza majibu yako kwa kila swali ili kubaini maeneo muhimu yanayokuwa na fursa za kusaidia shughuli zinazofaa kujenga uwezo sahihi - in shuguli za kujengea uwezo kwa kushirikiana na with Wazawa na wenyeji.

## NYENZO YA 5; UTAMBUZI— HATUA YA PAMOJA NA USHIRIKIANO WA KIJAMII

Hatua ya pamoja ni hitaji la lazima la utawala bora na inaathiriwa na rasilimali fulani na sifa za jumuiya. Taarifa hii inapaswa kujadiliwa na jumuiya, au taasisi zake wakilishi, wakati wa uchambuzi wa hali kwa njia ya mahojiano na watoa taaarifa wakuu na majadiliano ya makundi lengwa. Unaweza kutumia orodha kuingiza majibu yako kwa kila swali ili kubaini maeneo muhimu yanayokuwa na fursa za kusaidia shughuli zinazofaa kujengea uwezo kwa ushirikiano wa wazawa na wenyeji.

## NYENZO YA 6: UTAMBUZI—USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA PAMOJA

Usimamizi wa rasilimali ya pamoja unaonekana ndani ya maeneo ya wazawa na wenyeji kwa sehemu kubwa zaidi. Tunapoangalia ni kwa namna gani tunaweza kusaidia jamii katika usimaimizi endelevu wa maliasili, ni muhimu kutathmini masharti nane yanayoathiri ufanisi wa mifumo hii ya usimamizi wa mali.[69-70] Taarifa hii inapaswa kujadiliwa na jumuiya, au taasisi zake wakilishi, wakati wa uchambuzi wa hali kwa njia ya mahojiano na watoa taarifa wakuu na majadiliano ya makundi lengwa.Unaweza kutumia orodha kuingiza majibu yako kwa kila swali ili kubaini maeneo muhimu yanayokuwa na fursa za kusaidia shughuli zinazofaa kujengea uwezo kwa ushirikiano wa wazawa na wenyeji.

## NYENZO YA 7: MWONGOZO WA HATUA KWA HATUA—NYENZO YA USIMAMIZI WA MALIASILI

Mwongozo huu umeundwa ili kuwafundisha wahifadhi dhana za msingi na kuwapatia nyenzo ili kuelewa vyema, kutathmini, na kuunga mkono usimamizi makini wa rasilimali katika mandhari na mandhari ya bahari. Mwongozo huu umeundwa kusaidia katika kuelewa vigezo muhimu vya usimamizi bora wa maliasili na kutumika kama utambuzi.

Nguzo ya 3

# Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali na Kufanya Maamuzi


© JUAN ARREDONDO

## Maarifa, Ushahidi na Mazoea

**DONDOO MUHIMU**

- Mazungumzo ya wadau mbalimbali na kufanya maamuzi (MSD) ni mazuri zaidi katika mazingira magumu yenye wahuska mbalimbali ambao wana maslahi tofauti tofauti kwenye ardhi, maji au rasilimali.
- Mazungumzo ya wadau mbalimbali yanaweza kuwa na malengo mengi—kuanzia kupashana habari, usuluhishi wa migogoro hadi kufanya maamuzi —na yanaweza kutokea katika ngazi ya chini, mkoa au taifa/kimataifa. Hata hivyo ilikufanikiwa na kuwa na ushawishi, kiwango cha majadiliano na maamuzi ya wadau mbalimbali inatakiwa kiendane na kiwango cha jambo lenyewe na wanaohusika.
- Mikakati ambayo inahusisha mazungumzo ya wadau mbalimbali na kufanya maamuzi inapaswa kuambatana na mikakati ambayo huongeza uongozi wa Wazawa na wenyeji au uwezo wa kujihusisha sambamba na wadau kuhusu namna ya kujihusisha vyema na kwaheshima na Wazawa na wenyeji.
- Uwezeshaji wenye ustadi, wa mara kwa mara wa MSD ni muhimu kwa ajili ya kutengeneza uhusiano na mshikamano wa kijamii miongoni mwa wadau mbali mbali na kusaidia majadiliano, kujifunza kwa pamoja na usuluhishi wa migogoro kwa muda mrefu.
- Mabadiliko ya uongozi ni mambo ya muhimu kuzingatia kwenye mazungumzo ya wadau mbalimbali na kushindwa kutambua na kuyashuhulikia inaweza kuendeleza ukosefu wa usawa uliopo katika mfumo.
- Kutegemea na mfumo na mahitaji. mazungumzo ya wadau mbalimbali yanaweza kupangwa kama vikundi kazi vya muda mfupi au taasisi za muda mrefu –majukumu ya kudumu au majukwaa kwa ajili ya mazungumzo yanaweza kuwa muhimu endapo utatuzi wa migogoro unaoendelea na uamuzi unaoendana na kanuni au makubaliano vitahitajika.

**MANENO YA MSINGI**

**Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali**–jukwaa linalowakutanisha wahusika wenye maslahi ya aina moja kwenye jambo au maamuzi, kupashana habari na maarifa ya kitaasisi, kuleta majawabu na mazoea mazuri yanayoendana, kuongeza uaminifu/ kutatua migogoro au kufikia maamuzi. Jukwaa hili laweza kuwa la muda mfupi au la muda mrefu, linaweza kuwa katika kiwango tofauti na linaweza kuunganisha mazungumzo ya wadau mbalimbali wengine.

**Mwenye Haki ya Umiliki**–ni mtu au kundi la watu wenye haki zinazotambuliwa kuridhia au kutoridhia katika maamuzi kuhusu ardhi, maji, au usimamizi wa rasilimsli. Tunawatambua wazawa kama "Wenye Haki ya Umiliki" wamepewa haki yao inayotambulika kimataifa hivi karibuni inayotajwa kwenye tangazo la Umoja wa Mataifa la Haki za Wazawa, tangazo la mwaka 2007.

**Mdau**–mtu au kundi la watu wenye maslahi katika ardhi, maji au rasilimali wakati mwingine hujulikana kama "wenye maslahi"

## Kuelewa Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali na Kufanya Maamuzi

Katika muktadha wowote wa usimamizi wa maliasili kuna wahusika mbalimbali au makundi yenye maslahi kwenye ardhi,maji, au rasilimali na mara nyingi wahusika hawa wanaweza kuwa na ushindani na mlundikano wa malalmiko au kutumia haki. Wadau wengi wanaweza kushawishi matumizi na usimamizi wa maliasili hasa pale ambapo haki hazipo wazi,hazijarasimishwa, au rasilimali zimeachwa kiholela.Mazingira ni magumu yakihusisha mabadiliko ya uongozi wa mara kwa mara yamejikita kwenye historia ya ukosefu wa usawa inapofikia kwenye ushirikishaji, hasa kwa wazawa na jamii. Wazawa hususani wanaotambulika kama "Wenye Haki ya Umiliki" sio "Wadau" kwa kuzingatia na kuheshimu haki zao zinazotambuliwa kimataifa.kuridhia au kutoridhia kwenye ufanyaji wa maamuzi yanayohusu mipaka yao au rasilimari zao kwa kuongezea nchi yao,mkoa au haki za nchi zinazohusiana na wazawa.

Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali (MSD) yanalenga kuwakutanisha pamoja wahusika wenye haki ya umilikina wadau.MSD yana mengi ya pamoja kwenye utawala na vipengele vya uwajibikaji wa pamoja ambavyo vilivyoelezwa kwenye sehemu ya "Uongozi Imara na Uwezo wa Kuongoza" (Nguzo ya 2 ). Hata hivyo tofauti kwa nguzo hiyo ambayo imejikita kwenye kujengea uwezo ndani ya jamii au taasisi ya jamii, mazungumzo ya wadau mbalimbali yanajikita kwenye uwezo na ushirikiano baina ya makundi/wadau ambayo huja na mahitaji na changamoto zake na inaweza kufikia kiwango cha juu.

Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali (MSD) kama yakibuniwa na kutekelezwa yanaweza kutumika kufikia malengo mablimbali, Kama vile kuongeza viwango vya imani na mshikamano wa kijamii baina ya wahusika, kupeana taarifa na maarifa ya kitaasisi, kuleta majawabu na mazoea bora, kukuza ushirikiano na mafunzo mbalimbali, kufafanua haki, kusimamia usawa kiuongozi kwa wanao husika, husuluhisha migogoro au kufikia maamuzi kwa muda muafaka,rasilimali na maandalizi, (MSD) yanaweza kuwa chombo chenye ufanisi kwa ajili ya kuunganisha pamoja majimbo tofauti kuleta uelewano kwenye ugumu, kwenye mambo yenye sura tofauti tofauti na kwa baadhi ya mambo yenye migawanyo. kwa kweli,mapitio ya kimfumo ya hivi karibuni na uchambuzi imebainika kuwa mazungumzo ya wadau mbalimbali ni muhimu kwa mafanikio ya uhifadhi wa kutumia jamii na kwamba miradi ambayo huhusisha shughuli hizo huwa na uwezekano mkubwa wa kufikia ustawi chanya kwa binadamu na matokeo ya kimazingira.

Kwa upande wa kufanya maamuzi, MSD, majukwaa yanaweza kuhusisha wadau ambao hufanya maamuzi, wale ambao hushawishi kwenye maamuzi sambamba na wale wanaoathiriwa na maamuzi. Katika mazingira haya ni muhimu kubainisha lengo na mamlaka na ushiriki wa wadau mbalimbali katika kutengeneza mpango au kufanya maamuzi kwa kuwa huhusiana na ubia na wazawa na wenyeji. Mashirika ya uhifadhi yanaweza kusaidia na kuimarisha uwezo wao wa kushiriki, kushawishi na kufanya maamuzi kwenye majukwaa hayo, vilevile kuwaelimisha wadau wengine namna ya kuwahusisha wazawa na wenyeji kwa uthabiti na hekima.Jedwali namba 4 linaorodhesha baadhi ya majukumu ambayo mashirika ya uhifadhi yanaweza kufanya kwenye MSD huku ikizingatiwa kwamba mashirika haya yanaweza kuwa na majukumu mbalimbali kwenye MSD moja au MSD mbalimbali.

**Jedwali Na.4:** *Wajibu wa Mashirika ya Uhifadhi kwa MSD.*

| Wajibu | Maelezo |
|---|---|
| Mratibu | Kupanga kikao kwa wadau mbalimbali kushiriki mazungumzo yaweza kuwa kwa kugharamia majukwaa |
| Mwezeshaji | Kuwezesha mazungumzo yenyewe ikiwemo kusimamia agenda, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wamaridhiano/ mwafaka |
| Mjenga uwezo | Kujenga uwezo wa wahusika mbalimbali ili kuhusiana wao kwa wao thabiti na kwa kuheshimiana. |
| Mtoa msaada | Kugharamia na kutoa msaada wa vifaa kwa uongozi wa wazawa na wenyeji unaposhiriki kwenye MSD hasa pale ambapo kusafiri huwa ni muhimu. |
| Mtekelezaji | Huwasaidia wanaoshiriki na mashirika katika kutekeleza maamuzi, mipango na mahitaji ya ufuatiliaji ambayo huibuka kutoka kwenye mazungumzo ya wadau mbalimbali na kufanya maamuzi (MSD). |

MSD inaweza kufanyika kati ya ngazi nyingi kuanzia ngazi ya chini kwa mfano jamii moja, shirika au serikali ya mtaa yenye maslahi kwenye rasilimali mfano, chama cha watumiaji wa maji ya visima, mipango ya pamoja ya usimamizi wa wavuvi kwa ngazi ya mkoa inayohusisha wahusika mbalimbali kwa mamlaka moja au zaidi (mfano, Jukwaa la Soko la Amazonia la Kupunguza Ukataji Miti Para, Brazil) kwa ngazi ya dunia inayoendelea kwenye ngazi yaNchi au ngazi ya kimataifa. (Shindano la Micronesia la Kuhifadhi kwa Ufanisi asilimia 30 ya rasilimali za majini zilizopo karibu na ufukwe, mkataba wa mfumo wa mabadiliko ya tabia ya nchi wa umoja wa mataifa). Kwa umakinifu, kiwango muafaka cha mazungumzo ya wadau mbalimbali na kufanya maamuzi (MSD) hutegemea kiwango cha jambo na watekelezaji/ watendaji wanaohusika. Zaidi, inawezekana kuwa MSDs mengi yanayopishana yanayoshughulikia jambo kwa namna tofauti na MSDs yanayofanyika kwa muda mfupi au ya kudumu.Mashirikia viungo ambayo mara nyingi ni mashirika yasiyo ya kiserikali au taasisi za utafiti zinaweza kubeba majukumu kama wawezeshaji kujenga mahusiano miongoni mwa watekelezaji mbalimbali na kusaidia majadiliano, ujifunzaji jumuishi na utatuzi wa migogoro.

MSD ni ya muhimu kwa mifumo yote ya kiikolojia ya nchi kavu, pwani na maji safi kwani kila muktadha unahusisha watekelezaji ambao wakati mwingine wana maslahi tofauti. Hata hivyo, MSD ni ya muhimu hasa kwenye mifumo ya maeneo ya pwani na maji safi kwa sababu ya haki mbalimbali na muundo wa umiliki katika maeneo haya ambayo watekelezaji mbalimbali au taasisi zinaweza kuwa na haki kwa rasilimali hiyohiyo. Pale ambapo panaweza kuwa na watumiaji mbalimbali (wakiwemo walio nje ya mahali ilipo rasilimali) mahali ambapo kuna haki chache "Kipekee" au haki binafsi na "{kwa upande wa mito na mikondo} ambapo watumiaji wa mikondo wa maeneo ya juu wanaweza kuathiri ubora na kiasi cha rasilimali kwa watumiaji wa mabondeni kwa kuzingatia nyongeza hizi za magumu ya usimamizi wa rasilimali asilia katika maeneo ya maji safi na pwani, MSD mara nyingi ni mkakati muhimu kwa kuzitazama changamoto hizi katika kuyatambua mapungufu ya serikali,kuna hatua kubwa kuelekea usimamizi gatuzi wa madaraka ambao unatoa upendeleo kwa mbinu ya ufanyaji maamuzi jumuishi na shirikishi

## Ufanisi wa Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali na Kufanya Maamuzi (MSD)

ANGALIA **"Nyenzo ya 18: Sifa muhimu za mazungumzo yenye ufanisi ya wadau mbalimbali na kufanya maamuzi"**

ANGALIA **"Nyenzo ya 19: Mabara ya Jamii"** kwa ajli ya muongozo kwa mbinu ya MSD ambayo hujikita katika kuyakutanisha makundi tofauti ya watu walio katika mgogoro wa matatizo magumu na yenye changamoto na kuzitafutia majawabu ya pamoja.

Mambo mbalimbali yanaathiri ufanisi wa MSD. Kwa mfano, jambo linalowasukuma wote kushiriki ni uhalisia wa jambo lenyewe.Pale ambapo kuna changamoto ya usimamizi au jambo ni la dharura msukumo wa kijamii kwa wote kushirki unakuwa ni mkubwa hasa pale ambapo utegemezi baina ya wadau unapokuwa dhahiri. Kwa kuongezea ni muhimu kuhusisha watekelezaji wote – ambao ni wenye haki ya umiliki husika na wadau ambao wana maslahi ndani na wanaathiriwa na changamoto ya usimamizi au jambo sambamba na wale wenye maarifa kwa ajili ya kuwezesha kiujuzi zaidi. Endapo MSD sio chombo cha kufanya maamuzi (kwa mfano kuratibu upeanaji wamaarifa au usuluhishi wa migogoro) lazima kuwe na kiunganishi kwenye mchakato wa kufanya maamuzi ili kuwa na ushawishi.

MSD hufanikiwa zaidi endapo:

- yatapokea migogoro na mahusiano ya ndani na nje ya kundi, kutoa fursa kwa agenda za mtekelezaji mmoja mmoja na mfarakano, ilhali mazingira yakiwekwa kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya jumla (kuliko kujikita kwenye malengo jumuishi na maelewano ya timu),

- watafanya majaribio kwa utaratibu kwa mitazamo tofauti na kuleta majawabu ya pamoja, wakipiga hatua moja kwa wakati mmoja na kujijenga kupitia taarifa iliyopatikana kupitia majaribio (kuliko kusisitiza makubaliano kuhusu tatizo, suluhisho na mpango kabla hatua haijachukuliwa), na

- kujikita kwenye wajibu wa washiriki katika kuendeleza hali iliyopo na kubuni suluhisho mbadala (kuliko kujikita kwenye kubadili yale ambayo yanafanywa na wengine).

Hii inaungwa mkono na wanaopenda mbinu shirikishi ya kumaliza matatizo sugu ya jamii, ambayo ni aina moja. Wapo ya MSD ambayo ni maalum kwa maswala changamano na yasiyo tabirika ambayo huhusisha washiriki tofauti. Mara nyingi wenye mitazamo na uelewa wa tatizo. Mbinu shirikishi ya kumaliza matatizo sugu ya jamii kwenye mabadiliko ya mifumo hutegemea kuitisha kitengo kidogo cha mfumo mkubwa zaidi kwa kutumia uwezeshaji wenye ujuzi mkubwa. Mbinu hizo huvunja uongozi na kukuza mahusiano, kufahamu asili ya mfumo wote ikiwemo utofauti wa mitazamo ya tatizo, kutafakari kuhusiana na majukumu mbalimbali ndani ya mfumo na kubuni kwa pamoja au kufanya jaribio lenye majawabu yanayowezekana. Mchakato huu mara nyingi hupelekea kwenye mawazo ya kiubunifu na kupeleka mbele maendeleo ambapo hapo awali maswala "yalikwama".

Hadi sasa ushahidi kuhusu ufanisi wa MSD katika kufikia malengo ya uhifadhi bado unaibuka, program imara za tathmini na ufatiliaji zinaweza kusaidia kuziba haya mapengo ya maarifa. Uchambuzi wa mifano ya MSD unadhihirisha kwamba matokeo chanya kwa mafanikio ya kijamii – kama vile utambuzi wa haki, kuongezeka kwa watu, kupata habari, na usalama wa umuliki vimeshuhudiwa kwenye mambo mengi: hata hivyo hili linaonekana kuhusiana kwa ukaribu na ngazi na ubora wa ushiriki kwa wenyeji kwa mfano, Uchambuzi wa MSD kadhaa ulioshinikizwa na Kituo cha Utekelezaji wa Sheria ya Misitu, Utawala, na Biashara cha Umoja wa Ulaya (EU-FLEGT) kilibaini uhusiano wa jumla baina ya nguvu ya ushirika na kiwango cha athari chanya katika jambo lililofanyiwa mapitio. Wakati huo huo nchinI Brazil ardhi oevu ya Pantanal, uhifadhi na shughuli za serikali zilijaribu kuhakikisha uvuvi endelevu kupitia mbinu ya usimamizi wa pamoja chini ya Tume ya Udhibiti inayoundwa na wabunge, wanasayansi, na watekelezaji. Ukosefu wa ushiriki wa uvuvi kwenye MSD umepelekea kukosekana kwa uelewa wa mahitaji ya usimamizi, wavuvi kutowaamini wanasanyansi wa mjini walio kwenye MSD,na kutofuata kanuni.




© TIM CALVER





# Chunguzi Kifani

## Mazungumzo ya Wadau mbalimbali juu ya Ziwa Tonle Sap la Combodia na Maeneo yenye Mafuriko

ICON LEGEND
VCA Framework Biomes

- NCHI KAVU
- MAJI SAFI
- PWANI

Ziwa Tonle Sap la Combodia ni kubwa, ni la msimu, linapakana kwenye majimbo matano ya Cambodia na linatiririsha maji kwenye mfumo wa Mto Menkong. Mgogoro mkubwa umeibuka kwa watumiaji wa maeneo ya juu na wale wa mabondeni kutokana na ushindani wa kitaifa na kimataifa. Vyanzo vya ndani vya ushindani wa rasilimali vipo ndani ya sekta ya uvuvi, vilevile baina ya sekta ya uvuvi na sekta nyingine kuhusisha migogoro baina ya uvuvi na umwagiliaji wa mpunga msimu wa kiangazi. Upanuzi wa kilimo cha mpunga mara yingi hupewa nguvu na wawekezaji wenye nguvu kutoka nje ya wenyeji, wakibuni maeneo ya umwagiliaji binafsi ambayo huondoa matumizi ya kimila ya wenyeji.

Kuutatua mgogoro wa sekta ya uvuvi, serikali ya combodia ilibadilisha sera ya Taifa kutoka kwenye udhibiti mkuu wa biashara kubwa ya uvuvi kwenda kwenye aina ya usimamizi wa utatuzi wa pamoja unaojiegemeza kwa mashirika ya jamii ya wavuvi (CFO). Ugeni wa CFO ulimaanisha kwamba uhalali wao, uongozi wao na uwezo wa utawala wao ulikuwa duni kwa hiyo ushindani wa ndani kwa rasilimali za uvuvi uliongezeka kwa kadri watumiaji walivyojitahidi kutafuta haki chini ya mfumo mpya au kwa kujinufaisha na mapungufu ya utekelezaji ambayo yalisababisha kusambaa kwa uvuvi haramu.

Kuongeza uwezo wao wa utawala, CFO zilitumia mchakato shirikishi na wadau mbalimbali kuupanga upya usimamizi na kuboresha utekelezaji. CFO pia ziliongeza uwezo wao katika kutatua migogoro yao ya kijimbo na ile ya ndani ya sekta kwa upande wa msimu wa kiangazi vyama vya wakulima wa mpunga vilifanya makubaliano ya mdomo mbele ya idara ya kilimo na uvuvi za mkoa ambapo baadae yalirasimishwa na uongozi wa wavuvi. CFO pia ziliongeza uwezo wao wa kuomba msaada na serikali ili ibadili au kuruhusu misamaha kwenye kanuni zilizopo hii ilipelekea kuanzishwa kwa mradi wa majaribio ulioanzisha uvuvi wa kibiashara chini ya usimamizi wa wenyeji, na ulinzi ili kuhakikisha ulinzi wa kutosha wa rasilimali na kugawana faida. CFO pia zinajihusisha na kuziunganisha jamii zilizo kando ya ziwa (kupitia mfululizo wa matukio ya sokoni) na kwa mtandao wa ngazi ya chini wa kitaifa unaowakilisha jamii za wavuvi.

Mafanikio ya mchakato shirikishi wa wadau mbalimbali yalikuwa makubwa kiasi kwamba mtandao wa ngazi ya chini unaowakilisha jamii ya wavuvi ulirekebisha utawala wake wa ndani na kuongeza ushirikiano wa mamlaka ya serikali na sekta rasmi zisizo za kiserikali. Usimamizi wa uvuvi pia ulipendekeza kujumuisha mchakato huu kwenye utekelezaji wa mabadiliko yanayoendelea kwenye uvuvi. Matokeo yake yanaweza kuwa ya jumla kwa mifumo wazi ya mifereji ya maji mikubwa yenye umuhimu kimataifa kama vile ziwa Victoria (linalopakana na Kenya, Tanzania na Uganda) na Ziwa Kariba (linalopakana na Zambia na Zimbabwe)

*Source: Ratner et al. 2018 as cited in Zhang et al. 2020*[37]

# Nyenzo za Rasilimali

## NYENZO YA 8: UTAMBUZI - SIFA MUHIMU ZA MAZUNGUMZO YENYE UFANISI YA WADAU MBALIMBALI NA KUFANYA MAAMUZI

Mazungumzo ya wadau mbalimbali na kufanya maamuzi hulenga uwezo na ushirikiano kati ya makundi na wenye haki ya umiliki/ wadau ambayo huja na mahitaji na changamoto zake, jukumu muhimu la mashirika ya uhifadhi mara nyingi ni lile la "mratibu" na "mwezeshaji". Kama mashirika ya uhifadhi yanajihusisha na kusaidia uongozi wa Wazawa na wenyeji katika kuratibu mazungumzo mapya kuwezesha MSD au kusaidia ushiriki wa MSD ya sasa, orodha ya vigezo muhimu vya MSD yenye ufanisi inaweza kutumika kuelewa muundo wa MSD na kama marekebisho yanaweza kuwa ya lazima.

## NYENZO YA 9: MWONGOZO - MAABARA YA UBUNIFU JAMII

Mwongozo huu wa washirika wa Reos, wenye kujulikana kama "maabara ya mabadiliko ya Reos" inayoshughulikia changamoto ngumu kwa kutumia ubunifu jamii, huleta mbinu ya kubuni na kuongoza mabadiliko ndani ya mifumo tata ya kijamii. Wakati mwongozo huu haueleezi namna ya uchunguzi wa kina wa Mbinu Shirikishi ya kuleta Mabadiliko kwa Jamii, vilevile ni muhtasari wa baadhi ya kanuni zinazohusiana na nyenzo na rasilimali. Mwongozo unafafanua mchakato wa kuanzisha, kuratibu na kuwezesha mchakato wa mabadiliko ya kijamii ambao ni wa kimfumo wa kiubunifu na wa kushirikisha- mwongozo unaoangalia " nani" "nini" na" kwanini" ya ubunifu jamii kama waratibu na wawezeshaji wa MSD, wahifadhi waliopata mafunzo ya Mbinu Shirikishi ya kuleta Mabadiliko kwa Jamii wanaweza hili ni la msaada katika kusaidia uongozi wa Wazawa na wenyeji na ushiriki kwenye MSD, na kujenga uelewa na uwezo miongoni mwa wadau mbalimali.

Nguzo ya 4

# Fursa Endelevu za Maisha




## Maarifa, Ushahidi, na Mazoea

**DONDOO MUHIMU**

- Ni muhimu kwamba ushirikiano katika kuleta fursa endelevu za maisha uhusishwe moja kwa moja na usimamizi endelevu wa maliasili ili uhifadhi unaoongozwa na jumuiya uwe wa kufaa na wa kudumu.
- Mipango ya mustakabali endelevu hulenga biashara na kipato cha familia, na aghalabu haishughulikii jumla ya gharama za uhifadhi kikamilifu, jambo linaloainisha umuhimu wa mipango kama hii kuunganishwa na fedha za uhifadhi.
- Zaidi ya kuwezesha malengo ya kimazingira na kijamii, fursa endelevu za maisha sharti iwe na mashiko kwa mtazamo wa kibiashara, ambao unahitaji kuangazia masuala ya kifedha, soko, uendeshaji, utawala, udhibiti na masuala mengine. Uelewa wa kina wa miktadha mahususi ni muhimu vikiwemo vikwazo vinavyoweza kuzuia upembuzi yakinifu.
- Uchaguzi mseto wa  kujipatia riziki husaidia kupunguza changamoto za kifedha zinazohusishwa na kutofaulu kwa uchaguzi wowote.
- Ingawa sio kanuni thabiti, fursa endelevu za maisha kulingana nashughuli zilizomo katika jamii - kwa mfano kutambua soko la samaki wanaovuliwa kwa mbinu endelevu au kudumisha shughuli za misitu - huwa na matokeo bora na huhitaji uwezeshaji mdogo ikilinganishwa na nafasi ambazo zinawahitaji watu kujifunza stadi mpya kabisa, kama vile kuanzisha miradi ya utalii wa kiikolojia.

**MANENO YA MSINGI**

**Fedha za Uhifadhi**—mbinu na mikakati ambayo inaweza kuzalisha, kusimamia na kutoa rasilimali fedha na kuweka vichocheo vya kufikia matokeo ya uhifadhi wa mazingira.[98] Fedha za uhifadhi zinalenga kusimamia gharama zote za uhifadhi na kuhakikisha uendelevu wa kifedha wa muda mrefu.[99]

**Malipo ya Huduma za Mifumo ya Kiikolojia (PES)**—malipo ya huduma za mifumo ya kiikolojia ni malipo kutokana na wanaonufaika au watumiaji wa huduma za mifumo ya kiikolojia yanayotolewa kwa waangalizi wa huduma hiyo. Huduma za mifumo ya kiikolojia zinaweza kujumuisha ukusanyaji na uhifadhi wa hewa ya ukaa, bayoanuai, ulinzi wa makutano ya maji, na mvuto wa maliasili. PES hujumuisha mifumo iliyoandaliwa vizuri, kama vile pongezi kwa ajili ya kupunguza hewa ya ukaa na uwekezaji kwenye makutano ya maji, pamoja na miradi ya kiuchunguizi zaidi, kama vile malipo kwa ajili ya bayoanuai.

**Fursa Endelevu za Maisha**—rInarejelea uwepo na uwezo wa kujihusisha katika fursa endelevu za maisha ambazo zinamruhusu mtu kusalia mahali pamoja. Riziki ina maana ya njia ya kuchuma kipato au kutimiza mahitaji ya maisha Riziki huwa endelevu wakati ipunguza madhara kwa maliasili iliyopo, kuwawezesha watu kukabiliana pamoja na kupata nafuu kutokana na misukosuko na shinikizo za kifedha, pamoja na kuwezesha ustawi wa kimazingira, kijamii, kitamaduni, na kiuchumi kwa njia yenye usawa sasa na kwa vizazi vijavyo.

## Aina za Fursa Endelevu za Maisha

Fursa endelevu inajumuisha njia za kujikimu kimaisha - kama vile kilimo au uvuvi wa kujikimu- pamoja na fursa na hamasa kwa watu kuongeza kipato kupitia usimamizi wa maliasili ambao ni endelevu kimazingira, na sahihi kimila. Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wazawa linaeleza kwamba Wazawa wana haki ya kujiaamulia - ikiwemo kujiamulia kiuchumi.[3] Watu wanapoweza kuhusisha mahitaji yao ya kiuchumi na maono ya baadaye na matamanio yao ya uendelevu, wanaweza mawakala wa mazingira vema zaidi. Mapitio pangilifu ya maandiko ya hivi karibuni yalibainisha kwamba shughuli za kukuza uchumi zilikuwa vipengele muhimu zaidi vinavyowezesha matokeo bora ya kimazingira na ya ustawi wa binadamu, kuongeza uwezekano wa mafanikio maradufu.[16] Wakati zinapoundwa kwa ushirikiano, na kuendelezwa kwa kuzingatia maono ya wenyeji, na kusanifiwa na kutekelezwa kwa mbinu endelevu za maisha zinazofikiriwa kwa makini zinatoa fursa nzuri za kuimarisha ustawi wa jamii na mazingira.

Kwa jumla, fursa endelevu za maisha zinaweza kuainishwa katika makundi matatu:

1. riziki za kujikimu
2. fidia ya moja kwa moja, na
3. shughuli za jamii.

Kwa kutegemea muktadha husika, huenda isifae kujihusisha na zaidi ya kundi moja, au yote matatu (Jedwali Na. 5).

**Jedwali Na. 5:** *Makundi na mifano ya fursa endelevu za maisha*

| Category | Kundi Mfano wa Fursa Endelevu za Maisha |
|---|---|
| Riziki za kujikimu | Kuunda bidhaa na huduma ambazo zinatumiwa na mzalishaji na familia au jamii yake, badala ya kutangaza na kuuza k.m., kilimo cha kujikimu, bidhaa za uvuvi, mimea ya kimatibabu, desturi za kitamaduni). Jumuiya huenda zikawa na hamu ya kuimarisha uendelevu na hali zinazosaidia riziki ya kujikimu. Kwa mfano, kugeukia kilimo endelevu zaidi au desturi za kuvuna au kutenga maeneo ya hifadhi yanayosimamiwa na jamii kama njia za kuimarisha usalama wa chakula |
| Fidia ya moja kwa moja ambapo wanajamii hupokea kipato kwa kushiriki katika utunzaji wa mazingira | Motisha wa kimazingira (k.m, kupunguza hewa ya ukaa, fedha za maji, na malipo mengine kwa ajili ya huduma za mifumo ya kiikolojia), ajira ya moja kwa moja kwenye uhifadhi (k.m., walinzi/walezi, ufuatiliaji wa mazingira), na mbinu za kugawana faida (k.m. fedha ya jamii kwa ajili ya mradi wa uhifadhi) |
| Shughuli za kijamii | Utengenezaji wa bidhaa au utoaji wa huduma ambazo zinaweza kuuzwa, aghalabu zikifungamanishwa na matumizi ya maliasili (k.m. kakao, viungo, mpira, samaki, mwani, mifugo, au utalii wa kiikolojia) |

Makundi haya matatu yanaendana na fursa wezeshi zinazosaidia kupatikana kwa fedha na mafunzo. Fursa wezeshi za kifedha zinaweza kujumuisha benki ndogo ndogo, vyama vya akiba na mikopo vijijini, na fursa nyingine zinazoruhusu upatikanaji wa ajira, maendeleo ya biashara na usalama wa kifedha. Fursa wezeshi za ujengaji uwezo zinaweza kujumuisha mafunzo ya ujasiriamali, msaada na utaalamu wa kibiashara, na uimarishaji wa shughuli za kijamii.

Fursa endelevu za maisha huleta mapato ya kukidhi mahitaji binafsi na ya familia, jambo ambalo huimarisha usalama na usitahimilivu wa kifedha wa watu, huchochea usimamizi endelevu wa rasilimali, na kupunguza mashinikizo ya maendeleo ambayo si endelevu. Hata hivyo, kimsingi huwa hazizalishi mapato ya kutosha kulipia gharama za moja kwa moja za uhifadhi.[99] Kwa mfano, shughuli za kijamii za ufugaji wa samaki zinaweza kutengenezea watu kipato kutokana na mauzo ya mwani, lakini mapato haya hayaweza kulipia matengenezo, usimamizi na urejeshaji wa miamba inayozunguka eneo husika.

## Mafanikio ya Fursa Endelevu za Maisha

> Angalia **"Nyenzo ya 10: Mwongozo wa Fursa Endelevu na Mashirika ya Kijamii"** kwa maelezo ya jinsi ya kuimarisha nafasi za riziki endelevu kwa ushirikiano na wazawa na jumuiya za wenyeji.

> Angalia Sura ya **"Nyenzo ya 11: Kuiandaa Jamii Ifanikiwe"** —inayoanza ukurasa wa 183—ya "Mwongozo kwa Mwezeshaji wa Ulinzi wa Ardhi ya Jamii ya Namati"100 kwa maelekezo na shughuli za kuiandaa jamii ijadiliane na wawekezaji na kuchukua hatua za kufikia maono ya pamoja ya jamii.

Katika maeneo mengi duniani, Wazawa na wenyeji hukabiliwa na shinikizo za kiuchumi kukiwa na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira na fursa chache za kuzalisha mapato. Katika hali hizi, watu wanaothamini maliasili huenda wakakumbana na uhalisia wa kuchagua kati ya uhifadhi wa rasilimali hizi au kujisaidia pamoja na familia zao. Isitoshe, katika baadhi ya hali, huenda wakawa hawana budi kuziacha jamii zao na kwenda kutafuta nafasi za ajira na/au elimu. Uhamaji kwenda nje unapozidi, unaweza kuwa na athari ya kuyumbisha mpangilio wa kijamii, kuharibu mahusiano na mahali pamoja na uwezo wa kuchukua hatua za pamoja, na kupunguza idadi ya watu wanaolinda rasilimali jambo ambalo linaweza kuleta nafasi ya unyonyaji kutoka nje a/au viwanda vya uchimbaji vilivyo na masilahi yanayokinzana.

Ukuzaji wa pamoja wa fursa endelevu za maisha utagemea vipengele kadhaa muhimu. Kwanza, nafasi za kutumia stadi na maarifa yaliyopo ya jumuiya huelekea kusaidia ukubalifu kuliko pale ambapo jamii inahitajika kujifunza stadi mpya kabisa. Hata nafasi zinazolenga stadi zilizopo tayari huhitaji viwango vya juu vya uimarishaji wa uwezo wa kibiashara na wa kifedha ili kufanikiwa, aghalabu katika kipindi cha miaka 8-10 au zaidi.[101] Fursa endelevu za maisha huhitaji pia upatikanaji endelevu wa kutegemewa wa mikopo nafuu, ambayo aghalabu haipatikani katika hatua za kwanza za maendeleo.[101] Jumuiya sharti ziweze kuuza bidhaa na huduma kwa ustadi na kufikia soko kwa bei nzuri. Zinatakiwa kuwa na mpango wa biashara unaohitaji usimamizi unaofaa, utendaji, ufadhili, na soko pamoja na sheria zinazodhibiti, miongoni mwa masuala mengine. Msaada wa moja kwa moja kwa biashara na uelewa wa kina wa muktadha mahususi ni muhimu.[101] Mafanikio ya fursa endelevu za maisha pia hutegemea vipengele vya ustawi wa binadamu zaidi ya ulimbikaji wa mali kama vile mahitaji na maazimio ya watu wanaohusika, maadili ya kitamaduni, na maono ambayo wako nayo kwa jamii katika siku zijazo.[102-103] Ni muhimu kwanza kuelewa jinsi watu binafsi na jumuiya huthamini maliasili na jinsi shinikizo za kiuchumi zinaweza kuathiri uwezo wao wa kutenda kulingana na tunu zao.

Pengine muhimu zaidi ni kwamba, fursa endelevu za maisha - kwenye aina zote zilizopo hapo juu - zinahitaji kuhusishwa kwa karibu na usimamizi endelevu wa maliasili zenyewe. Kampuni moja ya ufugaji wa samaki nchini kenya iliwaajiri wanajamii wa jamii ya wenyeji ambao ni wavuvi, ikawapa mafunzo kwa ajili ya nafasi za uongozi siku zijazo, na kuilipa jamii hiyo malipo yaliyo juu ya yale ya kawaida pamoja na kulipia kodi ya ardhi yao waliyotumia. Kuanzishwa kwa eneo la uzalishaji ambalo lilikuwa salama kulichangia kugunduliwa upya kwa aina za samaki ambao awali waliaminika kuwa wametoweka.[101] Katika mfano mwingine, kampuni inayomilikiwa na wakulima huko India iliwasaidia wakulima kupata masomo kwa bei iliyo juu kwa asilimia 20-asilimia 30, ilitekeleza mbinu endelevu za uvunaji na kutoa mafunzo kuhusu afya, haki za wazawa, na maarifa mengine.[101] Kwa upande mwingine, mifano ya nafasi za riziki endelevu haihusiani kwa karibu na usimamizi endelevu wa maliasili jambo lililosababisha vyanzo mbadala vya mapato huku unyonyaji (usio endelevu) wa rasilimali ukiendelea kwa viwango sawa.[102,104] Hili lilidhihirishwa katika tafiti mojawapo ambapo wavuvi walipewa boti mpya bila kuzingatia zaidi kanuni za uvuvi, jambo lililosababisha ongezeko la mavuno ya samaki mwambaoni.[105] Katika mfano mwingine, jamii zilizoshiriki katika mpango mbadala wa kuongeza fursa za maisha bila matumizi endelevu na thabiti ya ardhi, zilitumia mapato yaliyoongezeka kuongeza idadi ya mifugo, jambo ambalo lilichangia uharibifu wa mazingira ambao programu ililenga kulinda.[106]

Kila zingatio lililoko hapo juu linadokeza umuhimu wa nafasi endelevu za ajira zinazoongozwa na jamii, zinazoelekezwa na jamii na ambazo huchangia tofauti hizi ndogo na kujumuisha mseto wa chaguzi mbalimbali, na hivyo kuondoa hatari ya kuanguka kwa mradi wowote. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba kuna gharama za awali zinazohusiana na upanuzi ambao huenda ukaviletea hasara vikundi vilivyo na mapato ya chini ukilinganisha na ushiriki katika shughuli kama hizi. Mazungumzo na watu binafsi na vikundi katika ngazi mbalimbali yanaweza kujenga uelewa kuhusu mabadiliko ya fursa na hatari kutokana na mitazamo tofauti; mazungumzo bora huruhusu mbinu za usimamizi kurekebishwa ipasavyo.[102,107]






## Chunguzi Kifani



### Kaskazini mwa Australia—Fursa Endelevu Kupitia Shughuli za Hewa ya Ukaa na Ajira ya Moja kwa Moja katika Usimamizi wa Uhifadhi

Kihistoria, sehemu kubwa ya Kaskazini mwa Australia ilikuwepo kama mpangilio changamano wa nchi kavu na bahari iliyosimamiwa na mamia ya koo za Wenyeji. Hata hivyo, ukoloni uliziacha koo hizi bila ardhi katika karne za 19 na 20, ukikatisha uhusiano wake, maarifa, na desturi ambazo zilitawala ruwaza za uwakili wa mazingira zilizokuwa zimeanzishwa zaidi ya miaka 65,000 iliyopita. Bila usimamizi huu wa kitamaduni, savana za Kaskazini mwa Australia zimekuwa zikiathiriwa ma moto katika misimu ya kiangazi, ambao huchoma kwa kasi, kuharibu mazingira ya mimea na wanyama asili, na kutoa viwango vya juu vya gesi zinazochafua mazingira. Hivi karibuni zaidi, maeneo makubwa ya ardhi yamerejeshwa katika usimamizi ya wazawa. Hati ya Wazawa pamoja na haki nyingine za umiliki wa wazawa sasa zinasimamia zaidi ya asilimia 60 ya savana za kaskazini. Haki hizi za kimsingi zimetekeleza jukumu muhimu la kuwa msingi wa ushirikiano baina ya TNC na jumuiya za wazawa ili kupata ufadhili na msaada kwa mifumo ya mashirika na ya utawala ili kukidhi shughuli zinazojikita kwenye nchi kavu na bahari. Kwa kweli, huu ni mfano muhimu wa jinsi riziki endelevu na ufadhili wa uhifadhi unaweza kushirikiana kuleta matokeo bora kwa jamii na kwa mazingira ya asili.

Programu ya TNC Kaskazini mwa Australia inashirikiana na Wazawa wa Australia katika kusimamia ardhi yao kiutamaduni na kufufua na kuimarisha uhusiano wao na nchi. Wazawa hujihusisha katika upangaji shirikishi wa himaya zao unaojulikana kama Mipango Bora ya nchi (Umetumika na Wamiliki wa Jadi nchini Australia kutoka kwenye Mi Upangaji wa Hatua za Uhifadhi ili uafiki muktadha na vipaumbele vyema zaidi). Hali hii huwasaidia kupanga siku zijazo kwa ardhi yao kukiwa na nafasi za kiuchumi ambazo zinaoana na vipaumbele vyao kitamaduni. Kama sehemu muhimu ya usimamizi wa ardhi,Wazawa wa Australia wamefufua

**SEHEMU YA AIKONI**
Maeneo ya Mfumo wa VCA

**NCHI KAVU** **MAJI SAFI** **PWANI**

desturi za usimamizi wa moto, na kusaidia kurejesha na kudumisha ukwasi wa mimea na wanyama wa eneo hilo na kulinda maeneo muhimu kitamaduni na sifa za kimazingira. Kwa kupunguza moto unaoleta uharibifu mwishoni mwa msimu, desturi hizi kwenye ardhi ya wazawa zimesababisha kuepuka kuachiliwa kwa tani milioni 8 za gesi ya ukaa hii ikiwa ni sawa na zaidi ya ekari milioni 50 (hekta milioni 19.3), kukiwa na mpango wa kupanua mfumo huu kote Kaskazini mwa Australia ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa gesi ya ukaa.

Kupunguza gesi zinazochafua mazingira huzisaidia jamii kuzalisha na kuuza pongezi kwa kupunguza gesi ya ukaa kupitia soko la gesi ya ukaa la Ausralia, jambo ambalo huunda nafasi muhimu kwa jamii. Udhibiti wa jadi wa moto umezalisha zaidi ya dola milioni 100 za Australia katika ufadhili wa gesi ya ukaa, ambayo huwezesha vikundi kutumia uwekezaji wa ziada kutoka kwa serikali, uhisani na vyanzo vingine. **Kampuni ya Usimamizi wa Ardhi ya Warddeken**, inayomilikiwa na jamii, inatekeleza wajibu wa ufadhili na huduma nyingine zinazohusiana na usimamizi wa ardhi na ustawi wa jamii. Kampuni hii inajumuisha wajumbe wa bodi kutoka koo zote na kamati ya kudumu ya wajuzi inayowakilisha maarifa mbalimbali.

Kampuni hii inatumia ufadhili huu kusaidia mashirika mbalimbali ya kijamii na fursa endelevu za maisha, jambo ambalo ni muhimu kwa maisha marefu na kujitosheleza kifedha. Hatua zinajumuisha kujengeana uwezo, miundombinu, mipango ya jamii, makampuni ya biashara ya kupunguza hewa ya ukaa, na mpango wa walinzi wazawa. Programu za walinzi inatoa ajira na mafunzo kwa wanaume na wanawake wa eneo husika katika usimamizi wa ardhi na urejeshaji wa mazingira na kuunganisha maarifa ya asili na Sayansi ya Mataifa ya Magharibi kwa matokeo ya kudumu. Stadi hizi, uwezo wa usimamizi, na mipango ya utawala iliyoandaliwa kupitia programu ya walinzi na makampuni ya biashara ya kupunguza hewa ya ukaa pia hutoa msingi wa kukuza fursa endelevu za maisha. Kwa mfano, baadhi ya wenyeji wanajihusisha na shughuli za malipo kwa huduma, kama vile udhibiti wa magugu, udhibiti wa wanyama wa mwituni, usalama wa mazingira, na utafiti wa wanyamapori kwa majirani wanaomiliki ardhi, mashirika ya serikali na viwanda vya rasilimali. Wengine hukuza utalii wa kiikolojia, fursa za utalii wa kiutamaduni, na biashara za chakula cha mwituni. Hii hutoa msingi muhimu kwa nafasi za riziki endelevu katika siku zijazo ambazo zimejikita kwa usimamizi faafu kitamaduni wa rasilimali ya ardhi.

*Mifano zaidi ya Uchunguzi Kifani kuhusu Fursa Endelevu za maisha inapatikana* ***hapa****.*



© TED WOOD

# Nyenzo na Rasilimali

## NYENZO YA 10: MWONGOZO WA FURSA ENDELEVU NA MASHIRIKA YA KIJAMII

Mwongozo umeandaliwa kuwasaidia wahifadhi kufanikisha fursa endelevu kwa kushirikiana na Wazawa na wenyeji. Mwongozo huu unatoa maarifa ya msingi ambayo ni muhimu kuelewa fursa endelevu na kueleza hatua zinazoweza kuchukuliwa na nyenzo ambazo wahifadhi wanaweza kutumia wanaposhiriki kuandaa shughuli endelevu za jamii.

## NYENZO YA 11: MWONGOZO - KUIANDAA JAMII IFANIKIWE

Kazi katika sura hii za Mwongozo kwa Mwezeshaji wa Ulinzi wa Ardhi ya Jamii ya Namati[100]—"Kuandaa jamii Kufanikiwa" kuanzia ukurasa wa 183—zimesanifiwa kusaidia ukuaji na ustawi wa muda mrefu, kwa mujibu wa mipango na nia za kila jumuiya. Zinasaidia wanajamii kuona fursa mbalimbali, kuunda upya mifumo ya ndani ya kiikolojia, kujiandaa kwa mazungumzo yanayoweza kutokea na wawekezaji, na kuchukua hatua mahususi ili kutimiza maono yao ya pamoja kama jumuiya.



© AMI VITALE

## Kipengele cha Msingi cha 1

# Manufaa, Athari na Ushirikishwaji Sawa



© AMI VITALE

## Maarifa, Ushahidi, na Mazoea

**HOJA KUU**

- Kuunga mkono haki za binadamu na usawa ni sharti la kimaadili na ni hitaji muhimu kwa matokeo ya uhifadhi endelevu. Kwa Wazawa, hii inajumuisha haki ya kujiamulia na kiwango cha Idhini ya Awali na ya Kumaanisha.

- Usawa unapaswa kuchunguzwa katika kiwango cha jumuiya (k.m., jumuiya kwa jumuiya, kampuni, na serikali) na vile vile kiwango cha mtu binafsi (k.m., katika utambulisho wa kijamii). Kwa kuzingatia muktadha, tafakari kama baadhi wanafaidika zaidi kuliko wengine, wanaathiriwa zaidi kuliko wengine, na kujumuishwa zaidi kuliko wengine—na uchukue hatua ili kuepuka/kutenda ipasavyo.

- Uchanganuzi shirikishi wa hali kwa kuchunguza jinsia na uwezo ni muhimu kwa uelewa wa msingi wa maana ya usawa katika muktadha wowote, na mahusiano ya kiuwezo yanayosababisha na kuathiri ushirikiano na jumuiya. Shughuli zozote zinapaswa kutegemea uelewa mzuri wa muktadha na kukitwa katika kuunga mkono uongozi wa makundi maalum ya utambulisho wa kijamii, vipaumbele, na maono ya ushiriki wao na maisha yao ya baadaye.

- Haki zinaweza kutofautiana ndani ya jumuiya na katika rasilimali, na baadhi ya makundi ya kijamii (k.m. wanawake, vijana, wahamiaji wapya) huenda visipate haki sawa na wengine, hivyo haja ya mtazamo wa usawa. Ni muhimu kuzingatia kwa uangalifu ni akina nani wana haki ya umiliki ndani ya Jumuiya na jinsi ya kulinda haki hizo, kwa kuwa hili linamwathiri mwenye mamlaka juu ya maamuzi ya matumizi na usimamizi, na mwenye kupata manufaa.

- Katika michakato shirikishi kama vile warsha za uongozi na usimamizi wa kuinua uwezo na majadiliano ya wadau mbalimbali, ni muhimu hasa kuhakikisha ushiriki sawa na fursa za uongozi katika makundi ya utambulisho mbalimbali wa kijamii, kuzingatia mienendo ya uwezo katika ngazi ndogo na kubwa na kuinua uwezo kwa pande zote ili kushughulikia ukosefu wa usawa wa kiuwezo, na kuelewa na kupunguza athari zinazowezekana na ambazo hazikukusudiwa za kushiriki kwa wanajamii.

- Wakati wa kuunga mkono mustakabali wa maisha, mkazo ule ule unapaswa kuwekwa katika kuhakikisha usawa katika fursa na manufaa katika makundi mbalimbali ya kijamii na kuepuka matokeo yasiyotarajiwa—hasa wakubwa kujimilikisha mali au nguvu, kuongeza tofauti za utajiri zilizopo, na ongezeko la unyanyasaji wa kijinsia.

## MANENO YA MSINGI

**Wakubwa kujimilikisha mali au nguvu**—inamaanisha hali mbalimbali zinazohusiana, ila ni tofauti, ikiwemo kutawala na kudhibiti michakato ya kufanya maamuzi, kuhodhi misaada na rasilimali za umma, na mchanganyiko wa yote mawili. Dhana hii pia hutumiwa kuelezea hali ambapo wakubwa wa kisiasa na kiuchumi hujiingiza katika matumizi mabaya ya rasilimali na fedha za umma au kufanya vitendo vya ubadhirifu.[108]

**Usawa**—ni dhana pana inayojikita kwenye shauku za kimaadili na haki za kijamii kuhusu mgawanyo wa gharama na faida, mchakato na ushirikishwaji, na utambuzi unaozingatia muktadha sahihi. Wakati mwingine dhana hii hutumiwa kama kisawe cha kutopendelea au haki.[109]

**Haki za binadamu**—ni haki za watu wote, bila kujali uraia, mahali wanapoishi, jinsi, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kijinsia, asili ya utaifa au ukabila, rangi, dini, lugha, umri, uwezo, au hali nyingine yoyote. Sote tuna haki sawa kwa haki za binadamu bila ubaguzi.[110]

**Utambuzi wa jumla wa kijamii**—ni dhana iliyoundwa kwa mara ya kwanza mnamo 1989 na profesa Kimberlé Crenshaw, inayoeleza kwamba sifa zinazojengeka katika jamii hazitokei kwa kujitenga, bali zina muunganiko na huathiriana kwa wazi au kwa kujificha.[111]

**Utambulisho wa kijamii**—ni mambo ambayo yanafafanuliwa kwa kuzingatia ushiriki wake katika makundi (k.m. utambulisho wa kiasili, rangii, kabila, dini, mwelekeo wa mfumo wa imani, uraia, umri, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, lugha, kiwango cha elimu, hali au tabaka la kijamii na kiuchumi, eneo la kijiografia, uhamiaji au hali ya kibali cha uhamiaji).[112]

Angalia **"Nyenzo ya 12: Kufanya Uchambuzi juu ya Nguvu"**kwa nyenzo inayoelezea masuala ya fani mbalimbali juu ya nguvu, na kutoa mwongozo na violezo vya kufanyia uchambuzi juu ya uwezo

Angalia **"Nyenzo ya 13: Mwongozo wa Haki za Binadamu"** kwa mwongozo wa kina kuhusu utekelezaji wenye mwelekeo wa haki za binadamu.

Angalia **"Nyenzo ya 14: Miongozo ya Kijinsia"** kwa mwongozo wa kina kuhusu kuhusisha usawa wa kijinsia katika miradi na mikakati ya uhifadhi.

Katika uga wa uhifadhi, usawa wa kijamii unaweza kuelezwa kuwa na mielekeo minne-1) usambazaji wa gharama, majukumu, haki na faida, 2) utaratibu wa kufanya maamuzi na mwenye sauti, 3) utambuzi na heshima kwa hadhi sawa ya utambulisho tofauti, historia, tunu na faida, na 4) historia ya hali zilizopo za kijamii, kiuchumi, kimazingira na kisiasa.[109] Katika hali ya chini zaidi, mashirika ya uhifadhi yanapaswa kujitolea "kwanza, kutoleta madhara" katika jamii ambazo tunashirikiana na kuhakikisha kwamba wenyeji hawabebeshwi mzigo wa gharama ya uhifadhi ilhali jamii inanufaika.[113-114]TNC imedhamiria kutimiza mahitaji haya ya msingi ya kijamii ili kulinda mahitaji na kuvuka mipaka ya kusaidia na kuwezesha maono na uwezo wa kujiamlia mambo wa Wazawa na wenyeji.

Dhamira hii yenye njia mbili – si tu kutoleta madhara tu bali pia kuweka mwelekeo wa kuwa na ushirikiano wa kweli uliojikita kwenye usawa na uwezo wa kujiamlia mambo- inahitaji uelewa mzuri wa muktadha mahususi. Ili kufanya hivi, ni muhimu kutambua jamii kuwa ni

mchanganyiko wa makundi tofauti na utambulisho tofauti. Makundi au utambulisho tofauti wa kijamii (k.m. kwa kuzingatia jinsia, umri, hali ya kijamii na kiuchumi, kabila, rangi, dini n.k.) aghalabu hutumia maliasili kwa njia tofauti, kutegemea ufahamu wao na maarifa, ambayo yanahusishwa moja kwa moja na wajibu na majukumu yao yaliyobainishwa kijamii kwa njia tofauti. Kwa mfano, baadhi ya shughuli huenda zinabadilisha mfao wa wakati na kuongeza mzigo wa kazi kwa wanafamilia ambao ni waathirika wakubwa kama vile wanawake na watoto. Kama gharama hizi zinazowezekana na tofauti hazieleweki kikamilifu, mafanikio ya shughuli yoyote huenda yakawa madogo, yenye uwezekano wa kuleta madhara kwa baadhi ya wanajumuiya. Kwa upande mwingine, wakati masuala ya usawa yanazingatiwa na kujumuishwa katika usanifu wa utakelezaji na ufuatiliaji, hatimaye matokeo yatakuwa bora kwa watu na mazingira na kuongeza maamuzi na matendo ya jumuiya kwa muda mrefu. Hii inaungwa mkono na tafiti ambazo zilibainishwa kwamba kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika usimamizi wa misitu na uvuvi kulileta kuimarika kwa kanuni za matumizi ya rasilimali, utii wa sheria, na mifumo ya kiikolojia iliyolindwa vyema zaidi.[115-116]

Kuunda mahusiano yenye heshima na usawa na Wazawa na wenyeji huchukua muda. Ingawa uhusika wa TNC utaonekana tofauti katika hali mbalimbali, wajibu wa kuweka maono ya baadaye ya jumuiya ya Wazawa na Wazawa, na kuheshimu tofauti za utambulisho wa kijamii katika makundi haya ni jambo linalodumu. Katika shughuli zote, uchambuzi thabiti wa hali shirikishi unaojumuisha jinsia ndani ya jamii na uchanganuzi wa uwezo ni muhimu ili kuelewa njia kubalifu kiutamaduni za kusaidia mamlaka na uwezo wa jumuiya. Kwa mfano, kutathmini mgawanyo wa faida—zinazoonekana (k.m., mapato, teknolojia) na zisizoonekana (k.m., elimu, hadhi, ushiriki, ushirikishwaji, usalama, nguvu)—kutoka kwa mikakati ya uhifadhi ni muhimu, kwani baadhi ya makundi yanaweza kufaidika zaidi kuliko vingine. Uchanganuzi huu unaweza kuelekeza jinsi ya kutoa msaada kwa njia ambazo zitaepuka kuzorota na uwezekano wa ubaguzi au ukatili kwa misingi ya utambulisho. Uchanganuzi sharti utambue na uangazie tofauti za kiuezo, ikiwemo uhalisia tofauti kwa makundi tofauti ya kijamii, na uvuke mipaka ya kuangazia utambulisho wowote wa kijamii kuwa kikundi sawa, badala yake, ni muhimu kutambua kwamba utambulisho kamili wa mtu umeundwa na makutano mengi katika utambulisho mbalimbali wa kijamii.[117] Kuwezesha ushiriki wa jamii unaolengwa na mzuri kwa utambulisho wa kijamii katika uchanganuzi wa hali ni muhimu ili kuhakikisha kuwa shughuli zinazofuata zinaendelezwa kwa ushirikiano na kukubalika kiutamaduni, na kwamba hazisababishi matokeo hasi yasiyotarajiwa, kama vile chuki, ukatili unaotokana na utambulisho, au kulazimisha mawazo ya nje—pamoja na mawazo kuhusu usawa ni nini—ambayo yanaweza kuendeleza mifumo au athari za kikoloni (mawasiliano ibinafsi, Janine Mohamed, Taasisi ya Lowitja).

## Usawa katika Haki na Umiliki

Haki za msingi za kujiamlia mambo za Wazawa zipo kwenye haki zilizolindwa juu ya ardhi, maji na rasilimali. Hii inathibitishwa katika **Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wazawa**. Kwa mfano, Ibara ya 25 inasisitiza haki ya Wazawa kudumisha na kuimarisha uhusiano wa kiroho na ardhi, maji na maeneo yao; Ibara ya 29 inaeleza haki ya Wazawa ya uhifadhi, ulinzi, na uwezo wa uzalishaji wa ardhi yao au himaya na rasilimali; na kifungu cha 32 kinaeleza haki ya Wazawa kuamua vipaumbele kuhusu ardhi, himaya, na matumizi na ukuzaji wa rasilimali.

Mtazamo wa usawa wa kupata haki za Wazawa na wenyeji za ardhi, maji na rasilimali unaweza kujumuisha kuunga mkono utekelezaji wa sera au mabadiliko yanayochangia haki nzuri zaidi na hali ya usawa. Mwelekeo huu pia huenda ukahusisha kuunga mkono usawa katika umiliki, matumizi na haki za urithi kwa makundi tofauti ya jamii katika jumuiya. Kihistoria, juhudi za kuongeza haki ya umiliki mara nyingi zimejikita zaidi kwanye rasilimali zinazotumiwa na wanaume, licha ya kwamba kuna matumizi tofauti na maarifa yanayomilikiwa na wanawake.

Isiotshe, Katika baadhi ya mikatdha wanawake huenda wasiweze kumiliki ardhi, na ikiwa wanaweza kumiliki ardhi pamoja na waume wao, ardhi mara nyingi humilikiwa na ndugu wa mwanaume kama atafariki. Picha hii ya ukosefu wa usawa kimuundo unapingana na ustawi na usalama wa wanawake, pamoja na jumuiya zao na mifumo ya kiikolojia wanayolinda. Wanawake wanapopewa zaidi uhakika wa haki, huwa wanaimarisha ustahimilivu wao, vipato vyao, chakula kwa familia zao, na ubora wa ardhi, maji na maliasili wanazosimamia.[118-119]

Eneo la kijiografia pia linaweza kuathiri mahusiano ya kiuwezo na mifumo ya haki. Kwa mfano, katika muktadha wa maji safi, kuwepo kwenye chanzo hutoa manufaa fulani kuliko kuwepo sehemu yanapotiririkia maji, na ukosefu wa usawa katika uwezo ama hukabili au kuunga mkono mabadiliko haya. Ingawa hivyo, juhudi za kulinda umiliki pia zinaweza kuongeza hatari ya mgogoro au kutoridhika, kwa kuwa kutoa na kubainisha haki kunaweza kuwa na matokeo ambayo hayaleti manufaa. Wakati mtu anawepa haki za mali, mtu mwingine au asasi inaweza kupoteza haki hizo (k.m, kuhama kutoka ufikiaji wazi wa wavuvi wadogo hadi mbinu za usimamizi zinazozingatia haki).

## Usawa katika Uongozi, Utawala, na Uwezo wa Usimamizi

Uwezo wa kujiamulia kwa Wazawa unapaswa kuwa kiini cha juhudi za kusaidia uongozi, utawala, na uwezo wa usimamizi wa Wazawa na wenyeji.[120] Hii inajumuisha kuheshimu na kufanya kazi na viongozi wa jumuiya na taasisi, mifumo ya kiutamaduni na ya kisasa ya utawala, na michakato ya kufanya maamuzi, pamoja na kuheshimu na kutumia ujuzi wa asili pamoja na kwa ngazi sawa na Sayansi ya nchi za Magharibi,[121] na kuchukua hatua za kulinda haki miliki ya Wazawa na wenyeji. Hakuna shughuli zinapaswa kufanyika bila Idhini huru na ya Awali ya Wazawa, ambayo ni mchakato unaoendelea ambao unapaswa kufanywa katika kipindi chote cha maisha ya mpango.[122] Kujenga uwezo huenda kwa njia zote mbili—uwezo wa wafanyakazi na washirika pia unahitaji kujengwa. kwa ajili ya kuendeleza mkabala wenye usawa na unaozingatia haki za binadamu kwa kazi hii. Wahifadhi wanapaswa kuwa wazi na wawe tayari kupata taarifa mpya, ujuzi na maarifa kadri wanavyohusika, kushirikiana, na kufanya kazi na Wazawa na Wazawa.

Wakati mikakati ya kuimarisha uwezo inasanifiwa na kutekelezwa, makini inafaa kutiliwa katika ujumuishwaji, usawa wa athari na manufaa, na uwazekano wa wakubwa kujimilikisha mali au nguvu kama sehemu muhimu ya mafanikio. Juhudi zinazofanikiwa za uimarishaji wa uwezo sharti zipiganie ufikiaji wenye usawa. (Kwa taarifa, nyenzo, na fursa), ushiriki wenye usawa (katika mafunzo, mikutano, na michakato ya kufanya maamuzi), na uongozi wenye usawa (katika upangaji, utekelezaji na tathmini). Wamiliki wa haki na wadau mbalimbali wana tajriba tofauti, mapendeleo na usuli, na hatua zinapaswa kuchukuliwa kuhakikisha wanajumuishwa. Kwa mfano, wanawake aghalabu huongoza maliasili tofauti kuliko wanaume, jambo ambalo ni muhimu katika upangaji unaohusu utawala wa maliasili na usimamizi.

Tunapendekeza mbinu inayozingatia usawa wa kijinsia. Ushahidi mwingi unathibitisha kwamba watu na mazingira hunufaika wakati wanawake wanapata haki zaidi, sauti na uchaguzi katika usimamizi wa maliasili.115-116Kwa kujumuisha sauti zote, tunaweza kusaidia vyema zaidi ulinzi wa jumla ya rasilimali ambazo watu wanategemea na kujali. Hii inahusisha kuwajumuisha wanaume na wavulana katika uchanganuzi wa jinsia na shughuli zinazolenga jinsia, ili kwa pamoja na wanawake na wasichana, mfanano na tofauti ziweze kubainishwa, na suluhu kupendekezwa kusaidia uelewa, uwajibikaji, usawa na uendelevu.

Mifano ya hatua ambazo zinaweza kukuza usawa kwenye juhudi za kusaidia uongozi thabiti katika jamii, uwezo na utawala imeorodheshwa katika jedwali la 6. Tafadhali zingatia kuwa huenda kuna mwingiliano baina ya utambulisho mbalimbali ulioorodheshwa.

**Jedwali Na. 6:** *Mifano ya hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa kukuza Usawa katika Uongozi, Utawala, na Uwezo wa Usimamizi kwa utambulisho mbalimbali wa kijamii.*

| Mfano wa Utambulisho wa Kijamii | Mfano wa Hatua za Kujenga Usawa |
|---|---|
| Jinsia | Mafunzo na msaada wa kifedha kwa mitandao na vikundi vya wanawake; kufanya mafunzo ya ziada, yaliyowezeshwa na wanawake kwa wanajamii wanawake; kutoa malezi ya watoto kwenye mikutano au kutoa malazi au posho kwa wanawake kuleta watoto wao na/au watoa huduma; kupanga mafunzo na mikutano ya nyakati na maeneo ambayo ni salama na yanayoweza kufikiwa na wanawake na hayaongezi mzigo wao wa muda, kukabiliwa na hatari, na mzigo wa kazi; kuwezesha kubadilishana kwa nafasi za kujifunza miongoni mwa wanawake kutoka jamii mbalimbali; kusaidia uwezo na imani ya wanawake katika maeneo kama vile kuzungumza hadharani, majadiliano, usimamizi wa fedha, na uongozi wa mradi |
| Umri | Mafunzo na msaada wa kifedha kwa mitandao na vikundi vya vijana; kukuza ushiriki wa vijana katika kufanya maamuzi na majukumu ya uongozi; kuendeleza fursa za riziki endelevu kwa vijana; kusaidia ushiriki wa Wazee; kusaidia miunganisho ya vizazi; kusaidia mabadiliko bora ya uongozi, ushauri, na mipango ya kurithishana |
| Kabila | Kuendesha warsha katika lugha ya kasili na/au kutoa huduma za tafsiri na utangazaji mapema; kuhakikisha nyenzo za mafunzo zinapatikana katika miundo na lugha zinazoweza kufikiwa; kutengeneza mbinu na taratibu za kujifunza na kubadilishana maarifa ya asili na ya kikabila yanayojitokeza na kufichuliwa; kutoa mpatanishi asiyeegemea upande wowote inapobidi |
| Hali ya kijamii na kiuchumi | Kuwafidia wanajamii kwa ushiriki wao; kuhakikisha mikutano na mafunzo hayafanyiki nyakati za mchana wakati kazi ya kutafuta riziki inahitajika au wakati wa msimu wa mavuno; kusaidia na kutafuta wauzaji wa ndani na watoa huduma kwa mikutano au shughuli inayofanyika mahali; kuepuka mahusiano yenye upendeleo na walio na mali zaidi au walio na elimu ya juu zaidi katika jamii. |

h. Hi i ni muhimu ili kuepuka matokeo yasiyotarajiwa ya watoto kukosa shule ili wasaidie katika kazi za nyumbani.

i. Zingatia viwango vya elimu, pamoja na uwezekano kwamba wanawake au makundi ya wachache huenda wakatumia lugha ua kiasili ambayo si lugha ya taifa.

## Usawa katika Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali

Masuala mengi ya usawa yanayozingatiwa yanayohusiana na usanifu wa mazungumzo ya wadau mbalimbali na mchakato wa kufanya maamuzi yanaingiliana na yale ambayo ni muhimu katika nguzo ya uongozi, utawala na uwezo wa usimamizi ya Mfumo wa VCA. Muktadha wa kihistoria na wa sasa wa ukoloni na ukosefu wa usawa katika mahusiano ya uwezo unahitaji uimarishaji wa uwezo wa wamiliki wa haki na wadau wanaohusika. Vinginevyo, kuna hatari ya mifumo ile ile ya uwezo katika ngazi ya juu kujidhihirisha ndani ya muktadha wa mpango. Hii inaweza kuhusisha uimarishaji wa uwezo wa serikali au wa kibinafsi katika mahusiano ya haki za asili, pamoja na msaada kwa uwezo wa jamii za Wazawa na Wazawa katika sera au mazingira ya ushirika. Ni muhimu kukumbuka kwamba wakati mashirika ya uhifadhi yanaweza kuwa wapangaji wa kuaminika katika mazingira haya, kuna yale yaliyo na mapendeleo, na baadhi ya kanuni zinazohusika kwa uimarishaji wetu wa uwezo katika nguzo ya uongozi pia zinahusika kwa uimarishaji wetu wa uwezo kwa mahusiano kwa kuaminiana kama washiriki ndani ya mazingira yenye wadau wengi.

Mifumo ya nguvu ni kipengele muhimu cha kuzingatiwa katika usanifu na mafanikio ya mazungumzo ya wadau mbalimbali ndani ya jamii zenyewe na kwa uhusiano na makundi mengine ya wadau. Katika hali nyingi, ukosefu wa haki rasmi, ukosefu wa uwezo, na ukosefu wa vibadala vya kiuchumi unaweza kuzitia jumuiya asili katika nafasi yenye upungufu katika ngazi ya uwezo na athari katika kufanya maamuzi. Tukiangazia uharibifu wa mazingira, wale wanaonufaika kutokana na shughuli za kuharibu mazingira aghalabu wana uwezo zaidi katika muktadha wa sasa wa kimfumo kuliko wale wanaodhurika na uharibifu huo, hivyo kuwafanya washiriki wenye uwezo mdogo kugharamika.123 Si rahisi kushughulikia tofauti katika ufikiaji, athari, rasilimali, na taarifa, na wale walio na uwezo huenda wakachelea kuachilia udhibiti, mara nyingi kwa kutumia nguvu kuamua aina (k.m. wakati, saa, eneo) na shughuli (k.m. mchakato) ya mazungumzo. Kutojali mahitaji ya Wazawa na wenyeji kunaweza kupunguza nafasi yao ya kuhusika kwa njia inayofaa.91 Katika hali hii, wenyeji zinaweza kupata ushiriki wa “ishara” usiokuwa na maana ambao hauleti mabadiliko yoyote katika mamlaka ya kufanya maamuzi. Vile vile ni muhimu kutambua ongezeko la serikali zisizopendelea lugha za asili na washiriki wengine wanaokuza vurugu dhidi ya watetezi wa mazingira na kupunguza usalama wa ardhi, maji na rasilimali. Baadhi ya washiriki hawatakuwa salama kutokana na lugha asili na uhusisho wa wenyeji na ni muhimu kuelewa kutokana na washiriki wenyewe nini wangependa kusaidia na nini wangependa kuepuka. Katika hali zote ambapo watendaji wanahusishwa, ni muhimu kushirikiana katika kuunda mpango wa kusuluhisha mgogoro ambao unakidhi mahitaji ya kitamaduni na unalenga majadiliano.[124]

Mazungumzo ya wadau mbalimbali yanapaswa kusaidia ufikiaji, ushirikishwaji, na uongozi wa wadau wote (ikiwemo makundi ya utambulisho wa kijamii ambayo yamo hatarini na ambayo hayawakilishwi inavyotakiwa) katika majadiliano na maamuzi yote.[125] Jamii zenyewe zina tofauti za ndani ambazo sharti zitambuliwe ili kuhakikisha uwakilishi na ushirikishwaji wa kutosha-kwa mfano, wanawake, wazee, na makundi mengine ambayo yana mielekeo na ufahamu wa kipekee kuongezea kwenye mjadala. Kuhusu usawa wa kijinsia haswa, kusaidia uhusiano na kubadilishana katika mitandao ya wanawake na mashirika kunaweza kutoa fursa muhimu ya kujifunza, kushiriki, na kuendeleza vipaumbele vya wanawake.

Tafadhali rejelea Jedwali la 6 kwa mifano ya hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa kukuza usawa katika mazingira ya Mazungumzo ya Wadau Mbalimbali (MSD). Kwa jumla, makini inafaa kutiliwa gharama zisizodhahiri/zisizokusudiwa za kushiriki katika mazungumzo ya wadau mbalimbali (k.m. kipato kilichopotea, mabadiliko katika mzigo wa saa), kukubali lugha za kiasili (k.m. kufanya shughuli katika lugha ya kiasili au kutoa tafsiri ya moja kwa moja), muda wa siku na mwaka ambao mazungumzo ya wadau mbalimbali hufanyika (k.m., isiwe wakati wa mavuno au msimu wa uvuvi), muundo wa mazungumzo (k.m. unaowiana na mbinu za jadi za majadiliano na kufanya maamuzi ), na kwamba watu wanaofaa wanajumuishwa (kwa mfano, sio tu wasomi matajiri na kuheshimu viongozi waliochaguliwa / wa jadi).

## Usawa katika Fursa Endelevu za Maisha

Nguzo hii, labda zaidi ya nyingine yoyote, ina uwezo wa kuzidisha tofauti zilizopo za usawa, na kwa hiyo uangalifu mkubwa unapaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha mtazamo unaokubalika kiutamaduni na wenye usawa wa ushiriki na faida. Kwa upande mwingine, fursa endelevu za maisha zina uwezo wa kufanya mifumo kuwa ya usawa zaidi, lakini hii ni ikiwa mipango hii itaunganishwa na au kuchangia katika mabadiliko ya miundo ya sasa, ambayo inategemea ukosefu wa usawa wa uwezo. Ili kufanya fursa za riziki endelevu kuwa na usawa, lazima tuendelee kuunga mkono ushiriki na uongozi wa makundi ya utambulisho mbalimbali wa kijamii katika kufafanua "nini" na "jinsi gani," na kusaidia ugawaji wa faida wenye usawa ndani ya familia na katika makundi mbaliambali ya utambulisho wa kijamii. Ugawaji wa manufaa wenye usawa pia ni muhimu katika kuzuia kuzidi kwa ukosefu wa usawa uliopo tayari au kuibua aina mpya ya ukosefu wa usawa ndani ya jamii, pamoja na kuunda manufaa muhimu. Kwa mfano, wanawake na watoto huenda wasipate manufaa mabayo yanadhibitiwa na mwanaume anayeongoza familia. Isitoshe, ikiwa wachache katika jam ii-aghalabu walio tajiri zaidi-wanashiriki katika fursa ya kujikimu kimaisha, mapato hayawezi kuifikia jamii nzima.126 Hatimaye, ni muhimu kutambua hatari na kulinda dhidi ya matokeo hasi ambayo hayakutarajiwa, kama vile chuki, unyanyasaji wa kijinsia au ubaguzi (kwa mfano, unaotokana na wivu, woga, au hasira kwa kukatizwa kwa mienendo ya uwezo au usambazaji wa mali), kuongezeka kwa mzigo wa saa na mzigo wa kazi, au kuzidishwa kwa pengo lililopo au tofauti zilizopo za mali .[127-129]

Mifano ya mipango ya usawa wa kijinsia inayolenga riziki endelevu ni pamoja na kusaidia wanawake kufikia teknolojia, mali, akiba, na mikopo; kusaidia wanawake katika uzalishaji na uuzaji endelevu wa bidhaa zinazotokana na rasilimali ambazo wanawake wamekuwa wakisimamia tangu jadi; kuongeza utambuzi na fidia kwa majukumu ambayo wanawake wameyafanya kijadi; au kusaidia wanawake katika shughuli mpya wanazochagua. Kimsingi, usawa wa kijinsia huboresha maisha, ikiwemo matokeo ya afya,[130] maendeleo ya kiuchumi,[131] sera za kijamii, uendelevu wa mazingira, na fursa kwa vizazi vijavyo.

Mipango ya fursa endelevu pia inaweza kuwa fursa muhimu sana kwa uongozi wa vijana na fidia, kuwawezesha kukaa katika jumuiya zao, kupokea ujuzi unaopitishwa kutoka kwa Wazee wao, na kuchukua majukumu katika ardhi, maji, na usimamizi wa rasilimali. Kulingana na uelewa wa muktadha, kulenga mipango fulani ya ushiriki wa vijana (ikiwa ni pamoja na wasichana na wanaume vijana) na ushirikiano kati ya vizazi unaweza kuwa muhimu kwa mabadiliko chanya ya kudumu na kwa endelevu siku zijazo.





© ERIK LOPES



© ERIK LOPES

# Chunguzi Kifani



## Uongozi wa Wanawake katika Jamii yenye Asili ya Xikrin ya Brazil

Jamii ya Wazawa ya Xikrin wa Bacajá, ambao ni takriban watu 1,300, wanaishi katika vijiji 20 kwenye Ardhi ya Wazawa ya Trincheira Bacajá, eneo linalochukua ekari milioni 4 (hekta milioni 1.65) katika jimbo la Pará la Brazil katikati mwa Msitu wa Amazon. Msitu wa Amazon ni muhimu katika kunyonya kaboni na ni kimbilio la wanyama wengi tofauti na bila shaka ni mojawapo ya mifumo ikolojia muhimu zaidi duniani—na ardhi za Wazawa ni muhimu kwa ulinzi wake, ikijumuisha zaidi ya asilimia 27 ya eneo la ardhi katika Bonde la Amazon na kushikilia asilimia 33 ya hifadhi zake za kaboni. TNC imeshirikiana na jamii ya Xikrin katika uhifadhi wa msitu na fursa za kujichumia riziki kwa miaka kadhaa, na hivi karibuni ushirikiano huu umejumuisha kimakusudi kipengele cha kuzingatia jinsia.

Kwa kutambua kuwa majukumu yaomara nyingihuonekana ndani na nje ya kijiji kuwa majukumu yasiyo ya msingi, wanawake wa Xikrin (wanaojulikana kama Menire) walijizatiti kupata utambuzi zaidi wa majukumu yao kama wasiamamizi wa maliasili, pamoja na nafasi nyingine zinazoelekeza kwa aina tofauti za miradi katika jamii zao. Lengo lao lilikuwa kujipanga na kuhusisha washiriki wanaowasaidia, kukuza ufahamu na stadi zao na kuongeza udhihirikaji wao ndani ya jamiii zao na katika ulimwengu wa Kuben (wazungu). Kwa kuwa majukumu yao mengi na ilhamu zao zinajikita kwa usimamizi endelevu wa maliasili, kusaidia maono na uongozi wa Menire ni suluhu la kiasili na la kudumu katika kuimarisha ustawi wa mazingira na wa binadamu.

Wanawake wa Xikrin walianza safari hii kwa udhihirikaji wa nje mnamo 2013, wakiwa na miradi mbalimbali ya usimamizi endelevu wa rasilimali na uzalishaji kwa ushirikiano na Mfuko wa Taifa wa Wazawa wa Brazil (FUNAI), Shirika la Uhifadhi wa Mazingira, Mpango wa Maendeleo Endelevu wKikanda wa Xingu ( PDRS Xingu), na jumuiya za kitamaduni za ribeirinho huko Rio Novo. Majukwaa haya ya ushiriki ya wadau wengi yamekuwa muhimu katika kuendesha na kudumisha ushirikiano wa kufanya kazi ili kuunga mkono sauti, uchaguzi na hatua za Wazawa katika eneo lote.

**PICHA YA AIKONI**
MAENEO YA MFUMO WA VCA

**NCHI KAVU** **MAJI SAFI** **PWANI**




Miradi hii inayoongozwa na wanawake- ikiwemo ushonaji wa nguo, utengenezaji wa unga, upandaji wa mboga, na uundaji wa rangi ya kupaka mwilini (na hivi karibuni ya kupaka vitu kama vile mifuko na shati)-yote ina lengo la kusaidia usimamizi endelevu, mavuno, na uzalishaji wa bidhaa za msitu zisizo za mbao, jambo linalokuza na kudumisha msitu wenye afya na unaoishi. Baadhi ya miradi hii inaendelea leo na inakuwa mifano kwa vijiji vingine, kuhimiza ushiriki wa familia zilizo na ilhamu zaidi.

Mradi mmoja ambao umepanuka na kwa sasa unajumuisha ushiriki wa vijiji kadhaa vya Xikrin ni mradi wa babaçu wa uzalishaji wa mafuta, kutokana na mbegu za mitende. Mradi huu unalenga kuimarisha uwezo wa Menire katika kuongoza usimamizi, uzalishaji, na biashara kutokana na mafuta ya babaçukwa matumizi ya nyumbani kwenye vijiji na kwa biashara ya nje. Mafuta haya huuzwa kwa bei nafuu na huelekezwa moja kwa moja kwa watumiaji au hifadhi katika miji, na kuondoa wanunuzi wa katikati na kuongeza thamani kubwa ya kiuchumi kwa shughuli yenye umuhimu wa kitamaduni na wa kiuchumi.

Mradi huu pia ulijumuisha kuanzishwa kwa nhô rõny kangõ nhõ kikre mpya (babaçu kiwanda cha kutengeneza mafuta) mashine ndogo ya kutoa mafuta, na chupa na vibandiko vya kufunga mafuta. Kutengeneza mafuta ya babaçu ya kupikia, ya kujipaka, na ya kutumika katika miviga ni jukumu la kitamaduni na lenye urithi muhimu wa kitamaduni kwa Menire tangu vizazi vya zamani, sasa linatoa nafasi ya uongozi zaidi, kuchuma kipato, na kutambuliwa kwa wanawake wa Xikrin na vijiji vyao. Mradi huu pia ulitambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo kwa kuwawezesha wanawake na kujisimamia kwa shughuli za mashambani ambazo zinakuza vyakula vyenye afya na vya kitamaduni.

Wanawake wazawa ni viongozi wa ahadi kwa vizazi vijavyo. Akina mama, wamama vikongwe,—wanawake wote katika jamii—wana uelewa wa pamoja muhimu na wajibu wa rasilimali za misitu, ambazo ni muhimu kwa usalama wa chakula kwa familia nzima, na kwa usimamizi endelevu wa rasilimali za jamii. Katika Mpango wa Usimamizi wa Eneo na Mazingira wa Watu wa Xikrin (PGTA—ulioandaliwa kwa ushirikiano na TNC), Menire walisisitiza umuhimu wa kuimarisha maarifa yao ya asili na usimamizi wa kibiashara wa mazao ya misitu yasiyo ya mbao, kama vile piy (mti aina ya Mbrazili). Familia nzima hushiriki katika utengenezaji wa piy, ikiwemo kukusanya, kuosha, kukausha, kusafirisha na kuhifadhi.




TNC pia husaidia jamii nyinginezo za Wazawa katika kusimamia na kufanyia biashara rasilimali kama vile mbegu za mti aina ya mbrazili, ikiwemo jamii ya Wazawa wa Parakanã katika Ardhi ya Wazawa ya Apiterewa karibu na Xikrin. Kama ilivyo kwa mradi wa mafuta ya babaçu, jamii za Xikrin na Parakanã zimeanzisha mashirika ambayo yanasimamia na kuuza mbegu za mti aina ya mbrazili moja kwa moja kwenye viwanda, kwa mfano kwa kiwanda cha mikate, na kuwaondoa wanunuzi wa katikati na kwa hivyo kupokea bei za juu zaidi. Jamii ya Parakanã pia inakuza msururu wa thamani ambao ni thabiti kwa vinyago vyao vya kitamaduni, ambavyo wanauza ughaibuni kwa thamani ya juu na kwa uhitaji thabiti. Hii inatoa mtiririko wa mapato unaoendelea moja kwa moja kwa wanawake, ambao wanautumia kuboresha maisha ya familia na vijiji vyao na hatimaye kuimarisha uhuru wa Parakanã kwenye ardhi yao.

Hali ambayo imechangia mafanikio katika maeneo haya ni uwepo wa haki za ardhi zilizobainishwa. Ingawa hazina usalama kamili dhidi ya uvamizi na uingiaji na uchimbaji haramu wa wahusika wa nje, ukweli kwamba maeneo ya Xikrin na Parakanã yamewekewa mipaka hufanya kuwe na mahali thabiti pa kuanzia katika juhudi hizi. Zaidi ya hayo, usaidizi wa ushirikiano wa muda mrefu na majukwaa thabiti ya wadau mbalimbali umekuwa sehemu muhimu ya kazi hii. Kwa mfano, Wazawa kutoka nchi mbalimbali wanakusanyika pamoja kwa ushirikiano kuhusu mipango ya riziki endelevu, ili kufikia kiwango kikubwa na athari, na kuunganishwa na mifumo kama **selo Origens Brasil®** kwa uidhinishaji endelevu. Njia mojawapo TNC Brazil huunga mkono kuendelea kwa ushirikishwaji wa wadau wengi ni kwa kudumisha makubaliano ya ushirika na FUNAI, kuhakikisha malengo na vitendo vya FUNAI na TNC vinashirikiana, vinakamilishana, na vinawiana na malengo ya pamoja katika kuunga mkono uongozi wa Wazawa na uwezo wa kujiamulia mambo mbalimbali kote katika mikoa ya makabila mbalimbali.

Kuongezeka kwa udhihirikaji wa uongozi wa wanawake Wazawa katika vyama na taasisi za Wazawa katika viwango vyote kote Brazil kunasababisha matokeo makubwa: Leo, Uratibu wa Mashirika ya Wazawa ya Amazon ya Brazil (COIAB) na Vuguvugu la Wadai Haki Wazawa Brazil (APIB), kwa mfano, yanawakilishwa na viongozi shupavu wa kike wanaoendeleza haki za Wazawa na uendelevu wa mazingira katika mizania ya kitaifa na kikanda.

Miunganisho kati ya shughuli za uhifadhi, usawa wa kijinsia, na haki za Wazawa inapoeleweka, kukubaliwa, na kuungwa mkono, shughuli za uhifadhi zina uwezekano wa juu zaidi wa kutoa athari chanya za kijamii na kuchangia matokeo ya kudumu zaidi ya uhifadhi. Na muhimu kwa mafanikio haya ni kuzingatia maono na uongozi wa wanawake wa kiasili wenyewe, na kuthamini mchakato wao wa ushirikishaji wa wanaume, vijana, na wanajamii wengine, huku TNC na washirika wengine wakitekeleza jukumu la kuunga mkono. Kusaidia wanawake wa kiasili kustawi kwa njia wanazoamua zinafaa kitamaduni na kupatana na maono yao ya siku zijazo ni muhimu katika kuhakikisha uhifadhi wa mamilioni ya hekta za ardhi muhimu kiikolojia katika Amerika ya Kusini na duniani kote.

# Nyenzo na Rasilimali

## NYENZO YA 12: KUFANYA UCHAMBUZI JUU YA NGUVU

Nguvu inaweza kufafanuliwa kuwa ni kiwango cha udhibiti wa rasilimali nyenzo, watu,akili na fedha kinachotekelezwa na sehemu tofauti za jamii. Kiwango cha uwezo wa mtu binafsi au kikundi kinahusiana na aina mbalimbali za rasilimali ambazo wanaweza kupata na kudhibiti. Nyenzo hii inaeleza vipengele mbalimbali vya nguvu, na inatoa mwongozo na violezo vya kufanya uchanganuzi wa nguvu. Uchanganuzi juu ya nguvu unapaswa kutekelezwa wakati wa uchanganuzi wa hali ambao ni sehemu ya mchakato wa upangaji wa uhifadhi kwa ushirikiano na Wazawa na wenyeji. Kwa hiyo, wahifadhi huenda wakapata manufaa kwa kuunganisha vipengele anuwai vya uchanganuzi wa hali ambavyo vinginevyo vingetekelezwa kipekee katika uchanganuzi mmoja mkubwa, ambao unaweza kusaidia kubana muda, rasilimali na mtaji wa kijamii. Hii inajumuisha hali ya jumla na uchanganuzi wa wadau, uchanganuzi wa jinsia, umiliki, ubainishaji wa wamiliki wa haki na wadau, na mazingatio ya usawa katika utekelezaji, usimamizi, tathmini, na ujifunzaji.

## NYENZO YA 13: NYENZO - MWONGOZO WA TNC WA HAKI ZA BINADAMU KATIKA KUFANYA KAZI NA WAZAWA NA WENYEJI

Hadhira ya mwongozo huu ni wahifadhi, mameneja na viongozi wandamizi. Unatumika kwa kazi yote ambayo inaweza kuathiri Wazawa na wenyeji, ni muhimu katika viwango vyote vya kazi na mielekeo ya kimkakati, na ni muhimu licha ya dhima ya mradi. Mwongozo una msingi wake katika Kanuni na Kinga ambazo zinatokana na kujitolea kwa TNC kwa sheria na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Maudhui makuu ya mwongozo huu yanajumuisha masomo sita na yanahusisha orodha, violezo, zana, na uchunguzi kifani.

*Mwongozo huu pia unapatikana kwa Kiingereza, Kichina Kifaransa, Kiindonesia, Kireno, na Kihispania Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kupitia tovuti ya* **Mwongozo wa Haki za Binadamu**.

## NYENZO YA 14: MWONGOZO - MWONGOZO WA TNC WENYE KUZINGATIA USAWA WA KIJINSIA KATIKA UHIFADHI

Lengo la mwongozo huu ni kuwasaidia wahifadhi kufungamanisha mazingatio ya usawa wa kijinsia katika mradi au mkakati wa uhifadhi. Mwongozo huu unafuata mzunguko wa **Uhifadhi kupitia Usanifu (CbD) 2.0** na unajumuisha taarifa muhimu, nyenzo na rasilimali za kufanya uchanganuzi wa kijinsia unaojikita kwa ushahidi, kuandaa mpango wa hatua wa jinsia, kujenga mfumo unaozingatia jinsia unaojikita kwa matokeo (CbD Awamu ya 1); kufungamanisha mielekeo na shughuli ziinazozingatia jinsia katika utekelezaji (CbD Awamu ya 2); na usimamizi, tathmini, na kuripoti kuhusu matokeo yanayohusiana na jinsia (CbD Awamu ya 3).

*Mwongozo huu pia unapatikana kwa Kiingereza, Kichina, Kifaransa, Kiindonesia, Kimongolia, Kireno, na Kihispania.*

Isitoshe, **Warsha ya Kufungamanisha Jinsia kwa Uhifadhi unaojikita kwa Wazawa na Jamii** kwa kuzingatia mwongozo huu inapatikana kupitia conservationtraining.org, ambayo inaangazia uchanganuzi wa jinsia, mpango wa hatua wa kijinsia, usawa wa kijinsia katika ufuatiliaji, tathmini, na mafunzo, na ukatili wa kijinsia na usalama. Ili kupata mtaala wa mafunzo, wasiliana kupitia **conservationtraining@tnc.org.**



© MARK GODFREY/TNC

## Kipengele cha Msingi cha 2

# Uhusiano Thabiti wa Maarifa na Maadili

## Maarifa, Ushahidi na Mazoea

**HOJA KUU**

- Kwa Wazawa na wenyeji walio wengi tunaoshirikiana, uhusiano wa maarifa na mahali ni suala muhimu kabisa ya utambulisho na ustawi na chanzo cha kunufaishana kimazingira na maadili ya kujaliana.

- Kiwango na nguvu ambayo wanadamu hupitia, uhusiano na mahali huweza kutofautiana na kubadilika kulingana na muda kwa sababu ya mazingira tofauti ikiwemo muda uliotumika katika eneo, uzoefu kwenye maarifa ya eneo husika, historia, hadithi na mafundisho .na uwezo wa kuhusisha shughuli za kiutamaduni.

- Maarifa ya Wazawa na maarifa ya wenyeji hutofautiana na sayansi ya nchi za Magharibi, kwani mara nyingi yamekusanywa na kupitishwa kwa maelfu ya miaka, na hayatenganishwi na mahali, watu, na uhusiano baina yao. Maarifa ya Wazawa yanaendelea leo katika enzi ya sasa, baada ya ukoloni na yanaweza kufikiwa na watunza maarifa wanaoaminika.

- Lugha ya Wazawa, pamoja na utamaduni, hutoa na kuwezesha utunzaji wa mazingira kwa kuyabeba na kuyaweka kimuktadha maarifa ya Wazawa na kuweka mtazamo wa ulimwengu wa heshima wa ushirikiano na ulimwengu wa asili. Hii hujumuisha na kubadili maagizo ya awali, sheria za asili na za kiroho, mazoea na falsafa zinazofafanua uhusiano na mahali.

- Kila jitihada ambayo inahusisha maarifa ya wazawa lazima iheshimu haki za hati miliki na uhuru wa takwimu; uliodhibitiwa na kukubaliwa kuhusu chanzo na ufikiaji, na kujikita kwenye kusaidia kile ambacho jamii zinaamua na kufafanua kama mahitaji yao na makubaliano ya matumizi ya maarifa ya pamoja.

**MANENO YA MSINGI**

**Uhusiano wa mahali**—Uhusiano ulioanzishwa baina ya watu, jumuiya, jamii na mazingira yao kupitia miktadha ya kihistoria, kiutamaduni, kimazingira,kibinafsi na kijami[132]

**Uhuru wa Takwimu**—haki ya kudumisha, kudhibiti, kulinda na kuendeleza urithi wa kiutamaduni, maarifa na ujielezaji wa kiutamaduni pamoja na haki ya kudumisha, kudhibiti kulinda na kuendeleza haki miliki kati ya hizi.[133]

**Maarifa ya Wazawa**—mkusanyiko wa maarifa, mazoea na imani yanayobadilika na kuongozwa na michakato inayobadilika na kurithishwa kwa vizazi kupitia urithishwaji wa kiutamaduni kuhusu uhusiano wa viumbe hai (wakiwemo binadamu )kwa binadamu na baina ya binadamu na mazimgira yao.[15] Dhana hii wakati mwingine hujulikana kama 'maarifa ya wenyeji' kwa wale ambao hawajitambulishi kama wazawa.

**Uhamishaji wa maarifa kutoka kizazi hadi kizazi**—Urithishaji wa maadili, imani ujuzi wa asili wa Wazawa na wenyeji kutoka kizazi kimoja hadi kingine ( kwa mfano kutoka kwa wazee kwenda kwa vijana kwa njia ya masimulizi).[134]

**Sayansi ya Mataifa ya Magharibi**—unaolenga uhalisia na wenye kuhesabika—unaotegemea matumizi ya mbinu ya kisayansi kwa matukio ya ulimwengu. Mchakato wa mbinu ya kisayansi huanza na uchunguzi na kufuatiwa na nadharitet ambayo baadaye hufanyiwa majaribio. Kulingana na matokeo ya jaribio (na matumizi ya matokeo hayo), nadhariatete huwa nadharia ya kisayansi au "ukweli" juu ya ulimwengu.

## Uhusiano wa Mahali, Ustawi na Utunzaji wa Mazingira

Uhusiano wa mahali huhusisha mahusiano yaliyoanzishwa baina ya watu binafsi, jumuiya na jamii na mazingira yao kupitia miktadha ya kihistoria, kiutamaduni, kiroho, kimazingira, kibinafsi na kijamii[132] Uhusiano wa watu na mazingira huathiri utamaduni, mitazamo na utambulisho duniani.[135-136] Mahali ni mawazo ya jamii yaliyojengwa kutokana na sifa kwamba wanadamu huchunguza na kuelewa kutoka kwenye mazingira yao,[137] na kiambatanisho cha mahali ni fungamano la kihisia kwa mahali ambapo hutofautiana kwa nguvu.[138-139] Jamii nyingi za wazawa haziwezi kutenganishwa na mahali ambapo zimefungamana na lugha yao, majina,hadithi,nyimbo na miundo ya mashirika ya kijamii, maarifa,sherehe na masuala ya kiroho. Kwa wazawa na wenyeji ambao tunashirikiana, utamaduni na mahali mara nyingi ni sehemu muhimu kabisa kwa ajili ya kuwatambua watu na mtazamo wa kidunia wa mifumo yao ya kijadi ya utunzaji wa kanuni na matumizi ya ardhi, maji na rasilimali na mikakati ya uhifadhi ambayo ni sahihi zaidi.

Kwa jumuiya nyingi za wazawa, uhusiano huu wa mahali huenda zaidi ya utoaji katika maadili ya utunzaji wa aina mbili ambapo binadamu wamesaidia kutunza mandhari yanayowazunguka na ikolojia na muendelezo uliojengwa kwa muda mrefu.[140] Kwa wazawa, uhusiano na mahali mara nyingi ni hisia halisi. Pia, ni mchakato wa kisaikolojia, kijamii na kiutamaduni ambapo umeendelezwa kupitia ukoo, historia na majukumu. Baadhi ya wenyeji ambao hawajitambulishi kama wazawa ambao wanatunza rasilimali wanaweza pia kuwa na uhusiano imara ambao unahusiana na urithi na utamaduni wao. Ngazi hii ya mahusiano hupunguza uwezo na kubadilisha maeneo, hupelekea utegemezi mkubwa katika eneo maalumu na inaweza kupelekea kuwa na kiwewe (kwa mtu mmoja mmoja na kwa vizazi) endapo watu wataondolewa kwa nguvu, vurugu na mabadiliko ya tabianchi au namna nyingine.[144-145]

Utafiti wa kina unaonyesha kwamba uhusiano imara wa mazingira na mahali husababisha tabia imara za utunzaji wa mazingira na matokeo ya uhifadhi,[141,146-147,148-156] wakati uharibifu wa mazingira una athari hasi kwa wanadamu kisaikolojia na kiroho.[157] Utafiti pia unaonesha kwamba kwa kadri watu wanavyoishi kwa muda mrefu kwenye eneo ndivyo wanavyokuwa na uhusiano mkubwa.[158-159]

Ingawa wanadamu wote hupitia kiambatanisho cha mahali, kuna ngazi tofauti za ukubwa. Kwanini kiambatanisho hiki hutokea na kutofautiana na kulingana na mashirika ya kijamii, jografia,lugha na miundo ya utambuzi,taratibu za ibada,kanuni kuhusu matumizi ya mahali,na uzalishaji wa mali.[160] Dhana hii ya mwisho hususani uwezo wa mahali kuchangia kwenye maisha na usalama kwa utoaji wa chakula, maji, malazi,kujikimu mara nyingi ni chanzo na kiwango cha kiambatanisho cha mahali kwa wenyeji ambao ni wahamiaji wapya kwenye eneo na ukosefu wa utamaduni na historia ambavyo huwawekwa kwenye eneo hilo. Kwa hawa wenyeji, uhusiano umejikita zaidi kwenye fursa[161] Mabadiliko ya tabianchi yanaathari hasi kwa uhusiano wa mahali kwa wakulima wa Australia Magharibi. Haya mahusiano ya jumuiya yamefungamana na umiliki wao na ufanyaji kazi kwenye ardhi. Wanaelezea mashamba yao kuwa ni eneo wanaloishi na kufanya kazi. Kumbe maandishi yanabainisha uhusiano wa wazawa haumaanishi eneo wanalofanyia kazi bali urithi wao na sehemu muhimu ya utamaduni/utu wao[162-163] Kuna uhusiano wa kukumbukana baina ya jamii za wakulima zilizotajwa hapo juu na ardhi yao ambayo wanalia na uharibifu wa mazingira na uwezekano wa kuzorota kwa kiambatanisho cha mahali.[162] Mahusiano yao na mahali yanatofautisha kati ya mandhari yaliyofanyiwa kazi na asili. Hili pia ni tofauti na uwelewa wa wazawa ambapo viwili hivi vimeunganishwa. Utafiti wa ziada kwenye maeneo mbalimbali na utamaduni unahitajika kwa ajili ya uwelewa wa motisha ya wenyeji kwa ajili ya utunzaji wa mandhari kwa namna ambayo hunufaisha mazingira na fursa zao.

## Maarifa ya Wazawa, Maarifa ya Wenyeji na Mitazamo Miwili Sawa (kama ilivyoelezewa na Dkt. Albert Marshall)

Uhusiano baina ya watu, mahali na uelewa na utumiaji wao wa rasilimali zinazowazunguka unafahamika kama Maarifa ya Wazawa na wale wanaojitambulisha kama Wazawa, na maarifa kwa wale wasiojitambulisha kama Wazawa. Maarifa ya wazawa na maarifa ya wenyeji huhusisha vitendo vya kudumisha na kuboresha mazingira – ardhi, maji, mimea, na wanyama—na ni muhimu kwa utamaduni na fursa kwa jumuiya.[165-167] Katika mtazamo huu wa dunia, utamaduni unachanganyika na mahali na mifumo ya kijamii na ikolojia badala ya kutengana kama inavyoonekana mara nyingi katika mifumo ya huduma za mfumo ikolojia, na Maarifa Asilia na maarifa ya mahali hapo hufahamisha usimamizi wa maliasili. Kwa mfano, mara nyingi huzingatia idadi ya watu, makazi, na mandhari kwa ajili ya kuvuna na kudumisha spishi ambazo zinaweza kusababisha idadi endelevu ya watu na rasilimali za kutosha zinazopatikana kwa matumizi ya ndani (k.m., kwa dawa, chakula, vikapu, mitumbwi, n.k.).[167-168] Maarifa ya Wazawa ni pamoja na dhana ya heshima, usawa, na kitendo cha kuomba ruhusa, yote ambayo yanaenezwa kwa viumbe ambavyo si binadamu na kurithishwa kizazi hadi kizazi.[168,160]

Maarifa ya namna ya kutunza mahali na maliasili yamesababisha kuwa na mgawanyo uliobadilishwa na rasilimali nyingi ambazo zimesababisha wanasayansi wa bayoanuai kubaini mandhari zinazosimamiwa na wazawa.[169] Mandhari hizi sio maeneo yasiyoguswa ila ni maeneo yanayosimamiwa na kanuni, hadithi na desturi ambazo husaidia wingi[169] Kwa mfano, miongoni mwa Watlingit huko Alaska, kuna kanuni zinzaohusu kuingia maeneo nyeti ya kuzaliana na huhimiza idadi ya watu wenye afya kwa muda fulani.160 Nchini Kenya, wanawake wa jamii ya wafugaji wamekuwa na maarifa ya kiikolojia yanayohusiana na uangalizi wa kila aina ya viumbe hai, wanafahamu kiundani utegemeanaji kati ya roho na ardhi,ambapo hurithishwa kupitia vizazi.[170]

Kwa wazawa lugha ya asili imefungamana kwa ukaribu na maarifa na mahali. Hili huruhusu majadiliano zaidi,sababu kuna sifa za asili za lugha za wazawa ambazo hazifahamiki kwa wasio wazungumzaji wa asili na kwamba wanaunganishwa kwenye usimamizi wa mazingira na mahusiano na mifumo asili ya kidunia. Kupitia wazawa na kuweka kimuktadha maarifa ya wazawa na kuingiza mtazamo kidunia wa heshimu na muingiliano na ulimwengu wa asili. Lugha ya wazawa, sambamba na utamaduni, hulea na kuwezesha utunzaji wa mazingira. Lugha ya wazawa huyafanya hayo kwa namna zifuatazo:

- Maarifa ya wazawa au usawa ulio ndani kwa majina ya aina ya viumbe hai, maliasili, mahali na mifumo ya uainishaji wa historia ya masimulizi,
- Dhana za uwakili au usimamizi wa maliasili (uangalizi) ambako hakuna fasili ya moja kwa moja kwenye lugha nyingine,
- Miundo ya kiisimu ambayo huleta kunufaishana, muingiliano, usawa na heshima kwenye ulimwengu wa asili kutokana maono tofauti tofauti,
- Lugha ya mahali inayounganisha watu na mazingira yao na majukumu inayoambatana nayo, na
- Mila simulizi, hadithi, historia, na kile ambacho tamaduni nyingi huita “maagizo asilia” ambayo yana Maarifa Asilia na maadili ya mazingira na maadili.[171]

Maarifa na uwezo wa kufafanua kile kinachojulika kama maarifa halisi upo kwenye kiini cha uelewa na maarifa ya asili ya ukoloni[171] Kwa mashirika ya uhifadhi, sayansi ni msingi kwenye kazi ya uhifadhi, na kwa miaka mingi, fikra za kisayansi za magharibi zimekuwa kinara kwenye mambo mengi. Lakini kimashirika na kibinafsi tunatambua na kukubali kwamba kuna namna nyingi za kufahamu na kuelewa ulimwengu asilia na kwamba mbinu hizo ziendelee kushirikishwa kwa watu na kutumika na tamaduni mbalimbali duniani kote kwa kuwa wamezitumia kwa maelfu ya miaka. Kwakuwa Wazawa wamekuwa wakitunza ardhi zao na maji kwa maelfu ya miaka, maarifa ya Wazawa yanatoa taarifa nyingi kuhusu mahali kwa uwazi na mara nyingi kwa vipindi virefu. Vilevile, mashirika ya Kimataifa ya Kisayansi yanasisitiza kuwa maarifa ya wazawa yahusishwe kama vikamilisho muhimu kwa taarifa ya Kisayansi ya nchi za Magharibi. Wakati hili ni la kweli, halijakamilika pia. Maarifa ya wazawa siyo takwimu ambayo huweza kutolewa na kuwekwa kwenye mifumo ya sayansi ya nchi za Magharibi. Maarifa ya wazawa hutoa mafunzo ya namna ya kuishi katika maadili na kwa namna endelevu. Hutoa mfumo wa maarifa na uchambuzi na hautengamanishwi na mahali, watu na mahusiano baina yao. Maarifa ya wazawa huunganisha maarifa ya kina ya majaribio, uzoefu, majukumu ya kimaadili na kiroho, na maadili ya kiasili au undugu na uwajibikaji wa pamoja.[173] Kwa kuongezea, maarifa ya Wazawa hayatengamanishwi na mahali na mahusiano baina ya viumbe vyote kwenye eneo hilo.

Jamii za wazawa ni changamani. Suala la kushrikisha Maarifa ya Wazawa hutokea kwenye sura ya vipengele muhimu vya uchangamani. Wanaoheshimu Maarifa ya Wazawa sio wale wenye ufahamu wa kitaalamu au elimu ya mifumo ya maarifa, jamii yao imeongozwa kwa maelfu ya miaka. Wanaoheshimu Maarifa ya Wazawa wanajibainisha kwa kutumia dhana zao. Kuna mifumo ya asili ya utawala iliyokuwepo kabla ya serikali za sasa za makabila ambazo zinaweza kusimamia uhuru, maarifa na namna gani maarifa yanawafikia wengine na akina nani wana maarifa ya jadi.

Kufanya kazinna washirika Wazawa katika kulinganisha maarifa ya wazawa na mbinu za Kimagharibi za uhifadhi huchukua muda, heshima na uelewa wa kina wa changamoto na hatari ambazo andiko hili linaweza kuwasilisha. Kwa kuwa Maarifa ya Wazawa yapo wazi katika eneo na mahusiano ya Wazawa na mahali, tunahitaji kuanza kujihusisha na Wazawa wa maeneo tunayofanyia kazi na kuheshimu akili ya kijiografia na hekima ya mahali. Tunatakiwa kuelewa kwamba baadhi ya maarifa sio sahihi kushirikishana. Kinachoonekana bora siku zote ni kudhani kwamba taarifa yote ni siri na zaidi inaweza isikidhi au kuwa sahihi kwenye eneo kama “vituo vya taarifa” kwenye mifumo ya nchi za Magharibi, mbinu au namna ya kufikiri.Hatuwezi kudhani kwamba tunaweza kuhifadhi taarifa za miradi ya wabia kwenye kanzi data au lazima tuifanye taarifa hii iwe ya umma. Msisitizo maalumu na unyeti vinahimizwa kupitia uainishaji wa njia ya mfumo wa taarifa za kijiografia (GIS) na matumizi ya teknolojia nyingine ambapo usalama wa mtandao na hatari nyingine vipo. Kwa kusema hayo, baadhi ya Wazawa watakaribisha fursa kupeana majina ya Asili ya mimea na maeneo ili kurejesha utambulisho wa Wzawa nyumbani kwao na kuyafanya maarifa hayo yawe hai na yanayoweza kuhifadhiwa. Tutarajie kuwahusisha wenye maarifa kwenye zoezi linaloendelea la kuandaa maswali, utafiti na mipango ya usimamizi.

## Kuimarisha na Kudumisha Uhusiano wa Maarifa na Mahali

Angalia **“Nyenzo ya 15 : Kuainisha Tunu za kiutamaduni”** kwa mwongozo kuhusu kujumuisha maadili ya kijamii, kiutamaduni na viumbe hai kwenye Uchoraji wa ramani na Uwekaji Mipango”

Angalia **“Nyenzo ya 16: Makubaliano ya Hati miliki”** kwa makubaliano ya kiolezo cha hati miliki inayoweza kubinafsishwa kwa matumizi ya wazawa na wenyeji.

Angalia **“Nyenzo ya 17: Uhamishaji wa maarifa kutoka kizazi hadi kizazi na ushirikishaji wa vijana”** kwa seti ya zana zilizobuniwa kusaidia na kuimarisha programu za elimu za nchi kavu na majini kwa vijana wazawa.

Uhusiano wa mahali sio hali ya kuwa tuli ila kitu fulani ambacho huendelea kubadilika na kukua. Katika miaka mamia kadhaa kumekuwa na mabadiliko makubwa kwenye uhusiano wa binadamu na mahali. Kwa baadhi ya mazingira, kuzorota kwa uhusiano na maarifa na mahali ni matokeo ya ukoloni, kuhamisha watu kwa lazima na vurugu, shule za bweni za wakazi na uenezi wa dini zenye kuamini uwepo wa Mungu mmoja- kwa wengine ni kwa sababu ya michakato ya taratibu ya utandawazi, ubepari, mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa fursa katika eneo.[137,144,174-175] Hii haijaathiri Uhusiano wa maarifa na mahali pekee, lakini pia imehusisha usalama wa umuliki miundo ya utawala wa kimila na ustawi wa jumla wa binadamu.[160]

Kama tunataka tumiliki historia yetu kama Mashirika ya Uhifadhi, lazima pia tutambue na tukague kiasi gani uhifadhi umechangia kwenye huu utengano. Harakati za uhifadhi zimeondoa mbinu za wazawa kwa kulazimishwa kuondoka kwa kigezo cha kulinda, kuzuia ufikiaji wa kiutamaduni au mbinu za kufahamu wakati au matumizi ya mali asili na kwa kupuuza na kukandamiza mbinu za wazawa za kufahamu wakati wameshikilia Sayansi ya nchi za Magharibi hasa Ulaya na Amerika.[176-177] Uhifadhi umetengeneza dhana ya kutengana kihistoria kuliko kuwa na umoja ("Uhifadhi wa kutoruhusu binadamu kuchangamana na viumbe vingine") unawatenga watu na mazingira.[178] Mbinu iliyoainishwa kwenye mfumo wa VCA hutoa mbadala ambao husaidia kuanzisha upya au kuendekeza uhusiano wa maarifa na mahali. Tumedhamiria kutambua na kuinua jukumu la wazawa na wenyeji kama mawakili. Tukitambua kwamba usawa, uongozi na nguvu ya wazawa na wenyeji, haki salama, maarifa ya mwenyeji na utawala wa kimila ni muhimu kwa ustawi na malengo ya pamoja ya mazingira.

Baadhi ya njia ambazo tunazitumia kuimarisha na kuufufua uhusiano wa maarifa na mahali ni kuwakilisha kwa usahihi maadili ya kiutamaduni kwenye Uchoraji wa ramani na Uwekaji wa Mipango, uboreshaji wa wazawa na wenyeji katika kuyafikia, kuyatamia na kuyalinda maeneo matakatifu,kukuza uhamishaji wa maarifa, lugha na elimu ya vijana kati ya vizazi. Mifano hii na mingine ya kuchua hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa zinapatikana kwenye jedwali namba 7.

Uhuru wa takwimu unaohusiana na wazawa ni haki yao kuudumisha, kuudhibiti, kuulinda na kuuendeleza urithi wao wa kiutamaduni, maarifa na maelezo ya kiutamaduni na kimila sambamba na haki yao ya kudumisha kudhibiti kulinda na kuendeleza haki zao za kumiliki.[133] Wakati wa kuchunguza na kusaidia uhusiano wa mahali na maarifa yaliyopo kwa wazawa na wenyeji ni muhimu kuzingatia kwamba taarifa nyingi ni za hati miliki nyeti, watu binafsi wanaweza wasiwe na hiari ya kutoa taarifa hii na wasio wanajumuiya wanaweza wasiwe na haki kujua taarifa hii. Umakini unahijika kuheshimu na kulinda hati miliki na uhuru wa takwimu za wazawa na wenyeji. Hii inajumuisha ufikiaji wa pamoja wa makubaliano ya hati miliki, kuheshimu wazawa na wenyeji kutokusambaza taarifa ambayo hawataki kuisambaza na kuweka kipaumbele lengo la uwepo endelevu na matumizi ya maarifa ya wazawa na wenyeji. Pia huhusisha mambo kama kuomba ruhusu kila wakati na ridhaa na kuhakiki kutoka kwa jamii kabla ya kuwasilisha taarifa iliyopokelewa kuhusu kazi iliyofanywa pamoja na kuheshimu matakwa ya jamii kama haitaki hadithi isimuliwe (au hawataki shirika la uhifadhi liitoe taarifa hiyo).



© AMI VITALE

**Jedwali Na. 7**: *Mifano ya Shughuli Kusaidia Uhusiano wa Maarifa na Mahali.*

| Mbinu | Mfano wa Shughuli |
|---|---|
| Kuboreshwa ufikiaji na matumizi ya ardhi, maji na rasilimali | Kuwezesha kuolewa tena au ufikiaji na kutumia makubaliano kwa ardhi binafsi au ya umma yenye umuhimu kiutamaduni. Kusaidia mbinu za kijamii kulinda maeneo na viumbe wenye umuhimu wa kibaiyolojia na kiutamduni. |
| Kuwezesha elimu ya eneo husika, mafunzo na kubadilishana maarifa. | Kusaidia utiaji nguvu upya, usimamizi wa kimila wa ardhi na maji (mfano: moto wa jadi, usimamizi wa uvuvi na ujuzi (mfano, ujenzi wa mashua). Kuzingatia mifumo ya kijadi ya utawala kuwezesha ujifunzaji mbalimbali wa jumuiya na kuunganisha jamii ya mazoea. |
| Kuweka kumbukumbu ya maarifa ya wazawa na wenyeji | Kuweka kumbukumbu na lugha ya wazawa, kuweka kumbukumbu ya hadithi kutumia media anuani na teknolojia nyingine kuvutia vijana na kizazi kijacho, kuwekeza kwenye kujifunza maarifa, kalenda za msimu, mahali na majina ya viumbe na historia ya mdomo ikichukuliwa kama chanzo msingi cha maarifa kama ikihitajika kwa sifa za pamoja (umoja dhidi ya ubinafsi) kwa wenye maarifa na vyanzo vya maarifa. |
| Kusaidia uhamishaji wa maarifa kati ya vizazi | Kuongoza makambi ya utamaduni, kusaidia kufikia lugha za wazawa kuwezesha uhusiano wa vijana/ watu wazima kwenye ardhi na maji, kusaidia uhuishaji wa mazoea na sherehe za kiutamaduni. |
| Kuunganisha maarifa ya Wazawa, maarifa ya wenyeji  na Sayansi ya nchi za Magharibi | Matumizi ya lugha ya Asili kwa dhana, maji ya aina za viumbe na mahali katika sera na mpango, kuwezesha ujumuishaji wa maadili ya kiutamaduni kwenye uchoraji wa ramani na uwekaji mipango;k , kuinua maarifa ya wazawa na wenyeji kama namna muhimu ya ushahidi wa ubia wa vyuo na taasisi za utafiti. |
| Kuinua heshima na utambuzi wa mbinu za wazawa na wenyeji za kujua na kutenda | Kuwezesha kubadilishana maarifa baina ya mawakala wa serikali na wanasayansi wa magharibi ili kuinua namna ya kujifunza, usimamizi wa rasilimali, utawala na kuwezesha ushirikiano wenye ufanisi na heshima, kuwezesha ushiriki wa wazawa na wenyeji kwenye majukumu ya sera, kushiriki jinsi ya kujifunza kuweka msimbo, sheria ya kiutamaduni ya wazawa na wenyeji kuwa sheria ya kisasa. |

j. Kumbuka. uwekaji kumbukumbu unaofanywa na wazawa na wenyeji ni  kwa ajili ya wazawa na wenyeji ili waweze kuendeleza utamaduni na histoaria yao. Heshima ya haki ya hati miliki na uhuru wa takwimu kupitia mbinu mwafaka na michakato ni lazima.

k. Pia, muhimu kwenye kupata haki ya ardhi na rasilimali kama Uchoraji wa ramani na Mipango ni hatua muhimu katika mchakato. Heshima ya hatimiliki na uhuru wa takwimu kwa kupitia mbinu sahihi na michakato ni jambo la lazima





© ELYANA DASUKI

# Chunguzi Kifani

## Uhusiano wa Maarifa na Mahali nchini Mongolia

Mongolia imetawaliwa na Mfumo na Kiikolojia wenye nyika inayopanuka ambayo bado imekaliwa na watu wachache hadi leo. Watu waMongolia ni wenye asili moja wenye tofauti ndogondogo za kiutamaduni na staili za maisha zilizotokana na mfumo wa kiikolojia kama nyika, milima au misitu. Kuna utamaduni wa jadi wenye nguvu, mfumo wa maisha na mazoea vilivyounganishwa kwenye maeneo ya malisho ya mifugo. Wafugaji wanahamahama,wanaishi na kuchunga wanyama maeneo mbalimbali kutegemeana na msimu wa mwaka.

Kipengele muhimu cha utamaduni wa Mongolia ni heshima na kunufaishana kwenye mazingira katika maisha ya kila siku. Kama sehemu ya hili, watu wengi wanahisia kali kwenye mazingira na wanafanya matambiko.

> “Katika utamaduni wetu wa jadi, kama mtu anaheshimu mazingira, mazingira yatamrudishia mafanikio na bahati. Kwa hiyo, sherehe na maisha ya kila siku yanahusiana na dhana hizi. Wamongolia wamekuwa wakiamini kila wakati kuwa ardhi na rasilimali sio yao, ni mali ya roho. Tangu zamani katika karne ya 13, walimwamini Tengri, kiumbe wa mbinguni... imani kuu ilikuwa kwamba tulikuwa na roho hiyo katika kila mlima na mto na rasilimali hizi zilikuwa zake si za wafugaji. Inabidi kwa upole kuwauliza mizimu kutumia vipengele muhimu kama vile maji na nyasi na wanyama na wafugaji hufanya hivyo kwa kufanya ibada. Kwa hiyo, katika kila jumuiya, kuna mahali maalum ambapo watu huenda na kuabudu. Utamaduni huo ulikuwa mojawapo ya misingi muhimu ya mtazamo wa Wamongolia juu ya mazingira.”
>
> *-Gankhuyag Balbar juu ya mila na mambo ya kiroho ya Wamongolia*

Tamaduni za watu zimeathiriwa kwa mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi kwa karne nyingi, madadiliko ya hivi karibuni ya sheria za mali asili kwa kipindi cha miongo mitatu iliyopita, Mongolia imepitia kipindi cha mapito kutoka uchumi ulipangwa na serikali kuu na kupewa ruzuku kwenda mfumo wa demokrasia ya soko huria. Baada ya miaka ya 1990 jamii na siasa ya Mongolia vilibadilika kutokana na kuibuka kwa sekta ya uchimbaji madini, kilimo, ujenzi na utalii ambazo zilipelekea kuwa na haki za kimiliki mali na uchumi binafsi. Hii ilimaanisha mabadiliko ya kiutamaduni kwa kuwa hapo awali hakukuwa na dhana ya umiliki binafsi wa ardhi nchini Mongolia - kila kitu kilikuwa mali ya umma.

Licha ya mabadiliko haya, njia ya asili ya kuhamisha maarifa ya ndani huendelea ndani na baina ya familia. Uhamishaji wa maarifa, Imani na heshima kwa ulimwengu asili unadumishwa kupitia hadithi, nyimbo tenzi na kupitia ujuzi wao wa kijadi na mazoea ya kuwinda na kuchunga.

**PICHA YA AIKONI**
Maeneo ya Mfumo wa VCA

**NCHI KAVU** **MAJI SAFI** **PWANI**

"Wazazi wanafundisha watoto wao kwa vitendo... wakiwa na umri wa miaka mitatu hadi mitano ni jambo kubwa kuwafundisha watoto wako kupanda farasi. Wazazi wanafurahi... mara tu unapowaanza kuwafundisha kupanda farasi, unaweza kuwasaidia wazazi wako kuchunga mifugo. Wanawafundisha kila kitu. Wanafundisha kuhusu mimea, mimea ipi ni mizuri kwa wanyama na mimea ipi ni mibaya. Mababu na bibi ndio walimu bora kwa sababu wana maarifa, na ni muhimu sana kwao kuhamishia maarifa hayo kwa watoto wao ili waweze kuwa wachungaji bora."

*-Gala Davaa juu ya Uhamishaji wa maarifa kutoka kizazi hadi kizazi*

Mwaka 2012 bunge la Mongolia lililidhia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali wa Kijamii inayohusu haki za pamoja. Kazi nyingi za awali za awali za mtandao na wafanya kazi wa TNC na uhamasishaji wa kijamii kuhusu haki hizi na namna ya kuzitekeleza. Kufanya kazi pamoja, wafugaji waliunda mikataba ya usimamizi wa maliasili wa kijamii na mashirika ya kijamii (CBOs). Uanzishaji wa mashirika haya ni kuwezesha ujenzi wa mfuko, heshima ya pamoja, ushirikiano na hatua ya pamoja na umoja miongoni mwa watu ambao kihistoria waliishi kwa kujitegemea, waliotupwa mbali kwenye mandhari kubwa.

Mafunzo ya mipango ya usimamizi wa kijamii na rasilimali asilia huwapa watu wa Mongolia fulsa ya kuongeza maarifa kwenye mfumo wa kisasa kwa kudumisha uhusiano kwenye ardhi yao na mifumo ya maisha. Kama hivyo, uhusiano wa mahali na muendelezo wa utamaduni huu umepewa kipaumbele kwenye uhifadhi wa kijamii nchini Mongolia.

*Michango na nukuu za wafanyakazi wa TNC Mongolia Gankhuyag Balbar na Gala Davaa*

## Maarifa ya Wazawa nchini Alaska

Uhusiano wa watu na Mahali nchini Alaska unawakilishwa na Tundra na eneo dogo la Arctic, kwenye misitu ya mvua ya milima ya Kusini – Mashariki. Uhusiano wa wazawa na mahali, utamaduni na maarifa ni wa zamani na wa kisasa, ikielekea kwenye usimamizi wa kijamii wa ardhi nzuri na maji. Nchini Alaska, kwa vizazi mtambuka kwa maelfu ya miaka, uhusiana na mahali ulipitia mizunguko ya asili. Wazee huelezea mifumo ya maisha ya kuhama hama na makambi wakati wa vuli, kiangazi, kipupwe, na masika. Watu wanaweza kufuata mizunguko tofauti tofauti ya maisha, wakijongea pale wanapopataka ili kujikimu wenyewe kulingana na sheria za asili,desturi, imani za kiroho na mfumo wa maarifa yaliyopatikana. Zilikuwa za kubadilika muda wote zikiwa kwenye mzunguko wa maandalizi kwa ajili ya misimu mingine.

"Kuwa kwenye mahusiano sahihi na mahali pako lilikuwa ndio la msingi. Kwa kiasi ambacho ardhi inatumika na kutupa mahitaji ni wajibu wetu pia tuzitunze rasilimali na ardhi; usimamizi ni yale mazoea ya kutunza na kutunzwa na mazingira yapo ya asilia. Hayo mahusiano ya maisha na usawa kuendelea leo na kurithishwa kizazi hadi kizazi."

*-Andrea Akall'eq Burgess (Yup'ik)*

Kote Alaska, Wazawa hutumia maarifa ya kiutamaduni na kimila kuonyesha kwa vitendo usimamizi kwa ustawi  na maisha. Mfano mmoja upo kwenye uhusiano wao na Salmon, kama ndugu.

> "Maarifa ya asili yanakuelekeza usivute wimbi la kwanza la samaki, inabidi uruhusu mvuo huo wa kwanza ufike kwenye sehemu za maji na kisha unaweza kufanyia kazi mavuno yako... Utambuzi kwamba hata kama tuna njaa ya samaki wabichi huko. kwanza, lazima umruhusu apite, ukiheshimu wale ambao ni aina zenye nguvu zaidi zinazostahimili, wanaojua mahali pa kurudi, na kuhakikisha wanafika hadi kwenye maji mengi ili vizazi vyao viweze kurudi katika miaka ijayo kwa idadi kubwa."

Wayup'k kabla ya ukoloni walitambulika kwa kuwa na athari kwa vitu vilivyowapa uhai endelevi utengaji wa makambi na kuacha ardhi kwa namna ambayo iliyoonekana "haijguswa", wakijua kutokana na maelezo ya awali kwamba haya mazoea yata ruhusu ndege wanaohamahama na aina nyingine muhimu za viumbe watarudi. Hata hivyo, mabadiliko yaliyoletwa na ukoloni yamekuwa ya kushangaza.

> "Ilibidi tuyaache mazoea yetu mengi, ilibidi tuweke blanketi kwenye maarifa yetu ya wazawa naya kiroho, ilibidi tuyafiche kabla hayajawa jinai na kupotea kabisa. Wanasema sasa tupo kwenye muda wa kuvua blanketi sababu  kuna usalama tena na vijana wetu wanatamani hayo maarifa,shukrani, maarifa haya yanatumika tena."
>
> "Harakati za kuponya zipo mbele na katikati, huwezi kuzungumzia lugha au ulinzi wa ardhi au kuja mkono kwa mkono na namna watu wanavyofikiria mwamko huu. Tunao msemo, Tsu Héidei shugaxhtootaan, yá yaa khusgédaakeit, haa jeex' anakh has kawdak'eet'. Ambao maana yake sasa tutafungua hili sanduku la maarifa" na ni msemo wa wazee ambao hurithishwa kizazi hadi kizazi. Ilituchosha."
>
> *-Crystal Nelson (Tlingit)*

Hili ni tamanio linalotoka kwa vijana Wazawa wenyewe na mfumo umekuwa ukiruhusu, wazee wanajua kwamba kuponya ardhi na kuponya watu huenda kwa pamoja. Ni wazi kuwa, kuponya ardhi, maji na watu huhusu kufungua na kukumbuka mazoea ya kiutamaduni na namna ya kujifunza.Harakati hizi zinaibuka kupitia wazawa vijana ambao wanatafuta urithishwaji wa maarifa ya wazawa na kiutamaduni kwa vizazi na vizazi, utunzaji, maadili, mazoea na kanuni.

# Nyenzo na Rasilimali

## NYENZO YA 15: MWONGOZO -KUAINISHA TUNU ZA KIUTAMADUNI

Mfumo wa TNC wa Maendeleo kwa Usanifu (DbD) huheshimu tunu za jamii zikiwemo za viumbe hai, kiutamaduni, maadili ya jamii na kiuchumi – Kwenye mchakato wa tathimini ya athari kwa ajili ya mapendekezo ya maendeleo. DbD hutoa muonekano wa jumla wa namna maendeleo ya baadaye yanavyoweza kuathiri maadili haya na hutoa majawabu kwa ajili ya maamuzi sahihi. DbB hutumia Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (GIS) na nyenzo za kuanzisha na kutathmini na kuonesha kwa vitendo athari ambazo zinaweza kutokea kwenye haya maadili yanayohusiana na jamii. DbD hukubaliana na dhana na ridhaa ya awali na ya kumaanisha na huyapa makundi fursa kushiriki kwa ukamilifu kwenye mchakato wa maamuzi ya maendeleo. Mwongozo huu uliandikwa kwa kuzingatia uzoefu wa kuainisha maadili ya kitamaduni nchini Australia, lakini unaweza kutumika popote.

## NYENZO YA 16: KIOLEZO - MAKUBALIANO YA HATI MILIKI

Mchakato wa kuimarisha uhusiano wa maarifa na mahali lazima uwe wa msingi kwa kuhusisha hadithi za wenyeji na ushahidi. Wakati tukifanya ubia na wazawa lazima tuheshimu taarifa kuhusu watu, maarifa yao na mipaka yao. Wale wanaofanya kwenye eneo hili wakitafuta kuchapisha taarifa au takwimu lazima wafuate itifaki sahihi katika kuanzisha dhana ya ridhaa ya awali na ya kumaanisha kabla ya kuchapisha kuhusu wazawa au maeneo yao. Mbali na kuheshima haki miliki na uhuru wa takwimu wa Wazawa na wenyeji, TNC imetengeneza kiolezo cha makubaliano ya kushirikishana data na taarifa ambacho kinaweza kurekebishwa kulingana na muktadha.

*Kiolezo hiki pia kinapatikana kwa kihispania, Kireno na Kiindonesia*

## “NYENZO YA 17: ZANA - UHAULISHAJI WA MAARIFA KUTOKA KIZAZI HADI KIZAZI NA USHIRIKISHAJI WA VIJANA

Zana ya kusaidia Mawakili Wazawa Wanaochipukia (SEAS) ilitengenezwa na Umoja wa kwa kushirikiana na wadau na jamii kusaidia kuimarisha programu zinazohusu ardhi, maji na elimu kwa vijana wazawa. Ilianzishwa ili kutoa mawazo, mapendekezo na muongozo kwa yeyote anayefanya kazi ya kuendeleza na kupeleka aina hizi za program. Zana hii ni kwa yeyote ambaye amependa kuanzisha au kimarisha programu za ardhi na za elimu ya maji kwa vijana wa zana hii imepangwa kwenye sura sita, kila sura ambayo hujibu maswali ya muhimu yanayohusu namna ya kubuni, kutekeleza na kuimarisha programu hizo kwa muda mrefu.

*Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kwa kutembelea* **tovuti ya SEAS.**



### Jambo la Msingi la 3

# Matokeo Endelevu kwa Ajili ya Watu na Mazingira

## Maarifa, Ushahidi, na Mazoea

**HOJA KUU**

- Fedha za uhifadhi – zikijumuisha mchanganyiko wa taasisi za fedha – zinahitajika kwa ajili ya kuongezea kwenye fursa endelevu za maisha kwa ajili ya kuwa na uendelevu wa kifedha kwa ajili ya uhifadhi kwa njia ya jamii.

- Vipengele vya msingi vya kupata jawabu la upatikanaji wa fedha za uhifadhi ni suala la uwekezaji endelevu wa kuwajengea uwezo mashirika ya wazawa na wenyeji; umiliki wa wazawa na wenyeji na kuongoza jitihada za kutafuta fedha za uhifadhi; uhakika wa umuliki; msaada wa kisiasa; jitihada zinazoendelea za kutafuta fedha; kuwa na vyanzo mbalimbali vya fedha; majukumu na wajibu ulio wazi ndani ya mkakati wa fedha; ushirikiano na sekta binafsi kwa ajili kupata majawabu ya kibiashara; na upatikanaji wa fedha unaoendana na fursa mpya zinazojitokeza.

- Ushirikiano wenye mafanikio wa utafutaji fedha ulimwenguni unahusisha muunganiko madhubuti na vipaumbele vya wazawa na wenyeji, uelewa wa kutosha wa muktadha katika utoaji wa ruzuku, ushirikiano madhubuti mashirika ya wazawa na ya wenyeji yanayotekeleza miradi, na uwezo wa kukuza mazingira wezeshi kwa miradi migumu. Wasuluhishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali huwa na mchango muhimu sana katika michakato hii.

- Mabadiliko ya sera katika za chini, kimkoa na/au kitaifa yanahitajika mara nyingi kwa ajili ya kuleta mazingira wezeshi na nafasi kwa wazawa na wenyeji kwa ajili ya kurasimisha hali zao za kutumia ardhi, maji na rasilimali, kuratibu mamlaka yao katika kufanya maamuzi yanayohusiana na rasilimali, na kushiriki katika fursa mbalimbali endelevu za maisha.

- Viwango na mfumo wa uenezaji vinategemea sifa za utaratibu uliopo wa usimamizi wa maliasili, jamii zenyewe, na muktadha. Kusaidia mitandao ya jamii na mfumo wa kubadilishana maarifa kati ya jamii na jamii ni njia muhimu ambazo mashirika ya uhifadhi yanaweza kutumia katika kuimarisha uenezaji wa uhifadhi kwa njia ya jamii na mbinu zake.

**DHANA KUU**

**Fedha za Uhifadhi**—taratibu na mikakati ya kutafuta, kusimamia na kutumia rasilimali fedha na kuendana na vichocheo vitakavyofanikisha kupatikana kwa matokeo ya uhifadhi wa mazingira.[98] Fedha za uhifadhi zinalenga kugharimia kwa ukamilifu gharama za uhifadhi na kuhakikisha kuwa kuna uendelevu wa kifedha.[180]

**Uenezaji**—mchakato wa awali wa kubadilisha utaratibu kwenye kundi la watu unasababisha uwezeko wa kutokea mabadiliko kwa wengine.[181]

**Uendelevu**—uwezekano wa kuwa na matokeo chanya kwa watu na mazingira kupitia jitihada za uhifadhi kwa njia ya jamii kuendelea kuwepo kwa muda wote. Vipengele muhimu vya uendelevu ni pamoja na upatikanaji wa muda mrefu wa fedha za uhifadhi, kuwa na mazingira wezeshi ya kisera, na uenezaji/kupanuka kwa uhifadhi wa jamii.

**Kupanuka kwa uhifadhi wa jamii**—kasi na mifumo ya mabadiliko, na kusambaa kwa sera za uhifadhi wa njia ya jamii, programu, miradi na mbinu za uhifadhi.[182] Inaweza kujumuisha ukuaji wa mbinu za uhifadhi katika eneo moja na kutumia mbinu hizo katika maeneo mengine.

Uendelevu wa uhifadhi kwa njia ya jamii unamaanisha kuwa matokeo chanya ya uhifadhi kwa watu namazingira yatakuwa ya kudumu. Uendelevu unaendana kwa karibu na nguzo nne za Mfumo wa Marekebisho ya Uthamini wa Mkopo kwa kuweka msingi imara na kutengeneza mazingira wezeshi kwa ajili ya kuwa na matokeo ya muda mrefu – vile vile, nguzo za Mfumo wa VCA zinahitaji kuwa endelevu. Vipengele muhimu vya uendelevu ni pamoja na upatikanaji wa fedha za uhifadhi wa muda mrefu, uwepo wa mazingira wezeshi ya kisera, na uenezaji/kupanuka kwa jitihada za kuendeleza uhifadhi kwa njia ya jamii.

## Fedha za Uhifadhi

**Angalia "Nyenzo ya 18: Mwongozo wa Fedha za Uhifadhi" kwa ajili ya kupata mwongozo wa kufanya tathmini, kupanga mipango, na kuandaa majawabu ya upatikanaji wa fedha za uhifadhi.**

Fedha za uhifadhi ni utaratibu wa kutafuta, kusimamia na kutumia rasilimali fedha na kuendana na dhamira ya kufikia malengo ya uhifadhi, na zinalenga kugharimia gharama zote za uhifadhi – ambazo huwa hazitolewi kwa ukamilifu na jitihada zinazofanyika za kuendeleza maisha endelevu – na kuwa na uendelevu wa kifedha wa muda mrefu. Fursa za maisha endelevu na fedha za uhifadhi vinafanya kazi pamoja kwa ajili ya kutoa kipato mara dufu kwa watu na mazingira. Fursa endelevu za maisha zinatoa kipato kwa watu ili waweze kumudu mahitaji ya kaya zao, na hivyo kuwa na maisha salama na yenye hadhi, kutoa motisha ya usimamizi endelevu wa rasilimali, na kupunguza shinikizo za kukosekana kwa maendeleo endelevu. Fedha za uhifadhi ni kwa ajili ya kuzisaidia jamii ziweze kuwa na mfuko wa muda mrefu wa kusimamia matumizi ya ardhi, maji na rasilimali kwa kulingana na maono yao ya usimamizi na uwakili wa maliasili.

Katika mazingira mengi, mchanganyiko wa vyenzo mbalimbali zinawekwa pamoja (mf. Vivutio vya masoko, ushuru, ruzuku, mtaji kutoka sekta ya umma na sekta binafsi/ hatifungani) na fedha hizo zinatolewa kwa njia ya ruzuku, malipo kulingana na utendaji, na huduma ndogondogo za fedha. Ripoti ya hivi karibuni inaonesha kuwa masuala muhimu ya mafanikio katika majawabu

ya kudumu ya upatikanaji wa fedha za uhifadhi yanahusisha jitihada za utafutaji wa fedha; kuwa na vyanzo mbalimbali vya fedha; kuwa na majukumu na wajibu ulio bayana kwenye mkakati wa utafutaji wa fedha; ushirikiano na sekta binafsi kwa ajili ya kuwa na majawabu yanayoendana na mazingira ya kibiashara; na fedha zinazoendana na fursa mpya.[180] Mbali na hayo, ripoti inahitimisha kuwa mafanikio ya jitihada za uhifadhi zinazofanywa na Wazawa na wenyeji yanatokana mfuko wa fedha za uhifadhi unaolenga kuwawezesha Wazawa na wenyeji kama mawakili, na siyo wanufaika, ambapo "uwakili" siyo tu ni jukumu la usimamizi wa maliasili, bali unajulikana kuwa sehemu ya umiliki, uwezo wa kufanya maamuzi, na uhifadhi ambao unahusishwa katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni katika jamii.

Fedha za uhifadhi ni msingi wa mafanikio ya muda mrefu ya jitihada za kupigania haki, kuongeza uwezo, kuongeza ushiriki katika majadiliano na maamuzi, na kusaidia kukuza fursa za maisha – kama ambavyo nguzo hizi za mfumo wa VCA zilivyo muhimu katika kupata na kuendeleza fedha za uhifadhi. Kwa mfano, siyo tu kwamba fedha za uhifadhi ni muhimu kwa ajili ya kupata haki (mf. Kwa kuwezesha uanzishwaji wa maeneo yaliyohifadhiwa) lakini pia kupata haki za umiliki ni hitaji muhimu la kupata huduma za kifedha kama vile mikopo benki. Mbali na hayo, mipango wa muda mrefu wa upatikanaji wa fedha unaiwezesha jamii kulinda ardhi na maji visivamiwe na watu wa nje na kuziwezesha jamii ziweze kusimamia. Hili lilifanyikwa kwa Makubaliano ya Msitu Mnene wa Bear, ambao ulihusisha mpango wa utetezi wa Wazawa na wenyeji wa Kanada, ambao ulitenga eneo kubwa lenye thamani kubwa kiikolojia katika eneo la pwani ya Pasifiki ya Canada kwa ajili ya kuwa na ulinzi na usimamizi wa mfumo wa kiikolojia. Kupitia makubaliano haya, Wazawa na Wenyeji wa Kanada wana mchango mkubwa katika utawala, kufanya maamuzi na usimamizi. Ili kuhakikisha kuwa mkataba huu unakamilika kulihitajika utayari wa kutoa fedha, ambazo zilipatikana kupitia mkataba wa fedha za uhifadhi ulioitwa "Coast Funds." Mfuko huu wa kusaidiana utaendeleza jitihada za kuendeleza uhifadhi, na ukijumlisha mfuko kwa ajili ya kuendeleza shughuli endelevu za uhifadhi. Matokeo ya msingi ya makubaliano haya ni pamoja na utambuzi rasmi na wa kiutendaji wa majukumu ya jamii kama wamiliki na wasimamizi wa rasilimali za kanda.

Ili fedha za uhifadhi ziweze kuwa na mafanikio katika muktadha wa uhifadhi kwa njia ya jamii, jamii na taasisi za wenyeji zinatakiwa ziwe na uwezo wa muda mrefu wa kuongoza katika kutafuta, kusimamia na kutumia fedha. Uwezo unahitajika kwa ajili kuendeleza mahusiano ya ndani na mahusiano na wadau wa nje; usimamizi wa ardhi na maliasili; uwezo na urahisi wa kuendana na mazingira ya kibiashara na taratibu za serikali; na usimamizi wa fedha bila ya kuathiri tunu.[180] Mchakato wa kupata fedha za uhifadhi mara zote unahusisha jamii katika kuandaa mipango yao na mipango ya matumizi ya rasilimali, jambo linalowezesha kuwa na mfumo bora wa uongozi na mamlaka katika kufanya maamuzi kuhusu namna ya kutumia rasilimali na kuzigawanya. Wafadhili na Asasi Zisizo za Kiserikali ni vema ziweke kipaumbele katika kujenga uwezo. Mifumo mingi ya utoaji wa fedha za uhifadhi kwa uwazi kabisa inahusisha pia fedha kwa ajili ya utawala bora na kujenga uwezo. Kwa mfano, mifuko ya fedha za majimbo ziko kwa ajili ya utawala na kuwajengea uwezo wamiliki wazawa wa eneo la hifadhi la Warddeken nchini Australia (linamilikiwa na kusimamiwa na Kampuni ya Kampuni ya Usimamizi wa Ardhi ya Warddeken). Taasisi na miundo ilianzishwa au kuimarishwa kama sehemu ya kupata fedha za uhifadhi, ambazo kwa hapo baadaye zingetumika katika masuala mengine (mf. Afya, ustawi wa maisha ya watu, elimu na usuluhishi wa migogoro), kusawazisha na kujenga uwezo mara kwa mara na kuimarisha mazingira wezeshi kwa ajili ya kupata matokeo bora kwa ajili ya watu na mazingira.[180]

Utafiti wa hivi karibuni umeonesha kuwa kanuni na masharti ya wafadhili yametajwa kama kikwazo kwa mashirika ya Wazawa na wenyeji katika kupata fedha kwa ajili ya kuhalalisha umiliki na usimamizi wa misitu.[183] Katika mazingira mengi, kanuni na masharti ya wafadhili yanayokwamisha yanatokana na utambuzi wa kisheria wa mashirika ya Wazawa na wenyeji na/au usimamizi wa miradi mikubwa inayohitaji rasilimali nyingi na sheria za utoaji taarifa. Wafadhili wengi hutumia mashirika ya kati kama daraja kwa ajili ya kusawazisha misimamo yao

ya kisheria pamoja na usimamizi wa mradi na uwezo wa kiutawala kwa ajili ya kuwa wakala wa fedha kati ya wafadhili na Wazawa na wenyeji. Kwa mfano, katika kujibu changamoto za utoaji wa fedha kwa mashirika ya wazawa na wenyeji, Mfuko wa Amazonia (Fundo Amazônia)[I] nyakati fulani umeshirikiana na taasisi za kati kutoa ruzuku na kusaidia mradi na kuendana na masharti ya uandishi wa ripoti ya taasisi kubwa kama vile Benki ya Maendeleo ya Brazil, ambayo ni msimamizi wa mfuko huo. Kwa ajili ya kutatua changamoto za utoaji wa fedha na kutekeleza matakwa ya wafadhili, fedha hizo wakati mwingine hutolewa kupitia mashirika ya kati ya ndani ya nchi ambayo yanakidhi mahitaji ya uaminifu na ni washirika yanayoaminika na mashirika ya Wazawa na wenyeji. Mashirika hayo yana mizizi ndani ya jamii, hasa yale yenye viongozi wazawa au uzoefu wa kutosha wa kufanya kazi na wenyeji, yameonesha kuendana kwa ufanisi mkubwa na mahitaji ya Wazawa na wenyeji na vipaumbele vyao, na hivyo kuwa na sifa za kuwa mashirika ya kati kwa ajili ya kutoa ufadhili wa kifedha.[183]

Zaidi ya hayo, mashirika ya Wazawa na wenyeji yanachukulia Mashirika yasiyo ya kiserikali yaani NGO na mifuko binafsi ya fedha kuwa wanaendana na vipaumbele vyao kuliko wahisani wengine, na yanatoa fedha za moja kwa moja. Faida zinazohusiana na mashirika suluhishi ya NGO ni pamoja na uelewa mkubwa wa mazingira ya utoaji wa ruzuku, ushirikiano madhubuti na mashirika ya wazawa na jamii za wenyeji katika kutekeleza miradi, na uwezo wa kuimarisha mazingira wezeshi ya kisiasa kwa miradi migumu. Kwa mazingira fulani, mashirika haya suluhishi ya NGO yameimarisha faida hizi kwa kuwajumuisha wawakilishi wa wazawa na wenyeji katika masuala ya kiutawala au kwenye vyombo vya ushauri.[183] Utafiti zaidi unahitajika kuunga mkono taratibu za wafadhili za kukabiliana na mabadiliko na mahitaji ya uwajibikaji kwa ajili ya kuwezesha fedha zaidi za moja kwa moja kwa mashirika ya Wazawa na wenyeji. Hata hivyo, faida za mashirika suluhishi ya NGO yanaonesha maeneo muhimu ya kujielekeza zaidi, ukiacha fursa kwa wahisani kuboresha uratibu na kuwalenga wasuluhishi wanaoaminika; kupunguza urasimu; kufanya mabadiliko ya muundo wa utoaji fedha kulingana na mahitaji ya maeneo husika; na jambo la muhimu zaidi ni kuongeza fedha kwa ajili ya uhifadhi kupitia Wazawa na wenyeji.

Kwa ajili ya majawabu ya kudumu ya upatikanaji wa fedha, jitihada ambazo zimeleta manufaa za kutokana na ushiriki madhubuti wa mashirika ya nje yasiyo ya kiserikali ambayo yanahitaji uwepo wa uwezo wa ndani kabla ya kuwepo kwa NGO. Ni muhimu kwa utawala wa eneo husika na mamlaka zake kuwa tayari kuendeleza yale yaliyofanywa baada ya ushirikiano na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kufikia tamati ili kuepuka kuona jamii inakumbana na tatizo la kusitishwa kwa usimamizi wa maliasili na mifumo ya upatikanaji wa fedha. Kwa mfano, Mfuko wa Nyanda za Malisho Kaskazini – taasisi isiyo ya kifaida kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa uhifadhi maeneo ya kaskazini mwa Kenya – umekuwa ukiendesha programu ya majaribio kwa ajili ya kuhitimisha baadhi ya miradi ya uhifadhi iliyoisaidia kwa miaka 15, kuelekeza ushirikiano kwenye eneo moja muhimu la uhifadhi na kujitegemea, kutoa mafunzo kuhusu uongozi na uwezo wa kujitafutia fedha kwa ajili ya hifadhi ziweze kuomba fedha zenyewe moja kwa moja. Uwekezaji ulihitajika kwa ajili ya mpito, hasa kwa maeneo yenye uwezo mdogo sana, na hilo lisipuuzwe.[180] Masuala kama hayo yanazingatiwa kwa ajili ya fedha za uhifadhi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wenyeji ili waweze kuwa na mipango ya muda mrefu wa kupata fedha endapo mashirika yasiyo ya kiserikali yataondoka. Lengo ni kuwa na kipindi cha mpito cha usimamizi wa miradi ya uhifadhi, jambo linalohitaji uongozi makini na unaochangamka kwa ajili ya kuwa na mpango wa kuandaa viongozi wa baadaye kwa lengo la kuendeleza uwezo uliopo baada ya viongozi waliopo kuondoka na kuwa na uhakika wa kuwaachia wengine majukumu yao.

---

I. Mfuko wa Amazon ni utaratibu wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutokana na Ukataji miti na Uharibifu wa mazingira (REDD+) iliyoundwa ili kuchangisha michango kwa ajili ya uwekezaji katika juhudi za kuzuia, kufuatilia, na kupambana na ukataji miti, pamoja na kukuza uhifadhi na matumizi endelevu ya Amazon ya Brazil.

## Sera

Uhifadhi kwa njia ya jamii mara nyingi huhitaji kuunganishwa kwa mabadiliko ya sera na hatua za usimamizi wa maliasili ikiwa zana zinazofaa za kisheria hazijawekwa.[184] Katika hali hii, mabadiliko ya sera katika ngazi ya mtaa, kimkoa, na/au kitaifa yanahitajika ili kuwa na mazingira wezeshi ya uhifadhi kwa njia ya jamii—haswa, kwa Wazawa na wenyeji kurasimisha haki zao juu ya ardhi, maji na rasilimali, na kuratibu mamlaka yao katika kufanya maamuzi juu ya maliasili. Sera kama hizo zinaweza kujumuisha utambuzi rasmi wa mamlaka na taasisi za Wazawa na serikali ya kitaifa, zile zinazosababisha ugatuzi wa haki na majukumu ya usimamizi kwa jamii, zile zenye mipangilio ya usimamizi shirikishi kati ya jamii na serikali, na zile zinazoanzisha vyombo vya kueleweka kwa ajili ya ushiriki wa Wazawa na wenyeji katika kufanya maamuzi ya usimamizi wa maliasili.

Kwa mfano, nchini Brazili, Katiba ya nchi ya 1988 iliweka msingi wa utambuzi wa haki tofauti za wazawa, na pia kuhamasisha uanzishwaji wa Vitengo vya Ardhi Asilia na Uhifadhi.[185] Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira na Maeneo kwenye Ardhi ya Wazawa (PNGATI) ilipitishwa mwaka 2012 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa maeneo ili Wazawa na mashirika yanayowawakilisha waweze kuhifadhi, kutetea, kusimamia, kutumia na kutawala ardhi yao ili kudumisha uhifadhi wao, na kuthamini na kukuza ustawi wa pamoja wa watu wao. Kupitia chombo hiki cha kisera, Mipango ya Usimamizi wa Maeneo na Mazingira inatengenezwa na Wazawa na taasisi zinazowawakilisha. Mpango huu unakamilishwa kwa kupitia mchakato shirikishi, ni mchakato wa wadau wengi ambao unaoweka ramani na kupanga kwenye kanda maeneo muhimu kwa kimazingira, kijamii na kiutamaduni, na wenye tija kwa Wazawa, kulingana na ujuzi wao.

Katika mfano mwingine, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya 2013 ya Kenya ilianzisha mfumo uliofafanua kisheria na kutambua rasmi uanzishwaji wa maeno ya uhifadhi - matumizi bora ya ardhi yanayotambulika yanayoipatia jamii haki za matumizi ya ardhi na rasilimali na upatikanaji wa vivutio kadiri wanavyoshiriki katika ulinzi wa wanyamapori na desturi nyingine endelevu - kutota muundo wa kisheria wa wazi kwa ajili ya uhifadhi kwa njia ya jamii.[186] Hii ilioanishwa na kuanzishwa kwa Umoja wa Uhifadhi wa Wanyamapori cha Kenya, umoja huu mpya unawakilisha uhifadhi kwa njia ya kutengeneza sera katika ngazi ya kitaifa. Sheria hiyo ilihitimisha jitihada za zaidi ya muongo mmoja za kupata sheria inayojitosheleza na kuratibu maoni ya mashirika ya kiraia ya mazingira, na ilikuwa muhimu kuweka muktadha unaofaa kwa ajili ya uhifadhi kwa njia ya jamii nchini Kenya. Katika Brazili na Kenya, mashirika ya uhifadhi yalifanya kazi kwa ushirikiano na Wazawa na wenyeji ili kutetea mabadiliko muhimu ya sera, na pia kuunga mkono uongozi wa Wazawa na wenyeji katika utekelezaji wa sera.

Kama ambavyo mazingira wezeshi ya sera ni muhimu kwa ajili ya kupata haki na ushiriki katika kufanya maamuzi, pia ni muhimu kwa ajili ya fursa nyingi za maisha ambazo jamii zinaweza kutafuta. Mifumo ya malipo kwa ajili ya huduma za mazingira (PES)—kwa mfano, masoko ya hewa ya ukaa—yanahitaji kuwepo kwa haki za kumiliki mali zilizofafanuliwa vyema na ni za kudumu kama sharti la kujiunga. Mbali na haki za wazi za kumiliki mali, taratibu za wazi za PES zinahitaji kuwepo mifumo ya kisasa ya kisheria na ya udhibiti. Kuwezesha sheria kuruhusu wahusika kuingia katika makubaliano ya malipo na mfumo wa kisheria wa kusimamia makubaliano ni sharti la jumla. Vile vile, fursa za maisha zinazohusisha ada za watumiaji zinahitaji kuwepo na uhalali wa kuwatoza wengine kwa matumizi ya eneo na inaweza kuhitajika kuwepo sheria katika ngazi ya eneo husika au kitaifa, pamoja na chombo halali kisheria kinachoweza kukusanya ada na kusimamia matumizi ya fedha hizo.[180]

Wataalamu wa uhifadhi wanaoshirikiana na Wazawa na wenyeji kuhusu ustawi wa binadamu na malengo ya kimazingira wanapaswa kufanya mapitio ya kina ya sera za mitaa, za kikabila, kimkoa na kitaifa kwa kufanya uchanganuzi wa hali zao wanapotengeneza mkakati. Hii inajumuisha

sera zinazotambua uhuru wa kujitawala wa wazawa na haki tofauti; kuainisha maeneo ya usimamizi wa rasilimali na maeneo ya kimamlaka; kuunda mamlaka za kiutawala, michakato inayohusisha wadau wengi, na taasisi wakilishi; na kuanzisha mifumo ya PES. Kwa ujuzi huu, wataalamu wa uhifadhi wana nafasi nzuri zaidi ya kubainisha muktadha wa sera unaofaa kwa uhifadhi kwa njia ya jamii, na endapo utetezi unahitajika kuimarisha mazingira wezeshi.

## Upanuzi na Uenezaji wa Uhifadhi

Changamoto inayokabiliwa na mashirika ya uhifadhi ni jinsi uhifadhi kwa njia ya jamii unavyoweza kuungwa mkono zaidi ya kiwango cha jamii ya mahali husika. Kupanua na kueneza uhifadhi kwa njia ya jamii ni muhimu kwa sababu: 1) kunawezesha Wazawa na wenyeji kujipanga katika makundi ili kushiriki katika utawala na maamuzi katika ngazi za kimkoa na kitaifa, na 2) kuhakikisha kwamba ukubwa wa kundi la utawala unalingana na ukubwa wa changamoto ya usimamizi wa maliasili.[187] Wazo la kujipanga huanzia katika ngazi ya chini, na ni muhimu kwamba vikundi vya kiutawala vinavyoibuka vinaungana na vile vilivyokuwa kwa viwango vikubwa, na kujengwa juu ya uaminifu uliokuwa umeanzishwa na kudumisha uhuru wao.[70] Kwa njia hii, wanaweza pia kuongeza uwezo wa vikundi vya utawala wa ngazi ya juu ili kudhibiti masuala ambayo yanaweza kuwa magumu katika ngazi ya mtaa, kama vile usimamizi wa mipaka na migogoro baina ya makundi.[187] Mazungumzo ya wadau wengi – yaliyojadiliwa katika sehemu iliyopita – ni njia muhimu ya kupanua na kueneza, kwani inatoa fursa kwa wazawa na wenyeji kushiriki katika utawala wa ngazi za juu na vikao vya kufanya maamuzi, kuonesha maarifa, na kusuluhisha migogoro.

Kueneza maana yake ni kuenea kwa uhifadhi kwa njia ya jamii kutoka kundi moja hadi jingine, na kuathiri eneo kubwa kwa kiwango kikubwa. Maandiko mengi kuhusu kueneza yanatokana na nadharia ya "kusambaa kwa uvumbuzi". Kwa kifupi, taarifa kuhusu mpango fulani hutawanywa kutoka kwa watumiaji waliofaulu hadi watumiaji watarajiwa kupitia ubadilishanaji wa mafunzo na ushawishi. Viwango vya kuasili mapema mara nyingi huwa hafifu kwa sababu idadi ndogo ya wapokeaji wa awali huzuia uenezaji wa taarifa. Ukuaji wa polepole wa awali baadaye hubadilika hadi kuwa ukuaji wa haraka, kwani idadi inayoongezeka ya watumiaji hushiriki uzoefu wao na kundi kubwa la watu wanaoweza kupitishwa. Kadiri muda unavyosonga, kasi ya utumiaji hupungua tena kadiri kundi la watu wenye uwezo na wanaokubali kutumia hupungua. Hatimaye, hatua ya kueneza inafikiwa ambapo watu wote walioufahamu mpango huo wameukubali, au wamekataa mpango huo katika muundo wake wa sasa.[182] Hata hivyo, ni vigumu kutabiri jinsi itakavyokuwa baada ya kuasili na jinsi uchukuaji utakavyotegemea viwango vya awali vya uchukuaji. Kwa hakika, utafiti wa hivi karibuni wa programu za uhifadhi kwa njia ya jamii haukupata mifano yoyote ya mipango iliyofanikisha utumiaji wa haraka na upitishwaji wa kiwango kikubwa, ukifichua tofauti kati ya kasi ya utumiaji na idadi ya mwisho ya watumiaji.[182] Hii inamaanisha kwamba matumizi makubwa huchukua muda, ambao unapatana na kile tunachojua kuhusu umuhimu na wakati wa kujenga uaminifu na mahusiano.

Viwango na mifumo ya uenezaji hutegemea mambo matatu muhimu: 1) sifa za usimamizi wa maliasili, 2) jamii zenyewe, na 3) muktadha.[188] Kwa mfano, kuenea kunatokea kwa haraka zaidi kwa mazoea rahisi ambayo yanalingana na maadili na imani za jamii, ambapo yanaweza kujaribiwa na kubadilishwa ili kuendana na muktadha wa mahali hapo, na ambapo faida ni kubwa. Kuenea pia kunatokea zaidi pale ambapo jamii tayari inafahamu kinachofanyika kwani zinakuwa zimeungamanishwa vyema na ulimwengu wa nje na kila mmoja, na panakuwa na ushindani wa kuja na mawazo mapya. Hatimaye,kuenea kwa uhifadhi kunatokea mahali palipo na mazingira wezeshi ya kisiasa, na ambapo muktadha wa kijiografia na kitamaduni unalingana vyema na taratibu za uhifadhi.[69,188-189]

**Jedwali la 8**: *Mifano ya shughuli za kusaidia uenezaji.*[69]

| Sababu Kuu za Uenezaji | Mfano wa Shughuli |
|---|---|
| Utaratibu wa usimamizi wa maliasili | Kusaidia muundo na utekelezaji wa taratibu za uhifadhi zinazolingana na maadili ya watu, mahitaji, na uzoefu wa kuishi; Kuunganisha na kujumuisha taarifa juu ya taratibu za uhifadhi kwa njia ambayo ni rahisi kuelewa na kutekeleza; Kuboresha mwonekano au kuhimiza jamii zitoe taarifa kuhusu taratibu hizo na matokeo yake ili kuwezesha jamii iweze |
| Jamii | Kuwezesha kubadilishana maarifa baina ya jamii juu ya fursa za usimamizi wa maliasili; Kusaidia maendeleo ya mitandao baina ya jumuiya na jumuiya zinazohusika na uhifadhi; Kuwezesha na kujenga uwezo wa majadiliano na wadau mbalimbali |
| Muktadha | Kusaidia kupitishwa kwa sheria ambayo inawezesha utekelezaji wa uhifadhi kwa njia ya jamii; Ikiwezekana, saidia utambuzi wa utangamano kati ya taratibu za uhifadhi na muktadham[m] |

Jedwali la 8 linaelezea baadhi ya hatua ambazo watendaji wa uhifadhi wanaweza kuchukua ili kusaidia kupanua na kueneza taratibu za uhifadhi kwa njia ya jamii. Usaidizi wa mitandao baina ya jumuiya na ubadilishanaji wa mafunzo vinastahili kuangaziwa kwa kuwa ni njia muhimu za kukuza upanuzi na uenezaji unaotokana na ujuzi dhabiti uliopo katika mashirika mengi ya uhifadhi. Tukirejea nyuma kuhusu nadharia ya "kusambaa kwa uvumbuzi", uwekezaji katika mitandao baina ya jamii na ubadilishanaji wa mafunzo huongeza uwezekano wa kuwa na watumiaji walioweza kukutana na watu wanaoweza kupitishwa na wanaoweza kubadilishana uzoefu, kuelimisha na kushawishi kuongeza kiwango cha usambaaji. Hivi ndivyo ilivyokuwa huko Amerika Kaskazini, ambapo Mtandao wa Wawaza wa Uzimaji Moto (IPBN) ulioanza mwaka wa 2015 ukiwa kwenye eneo moja la mababu wa Yurok, Hoopa, na Karuk ambayo ni makabila ya Kaskazini mwa California, na tangu wakati huo umekua na kujumuisha washiriki kutoka pueblos New Mexico, wasimamizi wa ardhi kutoka Ziwa la Leech maeneo ya Ojibwe huko Minnesota, makabila ya Klamath huko Oregon, na Kabila la Alabama-Coushatta huko Texas. IPBN ni mtandao wa usaidizi miongoni mwa jumuiya za wazawa wa Marekani ambao wanahuisha desturi zao za kitamaduni za kuzima moto kwa kuendana na mazingira ya sasa. Shughuli hizo ni pamoja na kupanga mikakati ya kufufua utamaduni wa kuzima moto, mafunzo kuhusu moto ikijumuisha sifa za shirikisho na uchomaji unaodhibitiwa kwa kuzingatia utamaduni, na kukuza mafunzo kati ya vizazi na vizazi. Hatua za kwanza mara nyingi hujumuisha watu kutoka kabila moja kutembelea eneo la watu wengine. Wengine hujihusisha kupitia matukio yanayohusu uhusiano wa kitamaduni wa masuala ya moto unaohusisha mafunzo ya moto. Ikijikita katika kujitawala, timu ya uongozi ya IPBN inaongoza ukuaji wa mtandao na kurekebisha muundo wa mtandao ili kuruhusu uwepo wa mandhari mpya za kikabila.

m. Zingatia kuwa baadhi ya masuala kimuktadha hayawezi kubadilishwa, kwa hiyo tathmini ya kiikolojia, na mazingira ya kisiasa na matumizi ya taratibu za kwenye mazingira zinapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya tathmini ya hali halisi.




# Chunguzi Kifani



## Uhifadhi wa Kudumu Kupitia Ahadi za Kisiasa, Uratibu wa Kikanda, na Fedha Endelevu nchini Micronesia.

Shindano la Micronesia linachukua maili za mraba milioni 2.5 (hekta milioni 1) za bahari, eneo ambalo linakaribia ukubwa wa bara la Marekani, na linasaidia takriban watu 450,000 katika visiwa 2,000, lugha 12 na maeneo ya kiutawala matano. Mnamo mwaka 2006, Watendaji Wakuu wa nchi tano na maeneo ya kiutawala katika ukanda kwa pamoja walitoa ahadi kwa Shindano la Mikronesia (MC) ya "kuhifadhi kwa ufanisi angalau asilimia 30 ya rasilimali za bahari zilizo karibu na ufukwe na asilimia 20 ya rasilimali za nchi kavu kote Mikronesia." Walipanga 2020 uwe ni mwaka wa kufikia lengo hili la pamoja, ambalo limechagiza juhudi za uhifadhi wa kikanda katika muongo mmoja uliopita.

### Ahadi ya Kisiasa ya Kikanda

Ahadi ya viongozi wa ngazi za juu wa kisiasa kwenye Shindano la Micronesia iliwezesha mataifa haya madogo, yaliyotawanyika, na ya visiwa vya mbali kuungana chini ya mpango unaofadhiliwa kwa pamoja ambao uliweza kutambulika duniani kote, uliweka msukumo wa dhamira ya kisiasa ya kuendeleza vipaumbele, na kuwezesha juhudi za pamoja (na za ushindani) za kufikia uhifadhi na kunufaika na uhifadhi. Ahadi hii imedumu katika vipindi tofauti vya kisiasa na kuwezesha mashirika na taasisi kutoa usaidizi bora wa kiufundi na kifedha kikanda kuliko kwa maeneo yao ya kiutawala. Maeneo matatu ya kiutawala kati ya matano yameanzisha Shindano la Micronesia kupitia sera, sheria au kanuni za Mtandao wa Maeneo y Hifadhi (PAN) na kuanzisha ofisi za PAN ili kuendeleza Shindano la Mikronesia. Maeneo mengine mawili yako chini ya Marekani na wametumia mbinu jumuishi ya usimamizi wa maeneo ya pwani inayowiana na sheria na mifumo ya Marekani.

**PICHA YA AIKONI**
MAENEO YA MFUMO WA VCA

**NCHI KAVU** **MAJI SAFI** **PWANI**

## Mifumo Endelevu ya Kifedha kwa Ngazi ya Kikanda na Kiutawala

Pamoja na ahadi za kisiasa katika uhifadhi, eneo lilianzishwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Micronesia (MCT) ulianzishwa kusimamia eneo hili. Mtazamo wa kikanda uliwezesha kujadiliwa kwa ada ya usimamizi ambayo iliweza kupunguzwa, na baadaye kukawa na njia mbalimbali za uwekezaji, ushirikiano na kujitolea kati ya watendaji wakuu ulidumishwa, na kupata ahadi za haraka za mashirika ya TNC na Conservation International (CI) ambazo zilijenga uaminifu katika jitihada zinazofanyika. Mipango endelevu ya fedha iliandaliwa kwa kila eneo ambalo lilibainisha vyanzo vilivyopo na vinavyowezekana vya ufadhili ikilinganishwa na jumla ya gharama za kuanzisha na za usimamizi ili kufikia malengo ya Shindano la Micronesia. Iliamuliwa kuwa pengo hilo lingeweza kujazwa na riba ya uwekezaji kutoka dola milioni 56 za wakfu ili kusaidia vyanzo vya ndani vitakavyoanzishwa au vilivyopo ndani ya eneo la kiutawala. Kufikia Desemba 2020, mfuko wa eneo ulikua hadi kufikia dola milioni 25.

Kila eneo la mamlaka limetekeleza majukumu kadhaa ili kupata fedha za ziada. Palau imeanzisha utaratibu wa kutoa fedha za Shindano la Micronesia kwa maeneo ya PAN, ambazo kwa kawaida zinasimamiwa na wenyeji, mashirika ya kijamii, au NGO, kama yanatimiza vigezo fulani. Ada ya Kijani ya Utalii ya Palau ilianzishwa ili kupata fedha za ziada. Mfumo kama huu unaandaliwa katika Maeneo ya Micronesia na Jamhuri ya Visiwa vya Marshall. Katika eneo lote, taratibu za ziada za fedha katika ngazi ya jamii zimeandaliwa katika maeneo mahususi ya mradi, kama vile hazina ya uhifadhi na urithi wa uhifadhi, na mikataba tisa ya uhifadhi wa "One Reef" ambayo huzishirikisha jamii zinazoshiriki kwa kuzipatia msaada wa kifedha kendeleza shughuli za usimamizi wa hifadhi za rasilimali za baharini.

Tangu kuzinduliwa kwa Shindano la Micronesia, makadirio ya kawaida yanaonesha kuwa washirika kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali (MCT na TNC) walichangia takribani dola milioni 45 kupitia mfuko wa fedha za ruzuku kusaidia utekelezaji wa Shindano ma Micronesia karika ukanda mzima, na mamlaka zilipata takribani dola milioni 17.5 kutokana na fedha za ruzuku pia.

## Maendeleo na Matokeo

Tathmini iliyofanyika mwaka 2020 ilibainisha fursa kadhaa za kuimarisha maendeleo na utekelezaji wa Shindano la Micronesia. Kwa mfano, uwekezaji mkubwa zaidi wa miundombinu ya Shindano la Micronesia ungeboresha uratibu wa ngazi ya kikanda, mawasiliano na ushirikiano. Hii ni pamoja na uongozi wa kiutendaji uliojitolea kwa ajili ya kuratibu, kuwa na vigezo na majukumu yaliyofafanuliwa kwa uwazi, michakato ya utawala iliyoimarishwa katika majukwaa ya kikanda, na mbinu iliyoratibiwa rasmi zaidi au mpango wa kukamilisha malengo ya Shindano la Micronesia kati ya mashirika yenye mamlaka, mashirika, na washirika. Zaidi ya hayo, mbinu za ziada za kupanga mipango ya kuanzia chini kabisa inaweza kuongeza ushiriki wa viongozi wa maeneo ya kiutawala—ikiwa ni pamoja na wabunge/baraza la mawaziri, uongozi wa wakala, na viongozi wa kimila—katika hatua ya kubuni na uzinduzi wa awali, kuimarisha uwianianishaji na vipaumbele vya jamii, na uanzishaji wa haraka wa Shindano la Micronesia katika mamlaka mbalimbali ya kiutawala.  Hatimaye, mfumo thabiti na wa uwazi zaidi wa kuripoti na mawasiliano yanayohusu  upatikanaji endelevu wa fedha unaotoa mapitio ya kila mwaka ya wakfu kwa kila eneo la kimamlaka, manufaa yaliyopatikana, na shughuli nyingine za kukusanya fedha na kukuza uwezo zinaweza kusaidia kushughulikia matatizo ya kutofikia malengo ya mipango endelevu ya fedha ndani ya eneo husika na kikanda.

*Masomo yaliyopatikana katika utafiti huu kifani yanatokana na tathmini ya Shindano la Micronesia iliyofanywa na mwandishi mkuu Meghan Gombos baada ya kufikia muda uliowekwa wa 2020. Chapisho la tathmini na muhtasari lilifadhiliwa na TNC na Jumuiya ya Eneo la Hifadhi la Visiwa vya Pasifiki, na linatokana na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Shindano la Micronesia.*

# Nyenzo na Rasilimali

## NYENZO YA 18: MWONGOZO—MWONGOZO WA FEDHA ZA UHIFADHI

Mwongozo wa Fedha wa Uhifadhi wa Muungano wa Uhifadhi wa Fedha (CFA's) unatoa maelezo ya kina kuhusu mifumo ya usimamizi wa fedha za uhifadhi; mwongozo wa kina wa namna ya kutekeleza baadhi ya taratibu za usimamizi wa fedha, ikiwemo nyenzo za kuwa na mipango ya kimkakati, upembuzi yakinifu, miundo ya usimamizi wa fedha, na taarifa za uthaminishaji wa rasilimali; na miongozo ya mipango ya biashara, kiolezo, na makavazi. Nyenzo za CFA zinatakiwa kutumika pamoja na Mfumo wa VCA na Mwongozo wa Haki za Binadamu wa TNC.

## NYENZO YA 19: UTAMBUZI—MAMBO MUHIMU NA MAZINGIRA WEZESHI KWA UPATIKANAJI ENDELEVU WA FEDHA

Idadi ya masuala wezeshi pamoja na vipengele vya mkakati na muundo ni muhimu kwa ajili ya kupata ufanisi wa fedha za uhifadhi wa Wazawa na wenyeji. Kwa kutoa majibu kwa kila kipengele kwenye orodha, watendaji wanaweza kutumia nyenzo hii kutathmini uwepo wa masharti haya muhimu ya uwezeshaji na vipengele vya ufadhili unaofaa. Kwa upande mwingine, hii inaweza kusaidia juhudi za kutathmini uwezekano wa fursa za ufadhili, kusaidia kutengenza muundo wa mikakati na mifumo ya kifedha, na kuamua vipaumbele ili kusaidia shughuli zinazofaa za kujenga uwezo kwa ushirikiano na Wazawa na wenyeji. Nyenzo hii itumike wakati wa majadilino na kwa kushirikiana na jamii, au wawakilishi wa taasisi, na wataalamu husika.

## Kiambatanisho

# Rasilimali za ziada

## Kupata haki za Ardhi, Maji na Rasilimali

### Alama

Jukwaa shirikishi la kimataifa la mtandaoni, linalosimamiwa na Taasisi ya Rasilimali Duniani (WRI) na Mpango wa Haki na Rasilimali (RRI) ili kutoa ramani na taarifa nyingine muhimu kuhusu ardhi ambayo ina milikiwa na kutumiwa na Wenyeji na jumuiya za wenyeji.Hii inajumuisha taarifa kuhusu umiliki rasmi dhidi ya umiliki usio rasmi, viashiria vya usalama wa kisheria wa ardhi, shinikizo la maendeleo na taarifa nyingine muhimu.

### Kielezo cha Kimataifa cha Haki za Kumiliki Mali (Prindex)

Kiashirio cha kimataifa cha mtazamo wa wananchi juu ya usalama wa haki za mali, mpango wa pamoja wa Muungano wa Kulinda Ardhi Duniani na Taasisi ya Maendeleo Ughaibuni unaokusudia kusimamia na kuhimiza utawala bora wa haki za kumiliki mali, na katika kuzingatia mitazamo, si lazima uakisi hali ya kisheria.

### Mwongozo kwa Wawezeshaji wa Ulinzi wa Ardhi ya jamii NAMATI: Uainishaji na Usajili wa Ardhi ya Jamii

Sehemu iliyoandikwa “Kuoanisha Mipaka na Kuweka Hati za Ardhi za jamii,” ukurasa wa 133-176. Sura hii inaelezea jinsi ya kusaidia jamii kutengeneza michoro shirikishi ya ramani za ardhi zao; kutatua migogoro ya mipaka na migogoro ya ardhi inayohusiana na ardhi zao; kisha kuandika mipaka iliyokubaliwa kwa aina mbalimbali za ushahidi halisi, ikiwa ni pamoja na mikataba iliyotiwa saini na majirani, miti ya mipaka au alama nyingine, na kuratibu eneo.

## Uongozi Thabiti, Utawala, na Uwezo wa Usimamizi

### Kadi ya Alama ya Jumuiya ya CARE (CSC) na Mbinu ya Uchambuzi wa Kijamii na Matendo (SAA)

Rasilimali hizi zilipendekezwa na sekta mbalimbali (afya, elimu, na maendeleo) wakaguzi wa Mfumo wa VCA na Mnyororo wa Matokeo na Msingi wa Ushahidi kama uwezavyo kuwa muhimu kwa programu kutumia mbinu ya uwajibikaji inayoendeshwa na jamii kwa ajili ya tathmini na uboreshaji wa utoaji wa programu (CSC); na mbinu shirikishi ya kuchunguza mambo ya kijamii ambayo yanaathiri vibaya wanajamii, kwa lengo la kukuza usawa wa kijinsia katika kubuni na utekelezaji wa programu (SAA). Mbinu kama hizo zinaweza kukuza uaminifu kati ya jamii na watendaji wa uhifadhi kwa kuangazia mambo muhimu ya kuzingatia kwa kubuni na utekelezaji wa mradi kama vile: Ni vipaumbele vya nani vinathaminiwa na kufanyiwa kazi? Je, kuna maelewano kuhusu vipaumbele kati ya chombo kizima cha wadau? Je, vipaumbele vilivyoainishwa vinahusiana na jamii kubwa zaidi? Je, vinajumuisha utofauti wa mahitaji na vipaumbele vinavyoelezwa? Je, vinakidhi mahitaji na maslahi ya watu waliotengwa zaidi na wasio na uwakilishi katika jamii?

### Mwongozo kwa Wawezeshaji wa Ulinzi wa Ardhi ya jamii NAMATI

Rasilimali hii ina mwongozo bora wa utendaji juu ya hatua nyingi zilizopendekezwa kwenye sehemu ya zana na rasilimali za kujenga uwezo (Nguzo ya 2), ikijumuisha jinsi ya kufanya kazi na viongozi wa jamii, kushirikisha wanawake na makundi yaliyotengwa, kufanya maono ya jamii, kusaidia kupanga matumizi ya ardhi, hati za ardhi za jamii, kutatua migogoro, na kufuatilia usajili na urasimishaji wa madai ya ardhi ya jamii.

### Tathmini ya Kitaasisi: Nyenzo ya Kuimarisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Licha ya kujenga uwezo wa jamii, TNC ina historia ndefu ya kusaidia uwezo wa mashirika ya kiraia ya ndani ya nchi na mashirika yasiyo ya faida ambayo kazi yao inaathiri moja kwa moja wazawa na wenyeji. Rasilimali hii inaweza kutumika kutathmini uwezo wetu na washirika wa mashirika ya kiraia na mashirika ya kujitolea, ikiwa ni pamoja na tathmini ya maono yao ya kimkakati na mipango, uongozi, usimamizi wa shirika, rasilimali watu, maendeleo ya rasilimali, usimamizi wa fedha, ujenzi wa eneo / ufikiaji, na uwezo wa mpango huu.

### Mradi wa Rasilimali za TNC za Minyororo ya Matokeo na Wenye Kuzingatia Ushahidi: Minyororo ya Matokeo Halisi na Maelezo kwa Ajili ya Nguzo Chaguliwa za Mfumo wa CVA

Rasilimali hii hutoa minyororo mitatu ya matokeo muhimu kwa ajili ya kujenga uwezo (pamoja na maisha endelevu), na ina maelezo ya ziada, orodha ya viashiria vinavyowezekana, na zana na nyenzo zilizopendekezwa za kutathmini na kuimarisha uaminifu ndani ya jamii (ukurasa wa 24-33) , pamoja na ufanisi wa viongozi wa jumuiya na taasisi (uk. 34-42).

### Nyenzo ya TNC ya Kujifanyia Tathmini ya Utawala

Rasilimali hii hutoa zana iliyotengenezwa na Timu ya TNC ya Australia Kaskazini kwa washirika wa jamii kutumia katika kutathmini ufanisi wa viongozi wa jamii na taasisi zao.

---

## Mazungumzo yenye Ufanisi ya Wadau Mbalimbali na Kufanya Maamuzi

### Mwongozo wa MSP: Jinsi ya Kuunda na Kuwezesha Ushirikiano wa Wadau Mbalimbali

Mwongozo unatoa mwelekeo wa kuunda na kuwezesha ushirikiano na wadau mbalimbali (MSP). Hiki si kitabu cha mapishi; badala yake, kinatoa muhtasari mpana. Uwezo wa mwongozo huu unatokana na mfumo wake wa msingi wa kuelewa na kuwezesha MSP. Mfumo huu unaunganisha nadharia na mazoezi na hutoa kanuni za kuongoza muundo wa MSP, vidokezo juu ya uwezeshaji, na seti ya zana za mchakato shirikishi.

### Mwongozo wa Ushirikiano wa Wadau Mbalimbali: Nyenzo Sitini za Kuwezesha Ushirikiano wa Wadau Mbalimbali

Kama mshirika wa Mwongozo wa ushirikiano wa wadau mbali mbali jinsi ya kubuni na kuwezesha ushirikiano na wadau mbali mbali, mwongozo huu unatoa zana 60 za mchakato zinazosaidia malengo tofauti yaliyoratibiwa na waandishi kama zile wanazoziona muhimu sana katika kusaidia michakato ya mwongozo wa ushirikiano.

### Kuelekea Mikataba Mipya ya Kijamii: Kutumia Michakato ya Mazungumzo ili Kukuza Mabadiliko ya Kijamii

Zana hii imeundwa ili kuchochea tafakari kuhusu uwezo na mipaka ya michakato ya wadau mbalimbali katika kukuza mabadiliko ya kijamii na kisiasa na kutoa zana na nyenzo za kazi ili kuwezesha matumizi ya michakato ya mazungumzo kwa njia mpya. Zana hii kimsingi inakusudiwa kwa asasi za kiraia, hususani mashirika madogo yanayofanya kazi katika ngazi za mtaa, na inataka kuongeza mtazamo wa asasi za kiraia katika mipango ya wadau mbalimbali. Inapatikana pia kwa kupakuliwa katika lugha ya Kifaransa, Kihispania na Kiarabu.

### Ushirikiano wa Sekta Mtambuka Kukabiliana na Uharibifu wa Misitu ya Kitropiki

Kiini cha nyaraka hii ni seti ya maswali ya uchunguzi ili kusaidia programu za mamlaka kubuni na kutathmini ushirikiano wa sekta mtambuka na usaidizi wake wa kina. Maswali yamegawanywa katika sehemu sita: hali ya awali, matokeo, mienendo ya ushirikiano, muundo wa ushirikiano, msaada wa kina, na uwajibikaji.

## Fursa Endelevu za Maisha

### Mipango Bora ya nchi

Mipango Sahihi ya Nchi (HCP) ni marekebisho ya Viwango vya Wazi (OS) vilivyotengenezwa kwa matumizi shirikishi na ya kitamaduni pamoja na wenyeji. Ili kuwezesha hili vyema, lugha ya Viwango Wazi imetafsiriwa kwa maneno rahisi zaidi, mfumo wa kuainisha vitu kwa rangi tofauti ulitumika, na chati mtiririko inayoonesha jinsi hatua zote zinavyolingana iliwekwa ili kutoa maelezo zaidi. Imetengenezwa na kujaribiwa karibu Australia yote , na miongoni mwa walimu wenye uzoefu wa kuitumia ni wa Waaustralia, lakini pia imetumika Amerika na Asia kwa mafanikio makubwa. Seti kamili ya faili za PowerPoint na mazoezi yanayohusiana ya kuendesha warsha ya mafunzo ya HCP yanaweza kupatikana hapo juu.

### Tathmini ya Biashara Zinazolenga Jamii Zinasaidia Fursa Endelevu za Maisha kwa Kushirikiana na Wazawa na Wenyeji

Lengo la utafiti huu lilikuwa kubainisha, kutathmini, na kuunganisha mafunzo tuliyojifunza kutoka kwenye mifano ya biashara zinazolenga jamii na uwekezaji unaosaidia shughuli za kiuchumi, ubinadamu na matokeo ya kimazingira kwa wazawa na wenyeji sehemu mbalimbali duniani. Mafunzo yaliyopatikana kutoka kwenye mifano hii yanatoa mwongozo wa kubuni na kufadhili miundo ya maisha ya jamii na kusaidia mashirika ambayo yanatafuta kuimarisha juhudi zilizopo au kuanzisha mipango mipya inayohusiana na mustakabali endelevu.

### Mwongozo wa Uboreshaji wa Maisha Endelevu na Mseto (SLED)

Mwongozo huu unatoa seti ya miongozo kwa watendaji wa maendeleo na uhifadhi ili kusaidia jamii katika kuimarisha na kubadilisha maisha yao. Mwongozo wa Uboreshaji wa Maisha Endelevu na Mseto hufanya hivi kwa kufanya kazi na wazawa na wenyeji ili kutambua na kuendeleza fursa za mabadiliko chanya katika maisha yao, kulingana na nguvu na uwezo wao, kwa kuangalia mambo ambayo husaidia na kuzuia mabadiliko ya maisha huku ikiakisi matarajio na matumaini ya watu hapo baadaye. Ingawa mbinu hii imeandikwa kwa kuzingatia miamba ya matumbawe na uvuvi wa pwani, inaweza kutumika kwa upana popote pale ambapo maliasili inakabiliwa na uharibifu kutokana na matumizi mabaya ya binadamu.

### Biashara za Jamii za Miti na Mazao ya Misitu– Mwongozo wa Uchambuzi na Maendeleo ya Soko na Miongozo ya Wawezeshaji wa Uwandani

Uchambuzi na Maendeleo ya Soko (MA&D) unafaa kwa biashara zinazotokana na bidhaa za maliasili zinazohitaji kulindwa au kuhifadhiwa, kwa sababu inaunganisha shughuli za usimamizi shirikishi wa maliasili na uhifadhi na fursa za kuzalisha mapato. MA&D inaweza kutoa wigo mpana wa kuelewa mifumo husika ya soko na hivyo kusaidia kuzuia kushindwa kwa biashara. Ingawa mbinu hiyo imeandikwa na misitu kama lengo, mbinu hiyo pia imetumika kwa mafanikio kwa miradi inayohusiana na utalii wa kijamii, mazao ya kilimo, mipango ya mifugo, na uvuvi.

### Jamii, Uhifadhi na Shughuli za kujikimu

Kitabu hiki kinaonyesha matokeo ya zaidi ya muongo mmoja wa tafiti zinazolenga jamii, uhifadhi, na maisha, kupitia Mtandao wa Utafiti wa Uhifadhi wa Jamii (CCRN), mpango wa kimataifa unaohusisha mashirika mbalimbali ya asili,kitaaluma, jamii na yasiyo ya kiserikali ( NGOs). Kama tutakavyoona katika kitabu hiki, miunganiko kati ya uhifadhi na shighuli za ujikimu hutokea ndani ya mifumo ya 'kijamii-ekolojia', yanatokana na maana tofauti na motisha ya uhifadhi, huathiriwa na masuala ya mamlaka na utawala, na kusababisha matokeo ya shughuli za kujikimu na viumbe hai.

### Mbinu Bora za Kushirikiana na Jamii Zinazotokana na Miradi ya Maendeleo ya Biashara: Mwongozo wa Ndani kuhusu Nini cha Kujifunza kwa Ajili ya Shirika la Uhifadhi wa Mazingira

Ripoti hii inakusudiwa kutumika kama hati ya mwongozo wa ndani kwa watendaji wa TNC ambao wanazingatia, au wanaoshiriki kikamilifu, katika miradi ya Maendeleo kupitia Usanifu na Mipango (DbD) au miradi mingine ya kijamii inayokabiliana na maendeleo yaliyopendekezwa au ya sasa. Ripoti hiyo ina sehemu nne za msingi zikiwemo (1) muhtasari wa misimamo na ahadi za Hifadhi kuhusu ustawi wa binadamu na ushirikishwaji wa jamii, (2) mapitio ya fasihi yaliyofupishwa yanayoangazia mbinu bora zinazotambulika za kushirikiana na jamii katika miradi inayoambana na uharibifu, (3) ) Tafiti za Uhifadhi ukitoa muhtasari wa uzoefu na mafunzo tuliyojifunza kuhusu kushirikiana na jamii wakati wa miradi ya maendeleo, na (4) mapendekezo ya jumla kwa watendaji wa uhifadhi kulingana na mapitio ya fasihi na uzoefu wa Uhifadhi.

## Manufaa, Athari na Ushirikishwaji

Mwongozo wa Kujifunza na Utekelezaji Shirikishi wa Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo kuhusu Bayoanuai na utamaduni: Kuchunguza itifaki za kijamii, haki na idhini. Angalia sehemu ya 16, ukurasa wa 179-183, kwa makala kuhusu "Kuelewa na kuwezesha mchakato wa itifaki ya jamii ya kitamaduni" na Holly Shrumm na Harry Jonas.

Mbali na awamu tatu za ushirikiano wa kijinsia katika hifadhi, wafanyakazi wa hifadhi wanapaswa kufahamu kuenea kwa unyanyasaji wa kijinsia duniani kote, na kufahamishwa jinsi ya kukabiliana, na pia jinsi ya kuchukua hatua ambazo hazitaleta au kuzidisha vurugu. IUCN na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani wana taarifa kuhusu **Unyanyasaji wa Kijinsia ni Nini?,** na RAINN inatoa maelezo kuhusu **Vidokezo vya Namna ya Kuzungumza na Waathirika wa Unyanyasaji wa Kijinsia.** Rasilimali zote mbili zinapatikana pia kwxa lugha ya Kiingereza, Kichina, Kifaransa, Kiindonesia, Kimongolia, Kireno, na Kihispania.

Kama ilivyosisitizwa katika waraka huu, kuchukua mtazamo wa kiutamaduni katika ushirikiano wa usawa wa kijinsia ni jambo la msingi, ikisisitiza umuhimu wa uchambuzi thabiti na shirikishi wa jinsia. Kuna nyenzo nyingine muhimu kuhusu mwitikio wa kitamaduni katika ujumuishaji wa usawa wa kijinsia pia, kwa mfano **Muhtasari wa Umoja wa Mataifa kuhusu Jinsia na wazawa**.

